

**MTINDO KWENYE NYIMBO ZA JADI KATIKA JAMII YA WAKISII NA
WASWAHILI WA NCHINI KENYA
STYLE AND STYLISTIC DEVICES IN THE TRADITIONAL SONGS OF THE
KISII AND THE SWAHILI OF KENYA**

OROKO KERUBO JUDITH


C50/CE/26750/2018

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

JUNE 2025

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijapata kuwasilishwa kwa mahitaji ya kutuzwa shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.


Sahihi.......... Tarehe: 20/6/2025.....

OROKO KERUBO JUDITH

C50/CE/26750/2018

MSIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yangu kama msimamizi.

Sahihi.......... Tarehe: 20/6/2025.....

DKT. JOSEPH JESSE MURIITHI

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili



TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa marehemu mama yangu Jelial Oroko na marehemu nyanya yangu Rosalia Oroko ambao walinielimisha kuhusu umuhimu wa kutia bidii katika jambo lolote maishani. Sitawasahau shangazi zangu ambao ni Irene Oroko na Catherine Nyaboke ambao walinihimiza niwe mvumilivu ijapokuwa safari hii ni ngumu.

SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumpa Mwenyezi Mungu shukrani zangu za dhiti kwa kipaji cha uhai na neema Zake nilizoshuhudia katia safari hii yangu ya elimu. Singetimiza jambo lolote masomoni bila uwepo na usaidizi wake. Wakati nilikumbwa na changamoto nyingi sana katika utafiti huu alikuwa kimbilio langu la pekee. Pili, ninamshukuru msimamizi wangu Dkt. Joseph Jesse Muriithi. Alinipa msaada, maelekezo, na mawaidha mufti tangu nilipoteua mada ya utafiti hadi sasa nimekamilisha utafiti wangu. Bila mwongozo na ushauri wake singeweza kukamilisha kazi hii. Kila nilipohitaji usaidizi wake alikuwa tayari. Pia siswezi kusahau ushauri niliopewa na wahadhiri wa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta kama vile Prof. Githinji ambaye ni mkuu wa idara, Dkt. Masinde, Dkt. B. Ngugi, Dkt. Osore, Dkt. P. Ngugi, Dkt. Wafula, Dkt. Munuku, Dkt. Chacha na wahadhiri wengine wote ambao sijawataja ambao walinisaidia kwa njia mbalimbali.

Sina budi kumshukuru mwanafunzi mwenzangu Doris Gakii ambaye tulianza safari hii ya kutwaa shahada ya uzamili pamoja. Nilipokaribia kukata tamaa alikuwa akiniambia kuwa “Heri mwisho wa jambo kuliko mwanzo wake.” Kando na hayo, mijadala ambayo tulikuwa tunafanya naye kila mara ilinipa mwongozo wa kuandika pendekezo la utafiti na hata uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Mathlan nawashukuru shangazi zangi Catherine Nyaboke na Irene Oroko ambao walinifaa kwa hali mali.

Hali kadhalika, ningependa kuwashukuru na wakaazi wa eneo la Kebirigo wakiongozwa na Mzee Maoga na wakaazi wa Mombasa katika eneo la Mvita hasa Likoni wakiongozwa na Mzee Bakari kwa kunipa fursa ya kukusanya data na pia kunielezea mambo mbalimbali ambayo yalifanikisha utafiti.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
MSIMAMIZI.....	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	xi
ABSTRACT.....	xii
UFAFANUZI WA ISTILAHU.....	v
UFAFANUZI WA AKRONIMU	x
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.2 Suala la Utafiti.....	5
1.3 Malengo ya Utafiti	5
1.4 Maswali ya Utafiti.....	6
1.5 Sababu za Kuchagua Mad.....	6
1.6 Upeo na mipaka.....	7
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	9
1.8 Misingi ya nadharia.....	11
1.8.1 Historia ya nadharia ya mtindo	11
1.8.2 Mihimili ya nadharia ya mtindo	14
1.9 Mbinu za utafiti	15
1.9.1 Muundo wa utafiti	15
1.9.2 Mahala pa utafiti.....	15
1.9.2.1 Maktabani.....	15
1.9.3 Sampuli na usampulishaji.....	17
1.9.4 Kurekodi	18

1.9.5 Uchanganuzi wa data.....	19
1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo.....	19
1.9.7 Maadili ya utafiti	20
SURA YA PILI.....	22
KUBAINISHA MCHANGO WA MBINU ZA MTINDO KWENYE NYIMBO ZA JADI KATIKA KUSAWIRI HISTORIA NA TAMADUNI ZA JAMII	
TEULE.....	22
2.0 Utangulizi	22
2.1 Historia na Tamaduni za Jamii ya Wakisii.....	23
2.1.1 Njaa	24
2.1.2 Vita vya Kwanza vya Dunia.....	28
2.1.3 Migogoro kati ya Wakisii na Majirani wao.....	30
2.1.4 Tohara.....	34
2.1.5 Ndoa.....	38
2.2 Historia na Tamaduni na Waswahili	42
2.2.1 Ndoa.....	43
2.2.2 Tohara.....	46
2.2.3 Taarabu	48
2.2.4 Sherehe za kuzaliwa kwa mtoto	51
2.2.5 Kanga/Leso	54
2.3 Hitimisho	56
SURA YA TATU.....	58
KUHAKIKI MBINU ZA MTINDO KWENYE NYIMBO ZA JADI ZA JAMII YA WAKISII NA WASWAHILI	
3.0 UTANGULIZI.....	58
3.2 Mbinu za Mtindo Katika Jamii ya Wakisii	59
3.1.1 Jazanda.....	59
3.1.2 Tashihisi/Uhaishaji	62

3.1.3 Taswira.....	65
3.1.4 Tashibihi.....	70
3.1.5 Takriri.....	72
3.1.6 Chuku.....	75
3.1.7 Kisengere Nyuma/ Mbinu Rejeshi	77
3.2 Mbinu za Mtindo Kwenye Nyimbo za Jadi za Jamii ya Waswahili	79
3.2.1 Taswira	79
3.2.2 Tashihisi.....	83
3.2.3 Jazanda	85
3.2.4 Kisengere Nyuma/Mbinu Rejeshi	89
3.2.5 Takriri	91
3.2.6 Chuku.....	94
3.2.7 Tashibihi/Tashbiha	95
3.2.8 Kinaya.....	97
3.3 Hitimisho.....	99
SURA YA NNE	100
KUCHUNGUZA JINSI AMBAVYO MBINU ZA MTINDO ZILIVYOTUMIWA	
KUFANIKISHA UWASILISHAJI WA MAUDHUI NA DHAMIRA YA	
NYIMBO TEULE	100
4.0 Utangulizi.....	100
4.1 Dhana ya Maudhui	100
4.2.0 Maudhui Katika Nyimbo za Jadi za Jamii ya Wakisii	101
4.2.1 Kazi.....	101
4.2.2 Mabadiliko.....	105
4.2.3 Migogoro	107
4.2.4 Ndoa.....	110
4.2.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii.....	114
4.2.6 Taasubi ya Kiume.....	118

4.2.7 Utamaushi.....	121
4.2.8 Kifo/Tanzia.....	123
4.3.0 Maudhui Katika Nyimbo za Jadi za Jamii ya Waswahili.....	126
4.3.1 Ndoa.....	127
4.3.2 Kifo/Tanzia.....	129
4.3.3 Malezi	131
4.3.4 Uwajibikaji	134
4.3.4 Nafasi ya Mwanamke kwenye Jamii.....	138
4.3.5 Dini	143
4.3.6 Mabadiliko	145
4.3.7 Nafasi ya Vijana kwenye Jamii	149
4.4 Hitimisho.....	153
SURA YA TANO	155
HITIMISHO	155
5.0 Utangulizi	155
5.2 Muhtasari wa Utafiti.....	155
5.3 Matokeo ya Utafiti	156
5.4 Mchango wa Utafiti.....	164
5.5 Matatizo ya Utafiti	165
5.5 Mapendekezo	166
MAREJELEO	167
VIAMBATISHO CHA KWANZA: Picha Za Utafiti	176
KIAMBATISHO CHA PILI: Nyimbo Za Jadi	186
NYIMBO ZA JADI ZA WAKISII	186
KIAMBATISHO CHA TATU: Nyimbo Za Jadi Za Waswahili.....	192
KIAMBATISHO CHA NNE: vibali ya utafiti.....	198
KIAMBATISHO CHA TANO: vibali ya kufanya utafiti.....	199

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Jadi:* Zamani au kutoka enzi na enzi
- Kanga:* Nguo nyepesi yenye nakshi na maandishi inayovaliwa na wanawake
- Mtindo:* Jinsi ya kufanya kazi kwa kufuata utaratibu
- Nyimbo:* Ni maneno yanatotamkwa kwa sauti ya muziki
- Nadharia:* Ni mwongozo, mawazo au maelezo ambayo yamepangwa kwa ajili ya kutumiwa katika kusuluhisha, kutekeleza au kufafanua, jambo fulani.
- Singa:* Suga mwili kwa kupaka mafuta na sandal ili uwe laini

UFAFANUZI WA AKRONIMU

- W.H.O.:** World Health Organization
- U.N.H.C.R.:** United Nations Human Rights Council
- N. I. H.:** National Institute of Health
- TUKI:** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
- NAT GEO:** National Geographic

IKISIRI

Mtindo ni uti wa mgongo katika tungo za kisanaa, iwe hadithi, tamthilia, ushairi na hata nyimbo. Utafiti huu umejikita katika kuhakiki mtindo kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na jamii ya Waswahili wa nchini Kenya. Watafiti mbalimbali wametafiti swala la mtindo katika nyimbo kama vile: Iyaya na wenzake (2021) walitafiti mtindo na lugha ya uwasilishaji katika nyimbo za nyiso za jamii ya Watachoni ambazo ni wenyeji wa Kenya. Muriuki (2013) alitafiti mtindo katika nyimbo za kazi katika jamii ya Warabai. Utafiti huu unatofautiana na tafiti za hapo awali hasa kwa msingi wa malengo na mambo mengine. Utafiti huu umefanikiwa katika: kubainisha jinsi ambavyo watunzi wametumia mbinu za mtindo katika kusawiri historian a tamaduni za jamii ya Wakisii na Waswahili wa nchini Kenya. Hali kadhalika, utafiti huu umehakiki mbinu za mtindo kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili. Mwisho kabisa, utafiti huu umefanikiwa kuchunguza jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilivyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika jamii teule. Nadharia ya mtindo ambayo iliasisiwa na Coombes ndiyo iliongoza utafiti huu. Coombes (1953) anasema kuwa mtindo huchunguza lugha na kanuni zinazoongoza lugha yenyewe ili kubainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa, sababu ya mbinu hizo kutumiwa na athari ya mbinu hizo katika kazi husika. Katika nadharia hii lazima mhakiki wa kazi yoyote ile ya fasihi achunguze vipengele hivyo na aelewe utendekazi wake. Waitifaki wengine ni kama Leech na Short (1981) ambapo wanasema kuwa nadharia hii ina lengo la kuelezea uhusiano uliopo baina ya lugha na majukumu ya kisanaa. Ambapo swali kuu ni mbona mwandishi akaamua kujieleza kwa njia fulani? Nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili zilizotumiwa katika utafiti ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya maksudi ambapo nyimbo zenye ukwasi wa mtindo ndizo zilizingatiwa. Utafiti hulifanywa makatabni na nyanjani. Maktabani ulihusisha kusoma vitabu, tasnifu, matini na majaida kuhusu mtindo. Nyanjani ulijumuhisha kuwahoji watu kumi wakongwe kutoka kila jamii na kila jinsia ikiwakilishwa na watu watano watano. Hali kadhalika, hadhira ambayo ilishiriki katika uimbaji isaliwa ambapo watu wawili wawili kutoka kila sherehe walishirikishwa na mwisho kabisa watu wanne kutoka kila jamii ambao waliongozwa katika uimbaji wa nyimbo hizo walishirikishwa katika utafiti. Wawili wawili kutoka kwa kila jinsia. Mbali na hayo, mbinu ya kusikiliza na kurekodi nyimbo hio za jadi ilitumiwa baada ya hapo uchambuzi ukaanza. Data ilichanganuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia, maswali na malengo ya utafiti. Kazi hii imepangwa katika sura tano. Utafiti huu uliweza kubainisha kuwa mbinu za mtindo zina nafasi kubwa katika kuendeleza nyimbo za jadi. Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika uwanaja wa fasihi simulizi kwa utawasadia wataalamu wa fasihi nawanafunzi wa fasihi kuchanganua na kuelewa mtindo katika nyimbo za jadi za jamii husika na pia katika kuhakiki mtindo katika tanzu zingine za fasihi simulizi.

ABSTRACT

Style is one of the major elements in any literary work, it can be in a story, a play, a poem or a song. This research embarked in analyzing and showing how styles and stylistics have been used in the traditional songs of the Abagusii people of Kebirigo and the Swahili people of Mvita. Various people have researched this area of statistics, they include: Iyaya et al (2021) researched on styles and stylistics and the mode of language used in the circumcision songs of the Atachoni people of Kenya. Muriuki (2013) researched styles and stylistics in work songs for the Arabai people. Finally, Wanjala (2007) looked at themes and the use of language on the Abukusu songs. Our research is different from those mentioned above in terms of aims and other areas. This research managed to determine how stylistic techniques have been used in depicting the history and culture of the Abagusii and the Swahili communities through the traditional songs. Similarly, this study managed to examine the stylistics in traditional songs of the Abagusii and Swahili communities. Finally, this study managed to successfully examine how stylistic were used to achieve the presentation of themes in the traditional communities in the selected communities. This research has been guided by the theory of Stylistics by Coombes. According to Coombes (1953) this theory endeavors in exploring how language is used to identify styles and stylistic used in the literary work, why they are being used and their effects on that work. Leech & Short (1981) demonstrates the value of stylistics in the analysis and interpretation of prose fiction, just as its companion volume. The researcher used purposive sampling in selecting the songs which gave her the data for the research. Data was collected from the library of Kenyatta University where it involved reading various theses that have dealt with songs more so on styles and stylistics and those research that have used the Stylistics theory. Secondly the researcher collected data from the field where she traveled to Kebirigo and Mvita to collect the required data on the month of November and December. The songs which have been used in this study were presented during their traditional ceremonies like traditional marriage and circumcision of the boys. The data was collected by listening to the songs and recording the traditional songs using a tape recorder and a mobile phone. Apart from the audio records the researcher wrote those songs using a paper and a pen which she used during analyzing the data as guided by the research questions, research aims, the principles of the stylistic theory and the research gap. The written songs have been attached on the theses for further reference and as evidence of the research. Data has been presented in a descriptive manner and also highlighting the examples where styles and stylistic devices have been used. The presentation of the data is depended on the research aims. This research will help literature students and literature teachers when it comes to analyzing styles and stylistics in any literary work. The findings have been presented in five chapters.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Nyimbo ni kipera mojawapo cha fasihi. Wataalamu mbalimbali wamefafanua maana ya nyimbo. Kwa mujibu wa Wamitila (2018), nyimbo ni tungo ambazo zina mahadhi ya sauti yanayoshuka na kupanda ambapo lugha ya mkato ndiyo hutumiwa katika kuunda tungo hizi, matumizi ya mpigo maalumu wa silabi na taswira. Nyimbo huwa na mpangilio uliofuata taratibu fulani au ambao una muwala ambao huchangia kuleta mapigo ya kimuziki au wizani. Kulingana na Kitula na Kisovi (2010), wimbo ni utungo ambao umepanga sauti, silabi, maneno, vipande na mishororo kwa kutumia mpangilio mahususi ambao una mahadhi ya kupanda na kushuka. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu.

Kwa mujibu wa Matei (2011), nyimbo ni tungo za kishairi ambazo zina mahadhi yanayopanda na yanayoshuka kupitia kwa mdundo wa kimuziki, muwala pamoja na sauti. Tungo hizi hupitishwa na kuwasilishwa kwa hadhira ambayo ni tendi kupitia kwa kuimba. Kuna sifa tatu kuu ambazo hutumiwa kutambulisha nyimbo, nazo ni: kuwepo kwa hadhira hai ambayo inaburudishwa, muziki unaoimbwa kwa sauti inayozingatia muziki maalum na kutumia ala tofauti za muziki kama vile: tarumbeta, kinubi, harimu pamoja na manyanya. Kwa upande mwingine Beja (2001), anafafanua wimbo kuwa ni kazi inayopatikana kwenye utanzu wa fasihi simulizi inayowasilisha taarifa kupitia kwa sauti na uchezeshaji viungo vya waimbaji. Mathalan Kitula na Kisovi (2010), nyimbo zinasambaa sana miongoni mwa jamii tofauti tofauti na huimbwa kwa kuingiliana na hafla na kazi tofautitofauti kama vile ugema, ujenzi wa majahazi au mitumbwi na uvuvi.

Wanafasihi wameainisha aina mbalimbali za nyimbo kwa kutumia vigezo tofauti kama vile: maudhui, muktadha na wahusika. Kulingana na Matei (2012), nyimbo zinaweka kuainishwa kwa kutumia kigezo kama vile maudhui ambapo kuna nyimbo mbalimbali zikiwemo: bembelezi, mbolezi na za mapenzi. Kwa kigezo cha wahusika ameanisha nyimbo mbalimbali zikiwemo: nyimbo na jandoni, za unyagoni, za sifo na za chekechea. Kwa kutumia kigezo cha muktadha ameanisha nyimbo kama vile: wawe, kimai, za maabadini, za kampeni na siasa, za kusifu na nyimbo za jadiya.

Kwa mjibu wa Wamitila (2018), nyimbo zimegawika katika aina tatu kuu: utanzu wa kitambiko/ibada ambao unahusisha bembelezi, nyimbo za arusi, sifo na nyimbo za sifa, jadi, mbolezi, nyimbo za utendaji kazi na sherehe mbalimbali. Kundi la pili huhusishwa zaidi na nyimbo za kimapenzi. Aina ya tatu huhusisha tendi na tenzi ambazo husimulia visa virefu vya kihistoria ambapo ametumia kigezo cha usimulizi. Kutokana na maelezo ya baadhi ya wataalamu wa fasihi nyimbo ambazo wameainisha ni kama zifuatazo: bembelezi, mbolezi, hodiya, sifo, mapenzi na jadiya. Utafiti huu umejikita katika kuchunguza nyimbo za jadi. Kulingana na Matei (2011), nyimbo za jadi ni nyimbo za kitamaduni ambazo zinaimbwa na kupitishwa kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kila jamii ina jadi ambazo hupokezwa kwa vizazi vyake. Kimaudhui, nyimbo hizi husimulia mambo mengi hasa yaliyotukia katika historia ya jamii kama vile matendo ya shujaa fulani, mateso, njaa na ucheshi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2018), wimbo wa jadi ni aina ya wimbo unaopatikana katika fasihi simulizi na ambao huwasilishwa kupitia kwa njia ya mdomo kutoka kizazi hadi kingine. Anaendelea kusema kuwa nyimbo za aina hii huwa katika jamii nyingi na huangazia mambo na matukio mbalimbali ambayo yalitokea katika enzi hizo.

Kwa jumla nyimbo za jadi ni nyimbo ambazo huimbwa na jamii fulani ambazo ni kiwakilishi cha utamaduni wa jamii hiyo pia zinahusu historia ya jamii husika. Nyimbo hizo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa mdomo ambapo pia zinaweza zikaandamana na ala za mbalimbali za muziki. Nyimbo hizi zaweza kuwasilishwa na mtu mmoja au kwenye kundi la watu wengi.

Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo mbalimbali kuhusu mbinu za kimtindo wataalamu hawa ni kama wafuatao: Senkoro (1982), anaeleza mtindo katika uwasilishaji au uandishi wa kazi yoyote ile fasihi ni jinsi ambavyo msanii hubuni utungo huo na kuupa muundo ambao kupitia kwa maudhui na kupitia kwa fani hudhihirisha arudhi au kawaida /sheria zilizozingatiwa au ni uwasilishaji wa maudhui na fani kwenye utunzi kipera chochote kile cha fasihi kwa mtindo ambao hudhihirisha ama huashiria nafsi na pia jinsi ambavyo mtunzi huyo anatofautiana na watunzi wengine kupitia kwa kazi hiyo.

Kwa mujibi wa Wamitila (2018), mtindo ni mbinu au sifa zote zinazoweza mtunzi kupitisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Hufafanua namna ambavyo mtunzi anavyoijenga kazi yake. Dhana hii inarejelea sifa maalum za mtunzi au hulka ya mtunzi fulani kudhihirika katika matumizi yake ya fani. Hulka hizo za mtunzi ni kama vile kuandika, sentensi, taswira, tamathali za semi, uakifishaji na uteuzi wa msamiati. Mtindo unapambanua msanii huyu na wasanii wenzake kufikia kiwango ambacho wewe kama mhakiki au msomaji wa kazi hiyo utatambua tu baada ya kusoma kuwa huo ni utunzi wa msanii, malenga au mtunzi mahususi kupitia kwa kuisoma tu. Wamitila anasema kuwa vipengele vifuatavyo ndivyo huangaziwa: matumizi ya lugha, dayolojia, usimulizi, toni na mandhari. Anaendelea kusema kuwa ni muhimu kujua kuwa mtindo fulani waweza kudhihirika katika kazi kadha za mtunzi mmoja au

pia kwa watunzi wa eneo fulani au katika kipindi fulani cha kihistoria kwa kuwa fani peke yake haitoshi kumtambulisha msanii. Mathalan ili kubainisha mtindo wa msanii fulani tunapaswa kuangalia: matumizi ya lugha, ploti, taswira au jazanda, tamathali za semi, ujenzi au usawiri na umuhimu wa wahusika, mandhari na uteuzi wa msamiati. Kulingana na Vuzo (2015), mtindo katika fasihi ni namna mwandishi anavyozea kuandika au kuitumia lugha kwa njia ya kipekee. Aidha, ni njia au namna ya kipekee inayotumiwa na mwandishi au mzungumzaji ambayo ndiyo inayomtofautisha na wengine. Mtindo wa mwandishi hueleweka zaidi wakati anapoitumia mitindo hiyo yake ya kipekee katika kazi nyingi. Kwa mfano: tabaini, lakabu, balagha, utohozi, tanakuzi na takriri.

Kuna baadhi ya tafiti ambazo zimeshughulikia mtindo kwa mfano: Ngugi (2018), alijikita kwenye maudhui ambayo yalishughulikiwa kwenye *Utenzi wa Haki za Watoto na Mashairi Bulbul* pamoja na mtindo ambao malenga alitumia ili kufanikisha uwailishaji wake. Maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto: Uchanganuzi wa *Utenzi wa Haki za Watoto na Mashairi Bulbul*. Muriuki (2013), alitafiti mtindo katika nyimbo za kazi ya jamii ya Warabai. Musyoka (2013), alitafiti jinsi ambavyo nyimbo zinazoimbwa wakati wa sherehe za mauko kwenye jamii ya Wakamba hutumia mtindo naye Wanjala (2007), alitafiti nyiso za Wabukusu ambapo alingazia maudhui na lugha.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia ni wazi kuwa kuna pengo ambalo lilipaswa kuzibwa kwa sababu nyimbo za jadi hususan za jamii ya Wakisii na Waswahili hazijatafitiwa katika mkabala wa mtindo ingawa watafiti mbalimbali wametafiti mbinu za kimtindo katika aina mbalimbali za nyimbo na vipera vingine vya fasihi. Hivyo basi ilihalisi utafiti kufanywa ili kuziba pengo lililopo katika nyimbo za jadi.

Mtafiti alinuia kuhakiki kwa kina mbinu za kimtindo katika jamii ya Wakisii na Waswahili wa nchini Kenya.

1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulihakiki mtindo kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili nchini Kenya. Nyimbo za jadi zimebeba historia, tamaduni na mila za jamii. Nyimbo hizi pia zimetumia mtindo kwa njia ambayo inasaidia kuelewa jamii vyema. Kuna baadhi ya tafiti ambazo zimefanywa kuhusiana na suala la mtindo katika nyimbo kama vile: Muriuki (2013) alitafiti mtindo nyimbo za kazi katika jamii ya Warabai, na Nyaga (2013) alitafiti mtindo unaodhihirika kwenye mashairi yaliyomo katika *Diwani ya Karne Moja*. Hata hivyo, kwa ufahamu wetu, nyimbo za jadi za jamii ya Waswahili na Wakisii hazijatafitiwa kwa mkabala huu. Hivyo basi utafiti huu ulikuwa na jukumu la kuchambua nyimbo hizi na kuweka wazi mtindo uliotumiwa katika nyimbo za jadi za jamii teule. Hali kadhalika, utafiti huu ulihakiki jinsi ambavyo watunzi walivyotumia mtindo katika kusawiri historia, tamaduni na maudhui katika nyimbo hizo.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo yafuatayo:

- i. Kubainisha mchango wa mbinu za mtindo kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili katika kusawiri historia na tamaduni za jamii hizo.
- ii. Kuhakiki mbinu za mtindo zilizotumiwa kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili wa nchini Kenya
- iii. Kuchunguza jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilivyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui na dhamira ya nyimbo teule.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulijibu maswali yafuatayo:

- i. Je, mbinu za mtindo zina mchango upi katika nyimbo za jadi katika kusawiri historia na tamaduni za jamii ya Wakisii na Waswahili wa Kenya?
- ii. Je, ni mbinu gani za mtindo ambazo zimetumiwa kwenye utunzi wa nyimbo za jadi kwenye jamii ya Wakisii na Waswahili wa nchini Kenya?
- iii. Je, watunzi wametumia vipi mbinu za mtindo katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui?

1.5 Sababu za Kuchagua Mad

Utafiti huu ulifanikiwa kuchunguza mtindo katika nyimbo za jadi katika jamii ya Wakisii na Waswahili nchini Kenya. Uamuzi wa kuchagua mada hii ulitokana na sababu kadhaa za kimsingi zilizojikita katika upungufu wa kitaaluma, umuhimu wa kifasihi, na mchango wa nyimbo hizi katika kuhifadhi tamaduni za jamii husika.

Kwanza, kipera cha nyimbo ni miongoni mwa vipera vya fasihi simulizi vinavyobeba utajiri mkubwa wa kijamii, kitamaduni, na kihistoria. Kuingana na Matei (2011), nyimbo zimeainishwa kwa vigezo vya muktadha, maudhui na wahusika, na hivyo kuchipua aina mbalimbali za nyimbo kama bembelezi, mbolezi, nyiso, kisiasa, sifo, kimai, wawe, mapenzi, chekechea na jadiiya. Kulingana na Wamitila (2018), nyimbo huweza pia kuainishwa kwa vigezo vya kitambiko, ibada na usimulizi, na kuhusisha aina nyingine kama nyimbo za harusi, tumbuizo, kazi, na tendi. Hii inaashiria kwamba nyimbo huchukua nafasi pana sana katika maisha ya jamii. Kupitia nyimbo, jamii huweza kuwasilisha mitazamo yao kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii kama vile siasa, uongozi, mapenzi, na maadili. Hii inaifanya nyimbo kuwa chombo muhimu cha kuelewa mienendo ya kijamii na kihistoria.

Pili, mtafiti aliona kuwa kuna upungufu mkubwa wa tafiti zilizojikita katika uchambuzi wa mtindo ya kisanaa katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili. Ingawa watafiti kama Serem (2018), walichunguza tamthilia za tafsiri, Silavwe (2016), alihakiki mtindo katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ya Edwin, na Ngugi (2018) alishughulikia mtindo na maudhui katika ushairi wa watoto, hakuna tafiti zilizolenga mitindo katika nyimbo za jadi kwa jamii hizi mbili kwa pamoja. Hili linaonyesha pengo la kitaaluma linalostahili kujazwa.

Tatu, jamii ya Wakisii na Waswahili ingawa zote ni za asili ya Kibantu, zina historia, maisha, na mazingira tofauti. Kwa hivyo, nyimbo za jadi kutoka kwa jamii hizi hutoa fursa nzuri ya kulinganisha matumizi ya mitindo ya kifasihi na namna zinavyosaidia kuwasilisha ujumbe. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mtindo ni mkondo au njia ambayo mtunzi huitumia kazi ya fasihi kuwasilisha ujumbe wake kupitia muundo wa sentensi, matumizi ya lugha na msamiati. Kwa hivyo, mtindo hauwezi kutenganishwa na ufanisi wa mawasiliano katika kazi ya fasihi.

Kwa msingi huu, mtafiti aliona umuhimu wa kuchunguza na kubainisha mitindo inayojitokeza katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili, pamoja na jinsi mitindo hiyo inavyosaidia kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo hizo. Utafiti huu hivyo basi unalenga kuchangia maarifa mapya katika fasihi simulizi ya Kiafrika, huku ukihifadhi na kuendeleza urithi wa jamii mbili muhimu nchini Kenya.

1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa mtindo katika nyimbo za jadi kutoka jamii mbili za Kibantu nchini Kenya: jamii ya Wakisii na jamii ya Waswahili. Uteuzi wa jamii hizi ulichangiwa na ukweli kuwa licha ya wote kuwa wa asili ya Kibantu, wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika historia, mandhari, na utamaduni. Hii iliibua

hitaji la kuhakiki mtindo unavyojitokeza katika nyimbo zao za jadi na mchango wake katika uwasilishaji wa ujumbe.

Kwa upande wa jamii ya Wakisii, utafiti uliendelezwa katika Kaunti ya Nyamira, hasa kijiji cha Kebirigo, ilhali kwa jamii ya Waswahili ulifanyika katika Kaunti ya Mombasa, eneo la Mvita. Maeneo haya yaliteuliwa kimaksudi kwa kuwa ni makao ya asili ya jamii husika ambapo nyimbo za jadi bado huimbwa katika shughuli za kijamii kama vile ndoa, tohara, mazishi, na katika sherehe za kuzaliwa kwa watoto.

Utafiti ulijikita katika kipera cha nyimbo za jadi pekee katika fasihi simulizi. Vipera vingine vya fasihi simulizi kama ngano, maigizo na mazungumzo havikuhusishwa. Lengo kuu la utafiti halikuwa tu kuchunguza maudhui ya nyimbo hizo bali kuelekeza macho kwa mtindo unaojitokeza, ambayo ni pamoja na matumizi ya taswira, takriri, tanakali za sauti, methali, tashbihi, jazanda na mpangilio wa mishororo. Uchanganuzi ulilenga kubaini jinsi mbinu hizi zinavyochangia uwasilishaji wa ujumbe.

Utafiti ulijikita katika nyimbo ishirini (20) tu, ambapo kumi (10) zilitoka kwa jamii ya Wakisii na kumi (10) kutoka kwa jamii ya Waswahili. Nyimbo hizi ziliteuliwa kwa njia ya usampulishaji lengwa kwa kuzingatia utajiri wa kimtindo na umuhimu wa muktadha wake katika maisha ya kijamii. Hali kadhalika, tafiti ulizingatia nyimbo za jadi ambazo bado zilikumbukwa au kutumika katika kipindi cha miongo michache iliyopita, ili kudumisha uhalisia wa data na uhusiano wa nyimbo hizo na jamii ya sasa.

Kwa sababu ya upana wa mada na changamoto za rasilimali (muda na fedha), utafiti huu haukuweza kujumuisha jamii nyingine za Kibantu nchini Kenya. Vilevile, nyimbo za kisasa na zile zenye athari kubwa za kigeni hazikujumuishwa, ili kudumisha usafi wa data ya jadi. Aidha, idadi ya washiriki walioshirikishwa

ilidhibitiwa hadi makundi maalum: wazee watano na akina mama watano kutoka kila jamii ambao ni wakongwe ndiyo walioteuliwa kushiriki katika utafiti. Waimbaji wawili wawili, na washiriki wa sherehe wawili wawili kutoka kila jamii na kila sherehe walishirikishwa kwa lengo la kuwakilisha kwa uwiano maarifa ya kimatamshi na kimuktadha.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti mbalimbali zimewahi kufanyika kuhusu mbinu za kimtindo katika vipera tofauti vya fasihi, zikiwemo riwaya, hadithi fupi, ushairi, tamthilia na nyimbo mbalimbali kama nyimbo za kazi, za mazishi, za taarabu, na za bembelezi. Hata hivyo, hakuna utafiti ulioangazia kwa kina matumizi ya mtindo katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili, hivyo basi utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo.

Iyaya na wenzake (2021), walitafiti mtindo na lugha katika nyimbo za jando za Watachoni, wakitumia nadharia ya baada ya umuundo na ubabe-dume. Ingawa utafiti huu ulichangia katika kuelewa matumizi ya lugha katika nyimbo, ulilenga zaidi uwasilishaji wa nyimbo (maghani, maigizo, n.k.) badala ya mbinu za mtindo, hivyo unatofautiana na utafiti huu. Hali kadhalika, Musyoka (2012), alichunguza mtindo katika nyimbo za mazishi miongoni mwa Wakamba. Alionyesha tamathali za usemi kama chombo cha kuwasilisha ujumbe wa imani kuhusu mauti. Alitumia nadharia ya mtindo na ethnografia ya mawasiliano. Ingawa alishughulikia nyimbo za jadi, alijikita katika nyimbo za mazishi za Kikristo na si nyimbo za jadi za kidini au kijadi kama utafiti huu. Utafiti huu unatofautiana na utafiti weti kwa sababu walichunguza nyimbo za Wakamba. Hali kadhalika, walitumia nadharia ya Ethnografia ila utafiti huu ulitufaa sana katika kuelewa nadharia ya mtindo.

Naye Mboti (2012), alihusisha mtindo katika nyimbo za michezo ya chekechea kwa watoto wa darasa la kwanza. Licha ya kuwepo kwa tamathali za semi na uchanganuzi wa kijinsia wa nyimbo, tafiti hizi zina tofauti na huu kwa kuwa haziangalii nyimbo za jadi za watu wazima katika jamii husika. Hali kadhalika, Gitonga (2017), alilinganisha fani na maudhui kwenye nyimbo za ndoa miongoni mwa Wameru na Waswahili. Ingawa kulikuwa na mguso wa mtindo, mwelekeo wa utafiti wake ulikuwa wa kimfumo katika kulinganisha jamii mbili. Utafiti huu wa sasa unazama kwa undani katika mbinu za kimtindo katika nyimbo za jamii hizo kwa mtazamo wa ndani.

Ngugi (2018), alichunguza maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto, akitumia nadharia ya uhalisia na ya mtindo. Ingawa anachambua mbinu za kimtindo, kazi yake ililenga ushairi wa watoto, tofauti na utafiti huu unaojikita kwenye nyimbo za jadi. Serem (2018), alilinganisha fani katika tafsiri mbili za tamthilia ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Utafiti huu ulichangia kuelewa matumizi ya msamiati kama kipengele cha kimtindo, lakini ulilenga tafsiri za kazi andishi.

Licha ya hayo, Mining (2016), alibainisha mbinu za kimtindo katika hadithi fupi kutoka diwani ya Pendo la Heba na Mayai Waziri wa Maradhi. Mitindo kama taswira, tashihisi, majazi na tashbihi zilichanganuliwa. Japokuwa utafiti wake ulifaa kuelewa nadharia ya mtindo, muktadha wake ni wa hadithi fupi, si wa nyimbo za jadi. Kwa upande mwingine, Mungai (2014), alichunguza fani katika nyimbo za Bi. Anastacia Mukabwa kwenye albamu *Kiatu Kivue*. Alitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Ingawa utafiti huu ulihusisha nyimbo, ulikuwa wa nyimbo za maabadini na si nyimbo za jadi kama utafiti huu. Muriuki (2013), naye alitathmini mtindo katika nyimbo za kazi za Warabai, akiongozwa na nadharia ya kimtindo. Utafiti wake uliongeza uelewa wa nadharia ya mtindo na ulivutia kwa kuwa ulijikita katika nyimbo za jadi, sawa na

utafiti huu, japokuwa ulilenga jamii tofauti. Wanjala (2007), alichunguza nyimbo za tohara (nyiso) za Wabukusu, akitumia nadharia ya ethnografia ya mawasiliano na uamilifu. Utafiti huu una ulinganifu wa karibu na huu kwa kuchunguza nyimbo za jadi, lakini utafiti huu mpya unaangalia jamii mbili tofauti (Wakisii na Waswahili) na unajikita zaidi katika mbinu za mtindo.

Kutokana na mapitio haya, ni wazi kwamba kuna pengo katika tafiti zilizotangulia kuhusu matumizi ya mtindo katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili. Wengi wa watafiti waliangazia nyimbo za jamii nyingine au vipera tofauti vya fasihi, huku baadhi wakijikita zaidi katika maudhui au fani kwa ujumla badala ya kuchambua kwa kina mbinu za kimtindo katika nyimbo za jadi. Utafiti huu unalenga kujaza pengo hilo kwa kuchunguza mbinu za kimtindo katika nyimbo za jadi za jamii hizi mbili, kwa kutumia nadharia ya mtindo kama msingi wa uchanganuzi wake.

1.8 Misingi ya nadharia

Kwa mjibu wa Wamitila (2003), nadharia ni mafikira, maelezo, maoni au mwongozo unaowasilishwa kupitia kwa mtindo maalum ili upige jeki, usuluhishe au utekeleze suala fulani. Hali kadhalika Wafula (2004) anasema kuwa nadharia ni mwongozo wa mikakati ya jinsi mtu anavyostahili kusoma kazi ya fasihi na huchukua nafasi ya dira kwenye kuchambua na kufanya uamuzi unaohitajika kuhusu kazi hiyo. Kwa jumla nadharia ni kanuni ama mwongozo unaotoa mwelekeo wa jinsi ya kuhakiki kazi mbalimbali za kifasihi.

1.8.1 Historia ya nadharia ya mtindo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia hii inaeleza kuwa ili utungo wowote wa fasihi ukamilike na ueleweke na wasomaji ni lazima mtunzi atumie lugha. Lugha hii ndiyo itaathiri watu watakaotagusana na kazi

yenyewe mbali na vipengele vingine vilivyo kwenye kazi hiyo. Nadharia hii iliasisiwa na Coombes (1953), ambapo alisema kuwa mtindo huchunguza lugha na kanuni zinaazoongoza lugha yenyewe ili kubainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa, sababu ya mbinu hizo kutumiwa na athari ya mbinu hizo katika kazi husika. Katika nadharia hii lazima mhakiki wa kazi yoyote ile ya fasihi achunguze vipengele hivyo na aelewe utendakazi wake. Nadharia hii ilitufaa sana katika utafiti huu kwani ilitusaidia kuelewa mtindo kwenye nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili. Nadharia hii iliendelezwa na Leech (1969, ambapo alieleza kuwa nadharia ya mtindo ni mwongozo muhimu sana katika uchunguzi wa jinsi ambavyo lugha inatumiwa katika fasihi, jinsi mwandishi anvyoitumia na kuipanga lugha yake, kipindi fulani cha wakati, utanzu fulani au hata katika ushairi. Anachukua mtindo dhahiri wa kiisimu katika kufafanua dhana ya lahaja na sajili na kufafanua jinsi ambavyo ushairi unatumia aina mbalimbali ambazo si za kimaandishi. Anaendelea kusema kuwa fasihi haiwezi kuchanganuliwa bila kuangazia jinsi ambavyo lugha imetumiwa katika kazi yenyewe. Fasihi inakusudia kutumia lugha kwa kiwango cha hali ya juu ili kuwasilisha hisia, ujumbe au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji.

Hali kadhalika, Crystal na Davy (1969), walieleza kuwa mtindo ni jinsi ambavyo mtu au jamii ina mazoea ya kutumia lugha pia mtindo unaangazia jinsi ambavyo mtu binafsi ana hulka ya kutumia lugha na hulka hiyo inamtofautisha na watu wengine. Muasisi mwingine ni Bloomfield (1976), ambaye amechangia katika nadharia hii kwa kusema kuwa ni uchunguzi na ufasiri wa elementi za lugha kwa maandishi, utunzi wa makundi ama ujumbe. Anaendelea kueleza kuwa dhana ya mtindo si dhahiri kwa sababu inapishana na taaluma nyingine kama vile uhakiki wa kimaandishi, kiisimu na usemi.

Kulingana na Leech na Short (1981), nadharia hii ina lengo la kueleza uhusiano uliopo baina ya lugha na majukumu ya kisanaa. Kulingana na wao swali kuu ambalo pia ndilo muhimu sana ni mbona mwandishi fulani akaamua kujieleza kwa njia fulani? Lakini kwa mhakiki yeyote wa fasihi swali kuu litakuwa jinsi gani mtunzi amefikia kiwango fulani katika uandishi kupitia kwa matumizi yake ya lugha. Wawili hawa wameegemeza mawazo yao kwa mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand de Saussure kwa dhana za *Parole* pamoja na *Langue*. *Langue* ni mfumo wa kinadharia wa lugha ambao unatumiawa na jamii fulani pia ni jumla ya ishara za maneno zilizo katika akili ya mtumiaji wa lugha. *Parole* ni jinsi lugha inavyotumiwa. Ni matamshi halisi yanavyotolewa na mtu binafsi. Nadharia hii inasaidia kuelewa jinsi ambavyo lugha ilivyotumiwa katika muktadha fulani na mtu fulani. Inasisitiza katika upekee wa kimitindo ambao mtunzi au msemaji ameamua kutumia na hii ndio inadhihirisha matumizi ya kiisimu katika kazi za kimaandishi. Wanendelea kueleza kuwa matumizi ya lugha katika kazi yoyote hujikita katika muktadha maalum. Hivyo ili kuelewa lugha ambayo inatumiawa ni lazima msomaji au msikilizaji aelewe muktadha wa kazi yenyewe ili kuifasiri kwa njia inayofaa.

Ngara (1982) anaeleza kuwa nadharia hii hushughulikia Isimu na Fasihi. Anaeleza mtindo kuwa ni njia ya mtunzi kuwasilisha mawazo yake kupitia kwa lugha, yaani jinsi ambavyo mtunzi wa kazi yoyote anavyojieleza kupitia kwa lugha aliyoitumia ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Mihimili ambayo Ngara ameorodhesha inafanana na ya Leech (1969). Simpson (2004) anasema kuwa nadharia ya mtindo hufafanua kuwa kazi yoyote ya fasihi ina kiwango kikuu cha ubunifu na wakati inapohakikiwa kwa kina humuwezesha msomaji kuelewa matini kwa ndani au kina zaidi matini au kazi husika. Kwa mujibu wa Jeffries (2017), nadharia hii ilianzishwa kule Urusi katika karne ya ishirini, huu ulikuwa ni mtindo tofauti wa kusoma kazi

zozote zile za fasihi ikilinganishwa na katika karne ya zilizotangulia ambapo uhakiki na kusoma kazi za fasihi uliangazia mwandishi badala ya kuangazia kazi husika.

1.8.2 Mihimili ya nadharia ya mtindo

Mihimili ambayo iliongoza utafiti huu ni kama ifuatayo kulingana na Leech (1969)

- i. Kiwango cha utambuzi ambacho kinashughulikia jinsi ya kutamka na kuandika mitindo mbalimbali ya lugha. Kiwango hiki kinajikita katika fonolojia (mfumo wa sauti katika lugha) ambapo rithimu, shadda na toni zinaangaziwa. Mhimili huu ulisaidia katika kutambua na kuelewa mbinu za mtindo zilizotumiwa na watunzi katika nyimbo teule. Hali kadhalika, ulisaidia katika kuelewa ujumbe ulipitishwa kupitia kwa mbinu hizo.
- ii. Kiwango cha umbo ambapo msamiati utaangaziwa na jinsi msamiati huu utatumiwa katika kutunga sentensi sahihi. Kiwango hiki kinaangazia jinsi ambavyo mtunzi anateua msamiati unaotumia vipashio vya lugha vimepengwa ili kuzua maana inayokusudiwa.
- iii. Kiwango cha semantiki ambacho kinashughulikia maana inayoibuliwa na lugha ambayo mtunzi ameamua kutumia. Mhimili huu utasaidia katika kuelewa ujumbe ambao unawasilishwa na mtunzi kupitia kwa mbinu za kimtindo zilizotumiwa na mtunzi.
- iv. Kiwango cha utendakazi. Kiwango hiki kinaangazia jukumu la mtindo fulani ameamua kuutumia katika lugha yake. Mhimili huu ulisaidia kuelewa jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilivyochochea uwasilishaji wa maudhui kama vile uwajibikaji, nafasi ya mwanamke katika jamii, taasubi ya kiume na malezi. Mihimili hii ndiyo ilichukua nafasi muhimu sana katika kutafiti mbinu za kimtindo katika jamii ya Wakisii na Waswahili.

1.9 Mbinu za utafiti

Sehemu hii ilishughulikia mbinu ambazo zilitumiwa kufanikisha utafiti huu. Mbinu hizi ziligawika katika makundi yafuatayo: muundo ambao utafiti huu ulizingatia, mahali ambapo utafiti ulifanyika, usampulishaji pamoja na sampuli, jinsi ambavyo data ilikusanywa na uchambuzi ambao ulipfuata baada ya data iliyohitajika kukusanywa.

1.9.1 Muundo wa utafiti

Kulingana na Maheswari (2017), muundo wa utafiti ni mwongozo rasmi wa jinsi mtafiti anastahili kufanya kazi yake. Unatoa mchakato wote ambao mtafiti anastahili kufuata, data ambayo mkusanyaji atakusanya na jinsi ambavyo data yenyewe itakavyochanganuliwa.

Kwa mujibu wa Bickman na Rog (2004), muundo wa utafiti ni mikakati ya kijumla ambayo mtafiti ameamua kutumia katika mchakato wa utafiti ili kumsaidia kupata majibu ya maswali.

Utafiti huu ni wa kimaelezo ambapo mtafiti atahakiki mbinu za kimtindo katika nyimbo za jadi kwenye jamii ya Waswahili na Wakisii.

1.9.2 Mahala pa utafiti

Utafiti huu uliendelezwa nyanjani na makatabani, ambapo data ya kimsingi ilitokana na utafiti wa nyanjani. Awamu ya kwanza ya utafiti ilifanyika maktabani kisha awamu ya pili ilifanyika nyanjani.

1.9.2.1 Maktabani

Mtafiti alisoma vitabu, majarida, tasnifu na makala mbalimbali ambayo yalishughulikia nyimbo hasa katika kipengele cha mtindo na pia kazi zilizoshughulikia mtindo hasa kwa kutumia nadharia ya umtindo. Kutokana na

kusoma kazi hizi, mtafiti alielewa zaidi jinsi ambavyo mbinu za kimtindo zilitumiwa katika nyimbo na matumizi ya nadharia ya mtindo katika uhakiki wa kazi za kifasihi.

1.9.2.2 Nyanjani

Data ya kimsingi ni ya nyanjani ambapo utafiti uliendelezwa kwenye jamii mbili. Jamii ya kwanza ni ya Wakisii ambapo utafiti ulifanyika katika eneo la Kebirigo kaunti ya Nyamira na katika jamii ya Waswahili utafiti uliendelezwa katika eneo la Mvita kwenye kaunti ya Mombasa.

Mtafiti alisafiri hadi eneo la Kebirigo na baadaye katika eneo la Mvita. Katika maeneo hayo mawili, mtafiti alihudhuria na kushiriki katika uimbaji wa sherehe za kitamaduni za jamii hizo ambapo nyimbo za jadi ziliimbwa. Sherehe hizo ni kama zifuatazo: sherehe za arusi au ndoa za kitamaduni, sherehe za kupeleka watoto wa kiume jandoni, sherehe za mazishi na kusherehekea kuzaliwa kwa mtoto pia wakati wa mavuno.

Kando na hayo, mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano, kusikiliza, kuchunguza na kurekodi nyimbo husika katika kila sherehe ili kupata data anayohitaji. Alizierekodi kwa simu ya rununu na kupiga picha kisha akachanganua baadaye kwa kuongozwa na malengo na maswali ya utafiti. Mtafiti alisaili watu mbalimbali kuhusiana na nyimbo za jadi. Kwanza alisaili watu wakongwe kumi kutoka kila jamii ambapo watano walikuwa ni wa jinsia ya kiume na watano walikuwa wa jinsia ya kike. Watu hawa waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu kwa sababu walikuwa na ujuzi mwingi sana kuhusiana na nyimbo za jadi na kwa kuwa walikuwa wameshiriki katika uimbaji wake kwa muda mrefu sana. Jamii ya Wakisii walikuwa ni wafuatao: Mzee Maoga, Erodion Mayaka, James Ombuya, Mzee Charles Onyancha, Mzee Nyakweba, Mary Kwamboka, Ruth Mokeira, Rachel Mong'ina, Teresia Bangweso na Anna Onchari.

Kwa upande mwingine, jamii ya Waswahili ilihusisha wafuatao: Mzee Bakari Kombo, Bw. Salim Swaleh, Bw. Juma Hamisi, Mzee Abdi na Bw. Mkombozi, Bi. Mwanaisha, Bi. Hadija, Bi Saida, Bi. Pendo Hamisi, Bi. Amani Fadhili. Hali kadhalika, hadhira iliyoshiriki katika sherehe hizo pia ilishiriki katika utafiti ambapo alisaili watu wawili wawili katika kila sherehe ya jamii mbili husika kisha alisaili wafuatao kwani waliongoza katika uimbaji: Nancy Kemunto, Jane Bochaberi, Douglas Onwong'a, Evans Makambo kwa jamii ya Wakisii na Mwanaheri Aisha, Mwanahamdi Juma, Riziki Hamisi, Juma Mamboleo, Salim Musa ambao ni wa jamii ya Waswahili.

1.9.3 Sampuli na usampulishaji

Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003), sampuli ni mchakato wa kuchagua asilimia fulani ya watu ambapo idadi iliyoteuliwa itawakilisha kikundi kikubwa. Wanaendelea kusema kuwa, sababu kuu ya kuteua sampuli ni kuwa mtafiti akiamua kutumia idadi yote itamwia vigumu katika kupata data anayohitaji kwa sababu itachukua muda mwingi na itamgharimu kiasi kikubwa cha fedha. Kulingana na Osuala (2007), usampulishaji ni ile hali ya kuchukua sehemu ya kitu au watu kutoka kwa kikundi kikubwa ili vitu hivi ama watu hawa wawakilishe kikundi kikubwa.

Kwa mujibu wa McCombes (2022), mtafiti anapofanya utafiti ni vigumu au ni nadra sana kukusanya data kutoka kwa kila mtu kwenye kikundi husika, mtafiti huyo atateua watu wachache ambao watawakilisha kikundi hicho. Hivyo basi sampuli ni kikundi kidogo cha watu ambacho kimeteuliwa na mtafiti kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kishiriki katika utafiti husika. Kikundi hiki kitampa mtafiti data anayohitaji katika kufanikisha utafiti wake.

Sekaran (2013) anaeleza kuwa mtafiti hapaswi kuteua sampuli kubwa kwa sababu asilimia ya makosa itaongezeka. Hivyo basi mtafiti anahitaji kuteua sampuli ndogo lakini iwe kiwakilishi tosha cha kikundi kikubwa.

Nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii katika eneo la Kebirigo na jamii ya Waswahili katika eneo la Mvita ndizo zilitafitiwa. Nyimbo hizi huimbwa hasa wakati wa sherehe za kitamaduni kama vile harusi na ndoa za kitamaduni na wakati wanapowapeleka wavulana jandoni. Nyimbo hizi huimbwa pia hasa wakati wa sherehe za mazishi, kuzaliwa kwa watoto na hata wakati wa mavuno. Mtafiti aliteua sampuli kwa kutumia mtindo wa kimaksudi ambapo nyimbo kumi ziliteuliwa kutoka kwa kila jamii. Nyimbo hizi ziliteuliwa kwa kuwa zilikidhi malengo ya utafiti. Nyimbo mbili za sherehe ya ndoa, mbili za sherehe ya mazishi, mbili za sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto na mbili za kusherehekea mvauno au nyimbo za kazi kutoka kwa jamii hizo mbili ziliteuliwa. Watu wakongwe, hadhira na waliongoza katika uimbaji wa nyimbo zenyewe ndio waliohojiwa kwa sababu walikuwa na ujuzi wa nyimbo hizo za jadi.

1.9.4 Kurekodi

Utafiti huu ulifanyika kati wa mwezi wa Novemba na Desemba ambapo ndio wakati sherehe hizi za kitamaduni hufanyika katika jamii hizi. Hivyo, kwa kutumia tepu rekoda na simu ya rununu, mtafiti alirekodi nyimbo mbalimbali za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili katika eneo la Kebirigo na Mvita wakati wa uwasilishaji wa nyimbo zenyewe. Kurekodi nyimbo hizi kulimsaidia mtafiti kwani kuzichanganua na kuzichunguza nyimbo zenyewe mshororo kwa mshororo kwa kutumia na malengo ambayo utafiti huu ulinuia kufikia pamoja na maswali husika.

1.9.5 Uchanganuzi wa data

Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza kuwa data iliyokusanywa lazima ipangwe kwa utaratibu ambao unafaa ili uchanganuzi wa data yenyewe uwe rahisi. Uchanganuzi hutegemea ikiwa ni wa kihesabu au ni wa kimaelezo. Baada ya utafiti wa nyanjani na mkatbani, mtafiti alizamia katika kuchanganua data aliyokusanya kutoka maktabani na nyanjani. Uchanganuzi huu uliongozwa na maswali, malengo, pengo na mihimili ya nadharia ya utafiti.

Lengo kuu lilikuwa kueleza matumizi ya mbinu za kimtindo katika nyimbo za jadi, kuonyesha jinsi mbinu za kimtindo zilivyotumiwa katika kuendeleza maudhui ya nyimbo za jadi katika jamii husika na kuonyesha mwingiliano na tofauti ya mbinu za kimtindo katika jamii hizi. Kimsingi uchanganuzi wa data ya nyanjani ulianza kwa kurekodi nyimbo zenyewe kwenye tepu rekoda na kwenye simu, kisha mtafiti akaichanganua data yenyewe na kuinakili yake na pia nyimbo hizo zimeambatishwa kwenye tasnifu hii.

1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya utafiti ambayo yalitokana na data iliyokusanywa yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari. Mpangilio wa uwasilishaji umezingatia malengo ya utafiti. Matokeo haya yamepangwa kwa njia inayofaa. Matokeo haya yamepangwa kwa sura tano. Sura ya kwanza inahusu msingi wa utafiti huu, sura ya pili imeshughulikia jinsi ambavyo mbinu za kimtindo zilivyotumiwa katika kusawiri historia ya jamii teule. Sura ya tatau ilishughulikia mbinu za mtindo katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili, sura ya nne imelenga mchango wa mtindo katika kuendeleza maudhui katika nyimbo husika. Mwisho kabisa, sura ya tano

imeshughulikia muhtasari wa utafiti wenyewe, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti Zaidi.

1.9.7 Maadili ya utafiti

Parveen na Showkat (2017) wanaeleza kuwa maadili ni kanuni zinazoongoza tabia za mtu. Hivyo basi maadili katika utafiti ni kule kuwa mwadilifu na kuzingatia sheria za utafiti. Kuna kaida ambazo zinaonyesha tabia ambazo ni nzuri na zile ambazo ni mbaya na yale yanayokubalika na yale yasiyokubalika katika mchakato wote wa utafiti. Mtafiti yeyote anajukumu la kudumisha usalama, heshima, haki na hali njema ya watakaoshiriki katika utafiti husika. Watakoshiriki katika utafiti husika hapaswi kushurutishwa na mtafiti ili wampe habari anazohitaji kwa sababu wana uhuru wa kuchagua kushiriki au kutoshiriki katika utafiti. Fouka na Mantzorou (2011) wanasema kuwa maadili katika utafiti wowote ule ni muhimu sana katika maisha ya mtafiti ambapo mtafiti anahitijika kuheshimu watafitiwa na pia kuchapisha habari za kweli ambazo ametafiti.

Mtafiti alidumisha maadili ya utafiti katika mchakato wote wa utafiti. Mtafiti alizungumza wa Bw. Maoga kwa jamii ya Wakisii na Bw. Bakari akawafahamisha kuhusu utafiti wake na kuwa angetaka usaidizi wao na pia akawaeleza kuwa maoni yao na wanajamii yangetumiwa kwenye tasnifu ya uzamili. Uzingativu huu ulijenga uaminifu kati ya mtafiti na wanajamii ambapo walikubali kushiriki katika utafiti huo. Mtafiti pia aliheshimu tamaduni za jamii husika, kudumisha usalama wa watafitiwa na pia haki zao. Kabla ya kuanza utafiti mtafiti alipata kibali kutoka chuo kikuu cha Kenyatta na shirika la NACOSTI.

Hitimisho

Sura hii imejadili mambo ya msingi kuhusiana na utafiti wetu. Mambo ambayo ni tulishughulikia ni pamoja na usuli wa mada, suala la utafiti ambalo ni “Mtindo kwenye nyimbo za jadi katika jamii ya Wakisii na Waswahili wa nchini Kenya”. Aidha, tulishughulikia malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mad ana mbinu za utafiti. Sura inayofuata ilianguzia jinsi ambavyo walitumia mbinu za mtindo katika nyimbo za jadi.

SURA YA PILI

KUBAINISHA MCHANGO WA MBINU ZA MTINDO KWENYE NYIMBO

ZA JADI KATIKA KUSAWIRI HISTORIA NA TAMADUNI ZA JAMII

TEULE

2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilianguzia msingi wa utafiti. Sura hii itaanguzia kwa kina jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilitumiwa kusawiri tamaduni na historia katika nyimbo za jadi za jamii teule. Nyimbo hizi ni malighafi kuu katika kuelewa tamaduni na historia za jamii hizi mbili kwa sababu nyimbo zinapotungwa kwenye jamii, zinajikita kwenye muktadha halisi hasa wa kiwakati.

Kulingana na Talekau na wenzake (2014), historia ni ufasiri na uchambuzi wa maisha ya kale ya binadamu ambayo yanatusaidia kusoma maendeleo na mabadiliko yanayotokea kadri muda unavyopita. Wanaendelea kueleza kuwa historia ni tendo la upelelezi au la kufikiria ambalo linalenga kueleza jinsi watu wamebadilika kutokana na mpito wa wakati. Wanahistoria wanatumia ushahidi wa kila aina ili kuchunguza, kufasiri na kuhakiki kale yetu. Wao hutumia majengo, picha, michoro, masimulizi na kazi za sanaa.

Kwa mujibu wa Ponera (2014), utamaduni kama jumla ya matendo, fikra, mifumo ya maisha na kuashiria kingine chochote ambacho kinaweza kutumika kumwongoza na kumtambulisha mtu mmoja kwa jamii nyingine. Kulingana na gazeti la Taifa Leo (2019), dhana ya utamaduni inarejelea jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake. Utamaduni unajumuisha vipengele vifuatavyo: ujuzi, imani na itikadi, sana, maadili sheria au kanuni na desturi na vinginevyo. Hivi ni vipengele ambavyo mtu anarithishwa na kujitwalia kama mwanajamii.

Kutokana na maelezo ya wataalamu mbalimbali, historia ni maisha ya jadi au ya kale ya jamii na utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii fulani. Katika jamii hizi mbili, historia na tamaduni zao zimedhihirishwa kupitia kwa nyimbo za jadi. Katika sura hii imeangazia jinsi mbinu mbalimbali za mtindo zilivyotumiwa katika kusawiri historia na tamaduni za jamii hizi mbili teule kwa kina. Baadhi ya mbinu ni kama vile: kisengere nyuma, takriri, taswira, Historia na tamaduni ni kama vile: tohara, ndoa, vita vya kwanza vya dunia, taarabu na janga la njaa. Sura hii ilifanikishwa kupitia kwa mhimili wa kiwango cha semantiki ambacho kinashughulikia maana inayoibuliwa na lugha ambayo mtunzi ameamua kutumia. Mhimili huu ulisaidia katika kuelewa jinsi ambavyo mbinu za kintindo zilitumiwa katika kusawiri historia na tamaduni za jamii husika.

2.1 Historia na Tamaduni za Jamii ya Wakisii

Wakisii ni mojawapo ya jamii kubwa ya Wabantu ambao wanaishi katika eneo la mkoa wa Nyanza kwenye kaunti ya Bosongo (Kisii) na Nyamira. Kulingana na Nyamwaka (2000) Wakisii wanaishi kwenye eneo ambalo lina miundo mbalimbali ya kijiografia ikiwemo milima na mito. Anaendelea kueleza kuwa eneo hili lina rutuba nzuri sana na hali yake ya anga huwapa wenyeji wa eneo hilo nafasi nzuri ya kushiriki katika kilimo. Eneo hili lina vijito vingi ambavyo huelekeza maji yake kwa mito tofauti. Kuna mito mingi sana katika eneo hili ambayo huelekeza maji yake katika ziwa Victoria na mito hii imeawasaidia katika kufanikisha shughuli zao za kilimo. Baadhi ya mito ni kama vile: Gucha, Sondu na Mogonga.

Kulingana na fasihi imulizi ya Wakisii, wanaaminiwa kuwa walitoka Misri kama Waluhya. Walikaa katika eneo lililokuwa karibu na mlima Elgon kwa miaka mingi. Kulingana na Ochieng (1974) Wakisii walilazimishwa kuhama na jamii ya Waluo

katika kipindi cha 1500 AD. Waliwasukuma hadi eneo la Kisumu na mwisho wakahama na kuingia kwenye milima ya Kisii eneo ambalo liligeuka na kuwa makao yao ya milele. Anaendelea kusema kuwa, kuhama kwa Wakisii kulichochea na mambo kama vile: njaa, kiangazi, migogoro ya kiuchumi, migogoro ya kijamii na migogoro ya kisiasa. Naye Odhiambo (1979) anaeleza kuwa kuhama kwa watu kulikuwa ni mchakato wa polepole ambao ulichukua zaidi ya miaka elfu mbili. Watu hao walikuwa wakihama kwa makundi madogomadogo ili kurahisisha shughuli hiyo.

Mzee Maoga alisema kuwa baada ya Wakisii kuingia nchini Kenya walishuhudia mambo mbalimbali kama vile: njaa, vitas na vifo. Pia walishughulika na mambo kama vile kilimo, uhunzi na wizi wa mifugo. Kando na hayo, walikuwa na tamaduni zao ambazo walikuwa wanashikilia kabla ya kutoka Misri na walipoingia nchini Kenya waliweza kukopa tamaduni zingine kutoka kwa majirani wao. Tamaduni zao zilisheni miviga mbalimbali kama vile: tohara, kuwapa watoto majina, ndoa na sherehe za mazishi.

2.1.1 Njaa

Dhana ya njaa imeelezwa na makundi mbalimbali kwenye jamii. Kulingana na UNHCR (2024), wanaeleza njaa kuwa ni hali ambapo idadi kubwa ya watu katika nchi au eneo fulani hawana uwezo wa kupata chakula cha kutosha jambo ambalo linapelekea utapiamlo na watu kuaga dunia kwa sababu ya njaa na magonjwa yanayohusiana na njaa. Kulingana na Nat Geo (2023), wameeleza njaa kuwa ni hali ya uhaba wa chakula uliosambaa miongoni mwa watu wengi katika eneo fulani. Wanakubaliana na UNHCR (2024), kuwa njaa inapelekea katika kuongezeka kwa utapiamlo, njaa, magonjwa na vifo vya watu wengi sana. Kulingana na TUKI (2019), njaa ni ukosefu mkubwa wa chakula. Njaa yaweza kusababisha maafa makubwa kwenye jamii. Kwa mujibu wa UNHCR (2024), inataja visababishi vikuu vya njaa

kama vile migogoro katika jamii, kuhama au kuhamishwa kwa watu, umaskini wa hali ya juu, uhaba wa chakula, majanga mbalimbali kama vile: kiangazi na masika. Njaa inawapelekea watu kukosa na kukosewa heshima, usawa katika jamii na hata maisha ya raha kwenye jamii.

Kupitia kwa mbinu ya kisengere nyuma, njaa ambayo ilikumba jamii hii kati ya mwaka 1888-1892 na 1914-1919 ilielezwa. Mbali na hayo, madhara ya njaa hiyo pia yaliangaziwa kwani watu wengi walipoteza uhai. Kulingana na Bogonko (1976), anasema kuwa jamii hii iliathirika na njaa sana hasa kati ya mwaka wa 1888-1892 na kati ya 1914-1919. Kutokana na janga hili la njaa jamii hii ilitunga nyimbo nyingi ambazo zilihusiana na janga hili na nyimbo hizi zimerithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Mzee Maoga alieleza kuwa tangu jadi, mashamba katika eneo la Kisii yalikuwa na rutuba na pia eneo hili lilikuwa likipokea mvua kwa wingi. Mvua hii iliwasaidia katika kukuza mime ana mifugo wao. Hivyo basi Wakisii kukumbwa na janga la njaa lilikuwa jambo la kushangaza sana ni kutokana na hali hii jamii hii iliapa kutosahau mkasa huu. Janga hili lilisababishwa na mambo yafutayo: ukame, vita, vyakula kuvamiwa na nzige pamoja na magonjwa na vita vya pili vya dunia.

Kipindi cha kati ya mwaka wa 1888-1892 kilikuwa kipindi cha kutisha kwa jamii hii. Walivamiwa na janga la njaa ambalo lilitokana na mifugo pamoja na mimea shambani kuvamiwa na magonjwa na mamilioni ya nzige. Tukio hili lilichangia katika vifo vya asilimia kubwa ya mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Mzee Maoga alisemea kuwa vifo vya mifugo hawa vilikuwa na athari mbaya kwa jamii hii kwa sababu walitegemea mifugo hawa kwa nyama, damu na maziwa. Kando na mifugo

wengi kufa pia mazao yao shambani yaliathirika. Mimea kama vile: mahindi, maharagwe, wimbi, mtama, viazi vitamu na viazi vikuu iliathirika. Mkasa huu haukutokea tu katika jamii ya Wakisii tu bali pia katika jamii ya Waluo na Wakipsigis.

Mzee Mayaka na mzee Nyakweba walieleza kuwa eneo la Kisii lilikuwa likishuhudia mvua kwa kiwango kikubwa sana. Na kutokana na mvua ambayo ilikuwa inanyesha kila mara, jamii ya Wakisii ilivalia njuga suala la kilimo. Walipanda mimea ambayo walitumia kama chakula na mimea ingine waliuza kama vile pareto na majani chai. Kwa kipindi kirefu sana hawakuwa wanafahamu lolote kuhusu ukame hivyo basi hawakuwa na mipango yoyote mbadala iwapo ukame ungetokea. Ukame wa 1888-1892 ulioathiri maeneo ya Afrika haukusaza eneo la Kisii. Athari ya ukame huo ilidhihirika. Vyakula ambavyo vilikuwa shambani vilikauka kwa kukosa maji ya kuvisaidia vinawiri. Katika mashamba ndogondogo (*ebiticha*) ambamo wanawake walikuwa wanapanda mboga za aina mbalimbali zilikauka pia. Kutokana na mimea kukauka athari hii ilihisika kwa mifugo na watu. Mifugo wengi waliangamia kwa kukosa chakula pamoja nasi. Baadhi ya mimea ambayo ilikuwa inakuwa kwenye viwanja kama vile nyasi ambayo ng'ombe walikuwa wanakula ambayo ilikauka pia. Kutokana na mifugo kufa na mimea kukauka watu waliangamia kwa sababu hawangepata chakula kutoka kwa mimea. Watoto, vijana na wazee wote waliangamia.

Kutokana na mkasa huu wa njaa, jamii hii ilianza kubadilisha mienendo yao hasa kuhusiana na maswala ya kilimo. Mvua iliporejea katika misimu yake ya kawaida, walianza kuhifadhi maji ya mvua ambayo wangetumia katika kunyunyizia mimea yao maji iwapo ukame ungetokea. Pili, walijenga maghala mengi ambayo walitumia kuhifadhi vyakula na mwisho walianza kuelimishana kuhusu kuchunga na kuhifadhi

mimea yao kwa sababu hawakutaka kupoteza maisha ya watu na wanyama kwa sababu ya chakula. Hali hii ilidhihirika katika ubeti ufuatao:

Enchara nembe, yaitire omogusii
Enchara nembe, enchara nembe
Enchara nembe, yaitire omogusii
Enchara nembe, enchara nembe
Baminto aiga Gusii
Baminto aaria Kisumo
Yaitire omogusii
Torende endagera yaito

Tafsiri

Njaa ni mbaya, imeua mkisii
Njaa ni mbaya, njaa ni mbaya
Njaa ni mbaya, imeua mkisii
Njaa ni mbaya, njaa ni mbaya
Watu wetu hapa Kisii
Watu wetu pale Kisumu
Imeua mkisii
Tulinde chakula chetu

Wimbo huu ulitoa mwanga zaidi kuhusu athari ya njaa ambayo walishuhudia. Ni dhahiri kuwa njaa ilisababisha maafa mengi. Haikusababisha maafa katika eneo la Kisii tu bali pia kwa jamii zingine. Wimbo huu ulitumiwa kutahadhirisha na kuwakumbusha watu wachunge chakula chao, walikumbushwa wahifadhi chakula chao na pia wakitumie chakula chao vizuri ili wasiangamie kwa sababu ya njaa.

Wimbo huu ulikuwa unaimbwa sana hasa msimu wa mvuno kati ya mwezi wa Agosti na Desemba kwa sababu huu ndio wakati waliokuwa wakivuna. Baada ya kuvuna mahindi, ngano na wimbi walikausha kisha kuweka nafaka hizi kwenye gunia na kuzihifadhi kwenye maghala. Nafaka hizi ziliaminiwa kuwa zingekaa kwa muda ya miaka miwili au mitatu bila kuharibika ikiwa zingeifadhiwa vizuri. Viongozi na wazee wa jamii walijitwika jukumu la kuwakumbusha watu kila mara umuhimu wa kuhifadhi vyakula vyao ili wasishuhudie maafa tena.

2.1.2 Vita vya Kwanza vya Dunia

Vita vya Kwanza vya Dunia vilikuwa Ulaya. Vita hivi vilianza mwaka wa 1914 na kuhitimishwa mwaka wa 1918. Kulingana na Williamson (1988), vita hivi vilizuka baada ya kuuliwa kwa Archduke Franz Ferdinand wa Austria. Vita hivi vilihusisha makundi mawili. Kundi la kwanza lilikuwa la Mataifa ya Kati (*Central Power*) ambalo lilikuwa na mataifa kama vile; Ujerumani, Austria-Hungaria, Bulgaria na Uturuki. Kundi la pili lilihusisha Mataifa ya Ushirikiano (*Allied Powers*) ambalo lilikuwa na Ufaransa, Urusi, Uingereza, Italia na Marekani. Vita hivi vilikuwa na athari kubwa ulimwengu mzima. Kulingana na Unacademy (2021) walieleza athari mbalimbali za vita hivi. Kwanza vilipelekea mataifa mengi ya Ulaya kuzama katika lindi la madeni, pili nchi ya Marekani iliinukia kuwa yenye nguvu zaidi kwa kutumia kipimo cha Uchumi hata zana za vita. Isitoshe, watu wengi walitekwa nyara hasa kutoka bara la Afrika ili keunda kupigana na mwisho kabisa hali ya kiuchumi ilikuwa ngumu sana kwa mataifa mengi ulimwenguni.

Mtunzi wa *Enchara Nembe* alitumia mbinu ya kisengere nyumba katika kuonyesha mchango wa jamii hii katika vita hivi. Kupitia kwa mbinu hii ilibainika kuwa wanajamii hawa walilazimishwa kushiriki katika vita hivyo kupitia kwa viongozi wao. Usaliti ambao uliendelezwa na viongozi wao katika kuwapeleka watu wao kupigana kwenye vita vya kwanza vya dunia ulidhihirika. Wimbo ufuatao uliangazia jinsi ambavyo vita hivyo viliathiri jamii hii na kuwakumbusha watu watunze mazao yao kwa sababu njaa ni kitu kinachosabisha huzuni mwingi sana.

Enchara nembe banto baito
Banto baito bakairwa
Abatureti bagatorwa buna ebing'wanso
Bakagenda korwanera abasongo
Megondo kabora omeremi
Abasae bakagenda korwana
Endagera ekobora mwanagentinge

Gaki abaminto renda rigesa

Tafsiri

Njaa ni mbaya watu wetu
Watu wetu wakachukuliwa
Wazee wa Kijiji walilitoa kama kafara
Wakaenda kupigania mwingereza
Mashamba yakakosa mkulima
Vijana wakaenda kupigana
Chakula kikamkosa mkisii
Jamani watu wetu tulinde mazao

Mzee Nyakweba alisema kuwa Waafrika hawakusazwa kwenye vita hivi kwani walikuwa viungo muhimu sana katika vita hivi. Vita hivyo vilipoanza mwaka wa 1914 nchi ya Uingereza ilihitaji wafanyakazi na watu zaidi wa kupigana dhidi ya nchi ya Ujerumani na wafuasi wa Ujerumani. Ilibidi nchi ya Uingereza iingie mashinani na kuchukua watoto, vijana na wazee wenye nguvu waende kupigana dhidi ya Ujerumani. Jamii ya Wakisii ni mojawapo ya jamii iliyoathirika sana kwa vita hivyo. Kwa mujibu wa Omwoyo (2015), kati ya mwaka wa 1914 na 1916 wakisii 21,864 walichukuliwa kuenda kushiriki katika vita hivyo. Kufikia mwaka wa 1918 Wakisii 42,990 walikuwa wamechukuliwa. Waingereza walitumia mitindo mbalimbali ili kuwateka watu kutoka kwa jamii.

Mzee Ombuya alieleza kuwa baadhi ya watu walilaghaiwa kwa kutumia zawadi ndogo ndogo hasa vitu ambavyo vilikuwa vinazalishwa kwenye viwanda vya nchi ya Marekani. Vijana wengi walitekwa nyara kupitia kwa usaidizi wa wazee wa kijiji hasa wakati ambapo kulikuwa na mashindano ya michezo. Baadhi ya boma zilivamiwa wakati wa usiku na watu kuchukuliwa na wakati mwingine walilazimisha *abatureti* na *abagambi* (wazee wa vijiji na machifu) kuwapa watu wenye nguvu ili waende kupigana. Mzee Mayaka naye alifafanua zaidi kuhusu athari ya watu hawa kutekwa nyara kutoka kwenye jamii ilikuwa wazi. Kwanza shughuli za biashara ziliathirika

sana kwa sababu watu wengi walikuwa wakihofia usalama wao kwani wangetekwa nyara wakati wowote ule. Pili, shughuli za kilimo zilianza kupungua miongoni mwa Wakisii jambo ambalo lilipelekea kupungua kwa uzalishaji wa vyakula kwa sababu watu ambao walikuwa na nguvu za kufanya kazi ngumu za shambani hawakuwa kwani waliobaki walikuwa wazee, wagonjwa, wanawake na watoto wachanga. Makundi haya hayakuwa na nguvu ya kufanya kazi za shambani hivyo mashamba ambayo yalitumiwa katika shughuli za kilimo yalipungua.

Vita hivi vilipoanza walilazimishwa kupanda mahindi na kuachana na kilimo cha awali ambacho lihusisha wimbi, mtama na njugu. Jambo hili liligeuka kuwa changamoto kuu kwa sababu hawakuwa na pembejeo. Ugavi wa pembejeo katika jamii yao ulikuwa unatamausha kwa sababu walikuwa wanapewa pembejeo kutokana na umaarufu na hadhi yako kwenye jamii. Hali hii ilifungia watu wengi sana nje katika kilimo cha mahindi.

Kutokana na mambo haya mbalimbali ambayo yalihusishwa na vita hivi, jamii ya Wakisii ilishuhudia kudorora kwa afya kwa sababu ya njaa ambayo ilisababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa chakula. Umaskini ulikithiri kwa sababu watu wengi waliogopa kushiriki kwenye biashara, watu kuishi kwa woga na wale ambao wangesaidia katika kuimarisha jamii walikuwa wameenda kupigana dhidi ya Ujerumani.

2.1.3 Migogoro kati ya Wakisii na Majirani wao

Kulingana na Levi (2013), anasema kuwa mgogoro ni hali ambapo watu au makundi fulani ya watu yanaona na kuhisi kuwa wengine wanafanya matendo ambayo yana athari hasi kwa maslahi yao au mambo wanathamini. Kwa mujibu wa Robbins na Judge (2008), waneleza mgogoro kuwa ni mchakato ambao huanza wakati kundi moja

linahisi kuwa kundi lingine linaenda kuwaathiri vibaya au kuleta madhara mabaya kwa kitu ambacho wanathamini. Kama asemavyo Weber (1968), uhusiano wa kijamii unarejelewa kama mgogoro hasa matendo ya mtu fulani yanapochukuliwa kuwa na kusudi la kibinafsi na yanayoenda kinyume na kikundi au makundi fulani. Kwa hivyo kulingana na yeye mgogoro ni ile hali ya mtu kuwa na hamu ya kulazimisha mapenzi yake au mambo yake kibinafsi kwa watu ambao wanapinga. Hivyo kwa jumla mgogoro ni mapambano kati ya watu yanayotokana na watu hao kuwa na mawazo, mitazamo, uelewa wa mambo tofauti na ubinafsi.

Jamii hii inapakana na jamii mbalimbali kama vile: Wamaasai, Wakuria, Waluo na Wakipsigis. Walitangamana na majirani wao kwa njia mbalimbali kama vile: biashara, vita na kadhalika.

Mbinu ya taswira ilitumiwa katika kusawiri mgogoro ambao umekuwa tangu jadi kati ya Wakisi na mairani wao. Mzee Nyakweba na Mzee Maoga walieleza kuwa migogoro hii ilijikita sana katika wizi wa mifugo pamoja na mahali pa kulisha mifugo wao. Mifugo hawa hasa ng'ombe na mbuzi walikuwa wanawapa nyama, maziwa pia walikuwa ishara ya utajiri na pia walilipa mahari kwa kutumia mifugo. Kando na hayo, fahali walitumiwa katika shughuli za kilimo hasa kwa watu ambao walikuwa wanamiliki mashamba makubwa. Hivyo basi jamii hizi zilitumia mbinu zozote zile ili kumiliki mifugo wengi iwezekanavyo. Kupitia kwa taswira hisi na taswira uoni wanajamii wanahamasisha wavulana ambao walipelekwa jandoni kuwa tayari ili kurejesha mifugo wao katika wimbo wa *Obeire Omomura*. Mzee Maoga alipohojiwa alisema kuwa katika jamii ya Wakipsigis wizi wa mifugo ulihalalishwa kwa sababu kupitia kwa wizi huo ndipo wangeweza kumiliki mifungo wengi. Familia ambayo ingefanikiwa kuiba mifugo wengi ilikuwa ikiheshimiwa na jamii kiasi kwamba ilikuwa inapewa nafasi ya kuongoza. Kutokana na ari ya kuwa na mali, heshima na

kuongoza wanaume wengi katika jamii ya Kipsigis walishiriki katika wizi wa mifugo. Kupitia kwa wimbo huu, kitendo hiki cha wizi wa mifugo kilidhihirika. Wakisii nao walidhihirsha hasira kutokana na wizi huo hivyo basi walihitaji kuirudisha mfugo wao.

Abasigisi batosamirie pi ee-yoo
Banto aba bairire chitugo chiaito ee-yoo
Toimoke bono iga tochiiranie ee-yoo
Toiranie chiombe chiaito ee-yoo

Tafsiri

Wakipsigis wametubia kabsaa ee-yoo
Watu hawa wmechukua mifugo wetu ee-yoo
Tuondoke sasa hivi tuirudishe ee-yoo
Turudishe ng'ombe wetu ee-yoo

Mzee Onyancha alisema kuwa vijana walipokuwa jandoni walikuwa wanafunzwa kuhusu mila, tamaduni, historia na majukumu yao mapya kwenye jamii. Jambo hili lilidhihirika kupitia kwa wimbo huu wa jandoni ambapo wavulana walihimizwa wajitayarisha kuenda kupigana ili kurudisha mifugo wao ambao waliibwa na majirani wao. Wimbo huu ulihusihwa na karne ya kumi na tisa ambapo jamii ya Wakipsigis ilitekeleza uvamizi mkuu kwenye jamii ya Wakisii ingawa bado wanaendeleza hulka hiyo sasa hivi. Mzee Mayaka alisimulia kwa katika karne ya kumi na tisa, Wakipsigis waliwavamia Wakisii usiku wakaiba mifugo wengi sana. Kando na kuiba, kuna mifugo ambao walikuwa wamezeeka na mifugo wengine walikuwa dhaifu hao walichomwa kwa sababu kulinana na wao ni kuwa hakuwa na faida yoyote. Kuongezea chumvi kwenye kidonda, walichoma nyumba za Wakisii jambo ambalo lilipelekea maafa ya watoto, watu wakongwe na wale wote ambao hawangeweza kujiokoa. Kitendo hiki kilisababisha uhasama mkubwa kati ya jamii hizi mbili. Kilichochea vita na wizi wa mifugo mara kwa mara. Kutokana na hasara zilizotokana

na tukio hili walitunga nyimbo nyingi kuhusu tukio hili ili kukumbusha vizazi vyote kuhusu asili ya uhasama wao.

Mbali na jamii ya Wakipsigis, Mzee Mayaka alipohojiwa alieleza kuwa Wakisii walikuwa na mgogoro mkubwa pia na jamii ya Wamaasai wa Transmara. Thamani ya mifugo hasa ng'ombe kwenye jamii ya Wamaasai ni sawa au ni zaidi ikilinganishwa na jamii ya Wakisii na Wakipsigis. Kutokana na kuthamini ng'ombe sana, Wamaasai walipigana na majirani wao sana kwa sababu ya wizi wa mifugo uliokuwa ukiendelea miongoni mwao, kwani fahari yao kuu ilikuwa ni kumiliki mifugo wengi. Kutokana na wizi wa mfugo, Wakisii walikuwa wanawafunza vijana wao umuhimu wa kuchunga mifugo wao na kuhakikisha kuwa wamedumisha usalama. Katika mafunzo yao ya jandoni wavulana hawa walifunzwa namna ya kutumia silaha mbalimbali kama vile: mikuki, mishale, ngao na kadhalika. Vijana hawa walikuwa wanatarishwa kisaikolojia kuhusu kuilinda mifugo ili wasiibwe au kuenda kurejesha mifugo walioibwa na *Abamanyi* (Wamaasai).

Katika ubeti wa kwanza kwenye wimbo wa Obeire Omomura mbinu ya takriri ilitumiwa ili kusisitiza kuwa wavulana waliopashwa tohara waistahili kuenda kupigana na kurejesha mifugo walioibwa. Hali kadhalika, mbinu ya taswira uoni inatumiwa kuenysha jinsi ambavyo silaha ambazo wangetumia zilistahili kuwa sa sababu kubeba silaha butu kungewasababishia kushindwa. Silaha hizo zingewasaidia kupigana na kuhakikisha kuwa mifugo wote wamerejeshwa. Wavulana hawa pia walihimizwa wawe jasiri kwa sababu sasa ni jukumu lao la kuhakikisha kuwa Wamaasai hawangewasumbua tena kwa kuiba mifugo, wadumishe usalama kijijini na ikiwezekana waibe mifugo kutoka kwa Wamaasai ili waheshimiwe. Kupitia kwa ubeti huu hayo ndiyo yalidhihirika.

Obeire omomura obeire omomura ee-yoo
Bono mambia bono mambia ee-yoo
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo ee-yoo
Nanguba boigo na nguba boigo ee-yoo
Abamanyi batochandire kera engaki ee-yoo

Tafsiri

Amekuwa mwanamume amekuwa mwanamume ee-yoo
Leo asubuhi leo asubuhi ee-yoo
Atayarishiwe mkuki pamoja na mshale ee-yoo
Wamaasai wametusumbua kila wakati ee-yoo

2.1.4 Tohara

Kulingana na Yoshanda Hosiptals (2023), tohara ni kuondolewa kwa govi kwa nia ya upasuaji. Tohara ni jambo la kawaida ulimwenguni kote ambapo inaweza kufanywa kwa sababu za kitamaduni, kidini au matibabu. Tohara ni mojawapo wa tamaduni muhimu sana katika jamii ya Wakisii. Kulingana na gazeti la Daily Nation (2023), ni kuwa kwa miaka michache iliyopita, tohara katika eneo la Kisii ilikuwa jambo ambalo ni muhimu sana. Baada ya wavulana kuingia na kutoka jandoni hapo ndipo walipewa nafasi ya kuingia utu uzima. Katika miaka ya 1980, sherehe hii ilikuwa imejikita katika utamaduni. Wavulana walikuwa wanakutana na kisu cha ngariba bila ngozi yao kufishwa ganzi. Watu walioandamana na wavulana kuenda jandoni walirudi wakiimba nyimbo za kiutamaduni za jandoni. Walipowasili nyumbani, milango ya boma ilifunguliwa na wanajamii kukaribishwa ili kusherehekea kwa kula, kunywa na kuimba. Baadhi ya watu walipewa jukumu la kuwaelekeza vijana hao kuhusu mambo wanayostahili kufanya, kuepuka na matarajio ya jamii kwao.

Mzee Ombuya alieleza kuwa sherehe hizi za tohara katika jamii ya Wakisii ziliandaliwa mwezi wa Agosti na mwezi wa Desemba kwa sababu hicho ndicho kipindi cha kuvuna mazao yao hivyo basi walitumia sherehe hizo pia kumshukuru Mungu kwa baraka za vyakula. Kupeleka wavulana jandoni ni tamaduni iliyoanza

kitambo na bado wanendelea kuipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine hata ingawa baadhi ya watu ambao hasa wanaishi mjini hawawapeleki vijana wao jandoni kwa kutumia mienendo ya mababu zao.

Anaendelea kueleza kuwa wavulana kati ya miaka kumi hadi kumi na mitatu ndio waliopolekwa jandoni. Sherehe hii ilihusisha kijiji chote kwani wavulana kutoka familia mbalimbali waliunganishwa na kupelekwa jandoni pamoja. Sherehe hizi zilianza jioni kabla ya siku yenyewe ya kuenda jandoni. *Abaare* (wavulana wanaoenda kupashwa tohara), *abakebi* (ngariba), vijana ambao ni wakubwa wao kiumri na ambao wamepashwa tohara, baadhi ya wazee wa umri wa makamo ambao walipewa jukumu la kuongoza vijana hawa na wazee wakongwe ambao waliongoza sherehe hizi walikusanyika kwa boma ya mmoja wa mvulana ambaye anapashwa tohara. Watu hao walisherehekea usiku kucha, wazee walitayarishiwa pombe ya kienyeji (amarwa) ambayo walikunywa usiku kucha.

Ili kufanikisha usiku huo, vijana hao walishirikishwa na kufanyiwa mambo mengi ambayo yalilenga kupima ujasiri wa wao. Kwanza walilazimishwa kuketi kwenye majani yaliyowasha au mimea yenye miiba. Kijana yeyote aliyelia au aliyeonyesha hisia za uchungu alichekelewa na kuambiwa kuwa yeye ni mnyonge na hakustahili kuwa mwanamume. Baada ya hapo vijana hao walipewa silaha za vita ili wazinoe kwa kutumia dakika chache sana. Yeyote aliyemaliza wa kwanza aliteuliwa kuwa kiongozi wa vijana wengine ambao wanapashwa tohara. Nafasi hii ya uongozi ni muhimu sana kwa sababu wangeishikilia hadi uzeeni hivyo kulikuwa na ushindani mkubwa.

Mzee Onyancha alieleza kuwa siku ya tohara ilianza saa tisa asubuhi. Wavulana waliopashwa tohara walipelekwa mtoni ili kuoga maji hayo baraidi. Lengo kuu la

kutumia maji hayo baridi lilikuwa la kuifanya ngozi igande hivyo wasihisi uchungu mwingi walipopashwa tohara. Pia ilikuwa ni ishara kuwa walikuwa tayari kutoka utotoni na kuingia utu uzima. Asubuhi hiyo katika mchakato wa kuwapasha tohara, vijana hao walipewa vitisho vingi kwa sababu wanajamii walijua kuwa kitendo hicho ni uchungu sana. Vijana hao waliambiwa kuwa wakilia, wanawake wote wa kijiji wangeitwa ili waje kuona uchi wao na kuwacheka. Hili jambo lilikuwa linatisha na la aibu kwa vijana hawa kwa sababu wanawake hawakupaswa kuona uchi wa vijana. Hivyo ili kuepuka aibu hii, vijana hao ilibidi wavumilie bila kuonyesha udhaifu wowote.

Kupitia kwa mbinu ya takriri, dhima ya jandoni ilidhihirika na matarajio ya jamii kwa wavulana waliotahiriwa katika wimbo wa *Obeire Omomura*. Wakiwa pale vijana walifunzwa na wazee pamoja na wakubwa wao kuhusu majukumu yao mapya kwenye jamii. Kwa mfano: kabla wavulana hao watahiriwe walienda mtoni, waliteka kuni, walisaidia katika kuandaa chakula ila baada ya kutahiriwa, vijana hawa hawakupaswa kuenda mtoni, hawakupaswa kuingia jikoni ili kupika, walistahili kuanza kujitayarisha kwa ajili ya ndoa, walistahili kuhakikisha kuwa familia zao zilikuwa salama. Kutokana na mgogoro wa mara kwa mara kati ya Wakasii na majrani wao hasa wa wizi wa mifugo, vijana hawa walikuwa wanatarajiwa kujiunga na wanamume kwenye jamii ili kuenda kurudisha mifugo walioibwa, kuiba mifugo na kuzuia mifugo wao wasiibwe. Kupitia kwa nyimbo wa wimbo wa *Obeire Omomura*, utamaduni huu ulidhihirika ifuatavyo:

Obeire omomura, obeire omomura bono mambia ee-yoo
Bono mambia, bono mambia ee-yoo
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo ee-yoo
Nanguba boigo, nanguba boigo ee-yoo
Abamanyi batochandire, kera engaki ee-yoo
Abasigisi batosamirie ee-yoo
Banto aba bairire chitugo chiato ee-yoo

Toimoke bono iga tochiiranie ee-yoo
Ng'ina amosike, ng'ina amosike ee-yoo
Tomotoma roche, tomotoma roche
Obeire buna cheri, aegwe obweri bwaye ee-yoo

Tafsiri

Amekuwa mwanamumwe, amekuwa mwanamume ee-yoo
Leo asubuhi, leo asubuhi ee-yoo
Anolewe mkuki, anolewe mkuki ee-yoo
Pamoja na mshale, pamoja na mshale ee-yoo
Wamaasai wametusumbua kila wakati ee-yoo
Wakipsigis wametusumbua ee-yoo
Watu hawa wamechukua mifugo wetu ee-yoo
Tuende sasa hivi tuwarudishe ee-yoo
Turudishe ng'ombe wetu ee-yoo
Mama yake amuheshimu, mama yake amuheshimu ee-yoo
Asimtume mtoni, asimtume mtoni ee-yoo
Amekuwa kama Fahari, epewe zizi lake ee-yoo

Kupitia nyimbo za jandoni, mabadiliko ya kimwili ambayo vijana hawa walishuhudia yalidhihirishwa. Mabadiliko hayo yalisawiriwa kupitia kwa mbinu ya takriri. Ambapo kuna kipande ambacho kinarudia kuwa amekuwa mwanamume na hivyo basi alipaswa kupewa silaha za kuenda kupigana. Vijana hawa walikumbushwa kuwa lazima wahakikishe kila kitu kiko sawa hasa kuhusiana na uume ambao ulirejelewa kama *enyamweri* (chatu-ambaye ni nyoka mkubwa na hatari). Uume kuwa katika hali nzuri ulichukuliwa kuwa jambo la muhimu sana kwani ndio ungezuia ndoa zao zisivunjike watakapohitimu umri wa kuoa.

Ise mokami oirire chimboro chiabo ee-yoo
Ise mokami oirire chimboro chiabo ee-yoo
Omoisia omoke bororo bwamorire ee-yoo
Twachire buya, twachire buya ee-yoo
Bono mambia, bono mambia ee-yoo
Oyotaegenetie tiga ache kwrorera ee-yoo
Kwrorera enyamweri korwa engero ime ee-yoo
Kwrorera enyamweri korwa engoro ime ee-yoo

Tafsiri

Babu yao amechukua uume wao ee-yoo
Babe yao amechukua uume wao ee-yoo
Kijana mdogo anahisi uchungu ee-yoo
Tumewasili sasa tumewasili sasa ee-yoo
Leo asubuhi leo asubuhi ee-yoo
Yeyote asieamini, wacha aje ajionee
Ajionee chatu iliyotoka kwa shimo ee-yoo
Ajionee chatu iliyotoka kwa shimo ee-yoo

2.1.5 Ndoa

Taasisi ya ndoa ni muhimu sana katika jamii yoyote ile ulimwenguni. Kwa mjibu wa Vidya na Sachdeva (2007), ndoa ni asasi ambayo huleta mume na mke pamoja ili kuanzisha familia. Kulingana na Durkheim (1962), asasi hii hudumisha jamii kupitia kwa majukumu yake ya kuhakikisha wanajamii wapya wanazaliwa, wanakidhiwa mahitaji yao na kufunzwa kanuni na amali za jamii zao. Kama asemavyo Mberesia (2021), anasema kuwa asasi hii inatarajiwa kutoa mazingira bora ya kuzaa na kulea kizazi kipya ambacho kinategemewa kuendeleza jamii. Anaendelea kusema kuwa ndoa ni mojawapo ya asasi zinazounda mfumo wa jamii na kukeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Kwa jumla ndoa ni makubaliano ya rasmi ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke.

Jinsi ambavyo jamii mbalimbali zilivyoenzi taasisi hii ya ndoa ndivyo pia jamii ya wakisii ilivyoenzi ndoa. Ndoa katika jamii ya Wakisii ilishirikisha watu kutoka ukoo tofauti kwa sababu ndoa kati ya watu wa ukoo mmoja ni mwiko. Vijana ambao wangejihusisha kimapenzi na wasichana kutoka kwenye ukoo wao waliadhibiwa na wazazi wao. Mama Mong'ina alieleza kuwa, baada ya mvulana au msichana kukomaa, wazazi wa msichana au mvulana walikuwa wanaanza kumtafutia mtoto wao mchumba. Kutambua msichana aliyetaka kuo na kuolewa na huyo msichana. Kwa mfano, wazazi wa mvulana walipopata msichana aliyewaridhisha, wazazi wa huyo mvulana walienda nyumbani mwa msichana huyo ili kukutana na wazazi na

wazee wa msichana huyo ili kujadili yaliyojiri. Wazazi hao walipokubali posa, mkutano wa pili uliandaliwa ambapo wazee kutoka kwa ukoo wa mvulana na wazee kutoka kwa ukoo wa msichana walikutana ili kujadili suala la mahari. Mahari yalikuwa yanahusisha utoaji wa ng'ombe ila siku hizi baadhi ya familia hukubali kuchuka pesa. Ili kuamua mahari yaliyostahili kutolewa kitu cha kwanza kilichozingatiwa ni hali ya kiuchumi ya familia ya mvulana, hali ya kiuchumi ya ukoo wa msichana na hadhi ya msichana huyo kwenye jamii. Ili ndoa yoyote ikamilike lazima mahari yangetolewa, ikiwa aila ya mvulana haijatoa mahari hata kama wawili wangeishi pamoja hiyo haingezingatiwa kama ndoa kamili.

Baada ya shughuli ya kulipa mahari kukamilika, familia hizo zilijipa muda wa miezi miwili hadi mitatu ili kujitayarisha kwa siku kuu. Katika harakati za maandalizi ya sherehe hiyo, msichana na wavulana walifunzwa kuhusu masuala ya ndoa na matarajio yao. Maandalizi yalipokamilika ndoa ilisherehekewa kwa siku moja kisha wanandoa wakapewa nafasi ya kuanza maisha yao.

Mbinu ya kisengere nyuma ilitumiwa kuonyesha imani ya jamii hii katika ndoa kupitia kwa mbinu hii kwenye wimbo wa *Abagusii Bakabora* kitu cha kwanza ambacho wawili hawa walikumbushwa ni kuhusu kupata watoto. Wanandoa ambao hawangefanikiwa kupata mtoto walirejelewa kama mti mkavu au mti ambao umekauka na hauna maaana ama umuhimu wowote kwenye jamii. Kupitia kwa mbinu ya jazanda, wanandoa walikumbushwa kuhusu jukumu lao kuu katika ndoa. Wawili hao wangekosa kupata watoto kila mtu kwenye jamii angewadharau. Hivyo, ili kuepukwa kuitwa mti mkavu, wawili hao walijitahidi kusudi wapate watoto. Imani hii ilidhihirika ifuatavyo:

Abagusii bakare bagakwana
Bagakwana bagateba ng'a
Oyatabwati omwana no'mote mwomo

Tafsiri

Wakisii wa kitambo walisema
Wakasema hivi
Asiye na mtoto ni mti mkavu

Jamii hii ya jadi ilikuwa inathamini sana watoto hasa wa kiume. Mzee Mayaka alieleza kuwa wanandoa hao walipokosa kujaliwa mtoto baada ya kuoana, walikuwa wanapelekwa kwa *abaragori* na *abanyamete* (waganga na daktari wa kienyeji) watu hawa walikuwa wanatumia miti shamba kutibu. Ikiwa mwanamke angepatikana kuwa yeye ndiye alikuwa na shida ya kupata watoto, mume wake alikuwa anahimizwa aoe mke mwingine ambaye angemzalia watoto kwa sababu walikuwa wanaamini kuwa mtoto wa kiume ndiye angeendeleza ukoo kwani mtoto wa kike angeenda kuanza familia yake na kusahahu alikozaliwa. Kando na hayo, ikiwa wawili hao wangejaliwa watoto wa kike tu mwanamume alikuwa anahimizwa aoe mke mwingine ambaye labda angemzalia mtoto wa kiume. Ikiwa mwanamume ndiye alikuwa na shida ya kupata watoto mwanamume huyo angemwomba ndugu yake ajihusishe na mke kimapenzi ili wapate mtoto.

Kwa wanaume ambao ni vitindamimba, siku hiyo ya harusi walikumbushwa wajibu wao kwa wazazi wao. Wanaume hao walistahili kuhakikisha kuwa *embonga* (shamba ambalo wazazi wametengewa) imelimwa vizuri, vyakula vimepandwa na kuvunwa kwa wakati unaofaa. Jukumu la kulea wazazi wao ni lao. Mbinu ya jazanda ilitumiwa katika wimbo huu ili kuwakumbusha wanaume hao hasa vitindamimba kuwa wana nguvu za kufanya kazi hasa kuenda shambani. Walilinganishwa na fahali, ambapo kimsingi fahali aliyekomaa ana nguvu kuliko ng'ombe yoyote yule. Kupitia kwa mbinu ya jazanda kwenye wimbo wa *Abagusii Bakabora* mwanamke aliyeletwa

katika boma hilo alirejelewa kama ndama, kwa hivyo kitindamimba huyo aliambiwa kuwa ana mwanamke ambaye jamii ilitarajia washirikiane katika kufanya kazi zote za shambani. Mwisho kabisa, wawili hao waliambia kuwa wasiwashau wazazi wao. Hili linadhahirika ifutavyo:

Ee eheri ya tata ereme embonga
Ee bono twagorete mbono ere nemanwa
Nabono twayegora mwanchane

Tafsiri

Ee fahali ya baba ilime shamba la wazazi
Ee ndio tulinunua na sahizi ina ndama
Ndio tumenunua mpendane

Mama Mong'ina alisema kuwa, siku ya ndoa wanawake walikumbushwa umuhimu wa kufanya kazi kwenye boma lao kupitia kwa nyimbo. Ili boma na familia iendelee kama zingine, mwanamke alisisitiziwa umuhimu wa kuenda shambani kama wanawake wengine. Akikosa kwenda shambani na kupanda vyakula familia yake ingeteseka kwa sababu ya njaa na watoto wake kugeuka kuwa ombaomba hivyo basi kukosa kuheshimiwa na watu kwenye jamii kwa jumla. Wanawake walipoenda kurandaranda na kutembea kwa boma za watu kwa ajili ya umbeya walikumbushwa umuhimu wa kutulia manyumbani mwao. Mbinu ya taswira uoni ilikuwa na nafasi kubwa sana katika kuhimiza wanawake wavivu waende shambani kufanya kazi. Kupitia kwa ubeti wa kwanza taswira ya jembe ambali ni nzuri kuanzia kwa mpini na ambalo lilinolewa vizuri lilihita jika ili kumsaidia mwanamke huyo kulima shamba lililokuwa limejaa magugu.

Katika ndoa, mwanamke alikuwa na jukumu la kuhakikisha chakula hakipungui kwenye ghala. Ili kuifiisha nasaha hii kwamwanamke siku ya ndoa kikamilifu, mtunzi

alitumia mbinu ya taswira uoni ili kueleza yale ambayo ambayo mwanake huyo alitarajiwa kutekeleza kama vile kulima shamba lake vizuri.

Mong'ere mokungu obokombe nekebago egesera
Nekebago egesera agende kwabusera omogondo
Omogondo nyakieni kebariri omaiya

Omaiya chingero bonyangero
Mokungu sioma siomi nkayi akomanya
Bwarugirwe omarwa are ase enyongo

Tafsiri

Mmepe mwanamke jembe lenye moini mzuri
Mpini mzuri aende kufagia shamba
Shamba linalopendeza

Nyimbo tamutamu
Mwanamke anayependa kuzurura amejuaje
Kumepikwa, pombe iko kwa chungu

2.2 Historia na Tamaduni na Waswahili

Kulingana na Mbaabu (1985), utamaduni unahusu mila, asili, jadi na desturi ya mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla. Waswahili ambao walikuwa wanajulikana kama Wangozi, walitoka katika eneo la Shungwaya na kuingia Pwani ya Kenya ambapo waliooana na Waarabu. Waswahili nchini Kenya wanapatikana kwenye eneo la pwani ambalo lina maeneo mbalimbali kama vile: Mombasa, Kilifi, Malindi, Lamu, Watamu na Diani.

Kulingana na Jones na Laviolette (2018), wanasema kuwa tamaduni za Waswahili ni aamaduni mbalimbali za Kiafrika zinazoundwa na mkusanyiko wa watu. Watu hawi wavuvi, wafanyabiashara, wakulima na wafugaji wa ng'ombe ambao wamehama kuingiliana katika ardhi na bahari kwa karne nyingi na la muhimu zaidi, kabla ya kuibuka kwa Uislamu mwishoni mwa karne ya nane. Tamaduni na historia ya Waswahili ni pana. Kwanza kuwapeleka wavulana jandoni, mchakato wa ndoa ambao

unahusisha wasichana kusingwa, mapishi, nyimbo za taarabu na kadhalika. Waswahili walishiriki biashara na wageni pamoja na wakenya wengine, walishiriki katika kilimo na uvuvi.

2.2.1 Ndoa

Mzee Salim alieleza kuwa wazazi walipanga ndoa za watoto wao. Kinyume na jamii ya Wakisii ambapo ndoa baina ya jamaa ni mwiko, kulingana na Knappert (2005), anasema kuwa Waswahili walishabikia ndoa baina ya jamaa zao hasa binamu. Sababu yao kuu ya kushabikia ndoa hizi ni ili kudumisha umoja miongoni mwa wanafamilia na pia kuhakikisha kuwa mali ya familia hayaendi kwingine.

Baada ya wazazi wa pande zote mbili kukubaliana kuhusu ndoa baina ya watoto wao, wazee kutoka kwa familia zote mbili wanaanza kuzungumzia kuhusu mahari. Familia ya mwanamume hutembelea familia ya msichana ili kujadili kuhusu swala hilo muhimu. Mahari uhusisha pesa, mapambo hasa ya dhahabu au vitu vingine vya thamani kwenye familia hizo. Baada ya familia hizo mbili kukubaliana, mchakato wa kupanga ndoa huanza ambapo familia hizi mbili hutembeleana sana na hata kubadilishana zawadi.

Kulingana na Maganda & Moshi (2014), wanasema kuwa matayarisho ya ndoa za Waswahili huchukua kati ya miezi mitatu hadi minne. Ambapo katika kipindi hiki sherehe mbalimbali huandaliwa. Sherehe hizi zinanuiwa kuimarisha uhusiano miongoni mwa familia hizi na pia kutimiza tamaduni mbalimbali za Waswahili. Mbinu ya taswira uoni ilitumiwa katika wimbo wa *Ndoa ni Baraka* amba oni wimbo maarufu sana katika sherehe za ndoa ili kumuonyesha mwanamke mambo anastahili kuyafanya.

Bi. Saida alieleza kuwa wanawake kutoka familia ya msichana huwa na kibarua kikubwa sana cha kumuandaa msichana kwa ajili ya maisha ya ndoa. Msichana alipelekwa unyagoni ambapo alisingwa. Wanawake wazee na ambao walikuwa ujuzi wa maisha ndio walipewa jukumu la kusinga wasichana. Bi. Saida aliendelea kueleza kuwa, kusingwa kulihusisha kufunzwa mambo mbalimbali ya ndoa kama vile: kuishi vizuri na mume wake. Msichana aliambiwa kuwa aiheshimu taasisi ya ndoa kwa sababu yeye mwenye ndiye alikuwa jukumu la kujenga au kuivunja ndoa yake. Ili ndoa yake ifanikiwe ni lazima aishi vizuri na mume wake, amheshimu na ampende milele kwa sababu kifo ndicho kilipaswa kuwatenganisha. Kando na hayo, Bi. Mwanaisha alieleza kuwa wasichana hao walisitiziwa umuhimu wa kuwaheshimu wazazi wa mume kwa sababu hiyo ndiyo familia yake mpya na pia kuishi vizuri na majirani pamoja na watu wengine kwenye jamii. Kupitia kwa taswira uoni, msichana huyo alisisitiziwa umuhimu wa kudumisha usafi wake wa kimwili, kuhakikisha kuwa mume wake ni safi na avalie mavazi safi. Kando na hayo, msichana alikumbushwa umuhimu wa kuwa na boma safi. Iliaminika kuwa asipodumisha usafi mwanamume angeweza kutoka nje ya ndoa. Kwa hivyo, usafi ni jambo la muhimu sana. Hata siku ya ndoa msichana bado anakumbushwa umuhimu wa kudumisha usafi nyumbani. Katika wimbo huu wa ndoa, taswira uoni ilitumiwa kuujenga. Ilitumiwa kuisitiza usafi wa kimwili ambao mwanamke yeyote alitarajiwa kudumisha kila wakati. Kwa mfano:

Mwanamke lazima awe safi
Kanga alisugue
Mume wako akirudi
sharti viatu kumvua

Msichana huyo pia alifunzwa kuhusu maswala ya mapenzi. Alielekezwa kuhusu mambo ambayo alistahili kuyafanya ili maisha yao ya ndo yaendeleo kuimarika.

Kupitia kwa taswira uoni, mtunzi wa *Ndoa ani Baraka* alieleza jinsi ambavyo mwanamke alistahili kuandaa chumba cha cha malazi na pia yeye mwenyewe kujitayarisha kwa ajili ya mume wake. Kwanza alikumbushwa kuhusu kuvalia shanga kiunoni. Kulingana na Knappert (2005), shanga ni sanaa muhimu sana katika jamii hii. Shanga hizi ni kivutio cha asili kwenye mapenzi. Bi. Fadhili alieleza kuwa lazima mwanamke ajue kuvalia shanga hii vizuri ili ichukuane na umbo lake. Pia alistahili kuhakikisha shanga hizo ni safi ili zimvutie mumewe. Kwa upande mwingine, mwanamume pia alikumbushwa kuwa lazima awe ufundi na utundu wa kucheza na shanga hizo. Waswahili wanaamini kwa shanga zilitumiwa kuongeza ladha kwenye mapenzi na ndio sababu zilikuwa na thamani kubwa kwao. Kwa mfano:

Mambo ya kuzima taa
Si mahaba ni kuwanga
Washa japo kamshumaa
Mmeo aone shanga.

Mzee Kombo alieleza kuwa kulikuwa na sherehe mbili za ndoa, sherehe ya kwanza ilifanyiwa msikitini kwa Waislamu na kanisani kwa Wakristo ambapo wanaume pekee pamoja na bibi arusi ndio uhudhuria kwa upande kwa Waislamu na kwa Wakristo kila mtu alikuwa na nafasi ya kuhudhuria sherehe hiyo. Sherehe hiyo ilipokamilika, arusi ya pili ya kitamaduni ilifanyika nyumbani kwa kina bibi arusi. Familia ya msichana iliandaa vyakula mbalimbali kwa ajili ya sherehe hiyo kama vile: biriani, pilau, vitumbua, mikate ya sinia na kadhalika. Wanawake walijipamba kwa kutumia mapambo mbalimbali ya kupendeza. Wanawake walivalia mavazi yao ya kitamaduni yaliyohusisha kanga na dera. Mavazi haya yaliwapa wanawake hawa nafasi kucheza densi. Nyimbo za taarabu pamoja na tenzi ndizo zilishamiri kwenye sherehe hizi kwa sababu ndizo kigezo cha kuburudisha wageni wao.

Mafunzo kuhusiana na ndoa yaliendelea hata siku hiyo ya arusi ambapo wawili hawa walikumbushwa majukumu yao. Katika kufanikisha mafundisho hayo, walitumia mbinu ya jazanda ambayo ilikuwa na jukumu la kusisitiza umuhimu wa wanandoa hao kufanya kazi. Katika wimbo wa *Ndoa ni Baraka* wanaambiwa kuwa ‘kuomba ni mwiko na raha ya chumvi ni kunua’. wanamume walikumbushwa kuhusu umuhimu wa kutia bidii na kuwajibikia familia zao kwa kuhakikisha kuwa walizumbua riziki ili ndoa yao isivunjike. Mbali na hayo, wawili hawa walihimizwa kufanya lolote wawezalo ili wasiivunje ndoa yao kwa sababu kulingana na wao ndoa ni baraka kutoka kwa Mungu hivyo wakiivunja ni kama kukufuru. Kwa mfano:

1. Baba akasema kuomba ni mwiko
Raha ya chumvi ni kununua
2. Kwetu talaka kuitoa ni kukufuru
Nimefunzwa nivumilie niushinde ujana
Ili kusudi kesho wasinong’one

2.2.2 Tohara

Tohara ilikuwa tamaaduni muhimu sana miongoni mwa Waswahili. Mzee Salim alieleza kuwa, wavulana kati ya miaka nane na miaka kumi na miwili ndio walikuwa wakitahiriwa. Sherehe hii ilikuwa muhimu sana kwa sababu ilikuwa ikiashiria wavulana hawa wametoka utotoni na kuingia utu uzima. Sherehe hizi zilianza usiku wa kuamkia siku yenyewe ya kupashwa tohara. Alieleza kuwa dhima kuu ya nyimbo hizi za tohara ilikuwa ni kuwatayarisha vijana hao kisaikolojia kuhusiana na hali ambayo wangekumbana nayo wakati wa kupashwa tohara. Kwanza walikumbushwa kuwa wangepitia uchungu mwingi sana hivyo basi lazima wangukuwa jasiri kama jogoo. Vijana hao waliambiwa kuwa uoga ni wa vifaranga na ingekuwa aibu kubwa sana kwao na ukoo mzima iwapo wangeonyesha uoga wa aina yoyote ile. Wavulana hao waliambiwa wawe jasiri ili wakumbane na kisu cha ngariba. Katika wimbo huu, mbinu ya taswira hisi ilitumiwa ili kusisitiza makali ya kisu cha ngariba. Ili

kuwasaidia vijana hawa kuelewa mazingira ya jandoni katika wimbo wa *Wewe ni Jogoo*, mtunzi alitumia mbinu ya jazanda kama vile 'jandoni si lelemama, leo tutajua tofauti kati ya jogoo na kunguru'.

Hali kadhalika, mbinu ya jazanda ilitumiwa ili kuwaonyesha wavulana hao umihimu wa kuwa jasiri kwa sababu hakuna ambaye angetaka kurejelewa kama kunguru. Kwa mfano:

Kijana kuingia jandoni si lelemama
Leo tutajua tofauti kati ya jogoo na kunguru
Kuwa tayari kukutana na kisu cha ngariba
Kilicho na makali kuwili
Ukoo wetu ni wa majagina
Ukoo wetu si wa kunguru

Mzee Abdi alieleza kuwa, baada ya wavulana kupashwa tohara walikuwa wakipelekwa jandoni (msituni) kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu ambapo walifunzwa kunga ya utu uzima. Vijana hawa walitarajiwa kuacha tabia za kitoto na kuwa na tabia za watu wazima. Wavulana hawa walitarajiwa kuchukua na kujitwika majukumu mapya baada ya kutoka jandoni. Kwanza walikumbushwa kuhusu majukumu yao kwa familia zao kama vile kushiriki katika biashara, uvuvi na ukulima ila kuhakikisha familia zao haziteseki. Kwa mfano:

Wewe mekuwa mmoja wetu
Majukumu ya familia kujitwika

Wavulana hawa pia walisitiziwa umuhimu wa kutokuwa na pupa. Hawakupaswi kukimbilia na kugusagusa vitu visivyowahusu. Walistahili kuwa na heshima kwa sababu mtu anapokimbia na kugusa vitu visivyomuhusu angeweza kujipata pabaya. Katika kuisitiza umuhimu wa kutokuwa na pupa hasa baada ya kutoka jandoni, mbinu ya taswira uoni ilitumiwa kuwaelekeza vijana hao katika wimbo huo. Hapa wavulana walikumbushwa kuwa wasifunue tandiko la mama au dada kwa sababu wangeweza

kupata mambo ya ajabu ajabu ‘mambo ya wanawake’ ambayo yangewafanya kuaibika kila wakati ambao wangekutana na mama au dada zao.

Kijanangu usifunue kinyamata cha mama
Mheshimu babayo na ninayo
Usirushe mikono yako kila mahali
Kugusagusa kisicho chako-ooo
Epuka kabisa epuka kabisa

Mzee Abadi alisema kuwa wavulana hao walipokuwa jandoni pia walionywa dhidi ya kusemasema sana. Kwa mwanamume, tabia ya kusemasema ilichukuliwa kuwa ni kukosa heshima na pia waliamini kuwa hii ilikuwa tabia ya wanawake. Sababu kuu ya kuwaonya ni kuwa wakati mwingine, mtu angeweza kuongea kuhusu jambo ambalo halikumuhusu au hajui asili yake hivyo kupelekea kuzuka kwa mgogoro miongoni mwa watu. Kwa mfano mume wa mtu fulani angeweza kumuuliza kama amemwona mke wake kisha amwambie amwona akipita mahali fulani akiwa na mtu mwingine jambo ambalo mume huyo hakuwa anajua hivyo kupelekea kuzuka kwa mgogoro kati ya wanandoa na hata kupelekea kuvunjika kwa ndoa. Kwa mfano:

Kusema kwingi achia wanawake
Usiwe na haraka ya kutangaza bila hakika
Eti wakati mwingine yule kapita yule
Hayo si yako zoea kufyata ulimili
Utavunja ndoa utavunjan ndoa fyata

2.2.3 Taarabu

Kulingana na TUKI (2004), taarabu ni muziki wa mahadhi yenye asili ya mwambao wa Afrika Mashariki unaotumia ala za mchanganyiko wa Kiarabu, Kihindi na Kizungu. Kwa mujibu wa Rougetin (1985), anasema kuwa neno *Taarabu* limetokana na neno *Tariba* ambalo ni kitenzi cha Kiarabu. Anaendelea kusema kuwa muziki huu unaingiliana sana na pwani ya Afrika Mashariki na unaingiliana na tamaduni za Waswahili na maisha yao. Kimsingi taarabu ni muziki ambao unatambulisha pwani

ya Afrika Mashariki na umekopa mtindo na mahadhi yake kutoka tamaduni mbalimbali ulimwengu na ujumbe wake umejikita katika tamaduni za Waswahili.

Kama asemavyo Jihad (2003), muziki huu ulianza katika kisiwa cha Zanzibar kati ya mwaka wa 1870-1880 ambapo ulishabikiwa sana na Sultan Seyyid kisha ukasambaa katika maeneo mengine ya pwani ya Afrika Mashariki kama vile: Mvita (Mombasa), Malindi, Tanga, Pemba na Kilwa kupitia kwa wafanyabiashara Waarabu. Anaendelea kusema kuwa nyimbo hizi ziliimbwa sana katika sherehe za mazishi na wanaume ndio walikuwa wanaziimba. Mwanamke wa kwanza kuimba taarab alikuwa Siti Binti Saad na kupitia kwa nyimbo hizi aliweza kutoa mchango mkubwa sana katika kupigana dhidi ya wakoloni.

Taarab zilikuwa maarufu sana katika sherehe za kitamaduni kama vile: sherehe za arusi, kuzaliwa kwa watoto, mazishi au maombolezo na jandoni. Kando na sherehe za kitamaduni, nyimbo hizi ziliimbwa wakati watu walipokuwa wakifanya kazi ili kuwatia motisha ya kufanya kazi. Muziki huu wa taarab ulikaribiana sana na mashairi ya kuimbwa. Ujumbe wake mkuu ulihusu maswala ya mapenzi na mahusiano. Ili kupunguza mgogoro na makali ya ujumbe wake nyimbo hizi hutumia majazi na jazanda. Kwa mfano:

Kitandani rashia marashi
Kumkanda kisha kumchua
Kisha anza sayansi- kiuno kutengua

Mambo ya kuzima taa
Si mahaba bali ni kuwanga
Washa japo kamshumaa
Mumeo aone shanga

Mbinu ya taswira mnuso ilitumiwa katika ubeti huu ili kuonyesha mwanamke aliyekuwa akiolewa siku hiyo jinsi ya kumtunza mume wake. Hali kadhalika, mbinu

ya taswira mguso ilitumiwa hasa katika kumkanda mwanamume kwani mwanamke alitarajiwa kusinga mume wake angalau mara mbili kwa wiki. Wimbo huu ni wa taarabu ambao uliimbwa wakati wa ndoa. Bi. Hadija alieleza kuwa wimbo wa *Ndoa ni Baraka* ulitumiwa kutoa nasaha kwa bibi arusi kuhusu maswala ya kindoa. Mwanamke alikumbushwa kuwa anapoingia chumbani lazima angehakisha kuwa yeye ni safi na lazima awe ananukia ili kumvutia mume wake. Waliposema kuhusu *kisha anza sayansi-kiuono kutengua* mwanamke aliambiwa mambo ya kumfanyia mumewe ili aweze kumsisimua. Kando na hapo ubeti unaofuata unazungumzia kuhusu kuwasha mshumaa wakiwa chumbani, jamii hii ilitumia mishumaa kwa majukumu mbalimbali. Kuna baadhi ya mishumaa ambayo ilinukia sana, mishumaa kama hii iliaminiwa kuwa ingeleta au ingeongeza mahaba kati ya wanandoa na ule mwanga hafifu uliaminiwa kuwa ungewasaidia wasipate ajali yoyote na pia ungeleta mvuto wa aina fulani chumbani.

Kando na sherehe za arusi, taarabu pia ziliimbwa katika sherehe za mazishi. Katika sherehe hizi, nyimbo hizi zilitumiwa kuwafariji waliofiwa. Mbinu ya taswira hizi ilitumiwa katika ubeti ili kuonyesha hisia za waliofiwa na pia kuonyesha hali ya kuridhia kifo chenyewe. Baadhi ya watu walipowapoteza wapendwa wao, walihisi kuwa maisha hayana maana tena. Walihisi kuwa maisha yamekuwa ombwe tupu kiasi kwamba wakatamani kuwafuata wapendwa wao walioaga dunia. Hali kadhalika, waliofiwa walitumia nyimbo hizi kama sifo kwa marehemu na pia kudhihirisha mapenzi yao kwa mwendazake.

Ni wakati wa kusema kwaheri
Siamini kuwa umeenda kabisa
Huu ni usingizi wa milele
Nitaendelea kuimba taarab zisizo mwisho
Kwa sababu nakupenda sana

2.2.4 Sherehe za kuzaliwa kwa mtoto

Kuzaliwa kwa mtoto ni jambo muhimu sana katika jamii hii. Bi. Pendo baada ya mtoto kuzaliwa tu, mkunga na akina mama waliomsaidia mama huyo kujifungua walimwosha mtoto huyo kisha wakampa shubiri na asali. Katika riwaya ya Utengano ya Mohamed (2010), tunamwona mhusika kwa jina Farashuu akiamrisha aletewe asali na shubiri ili mtoto alambishwa. Biti Kocho alimlambisha mtoto wa Maksuudi shubiri akapiga ukwenzi mkali sana. Kisha Biti Kocho akamwambia huo ndo uchungu wa dunia kwani itamwandama atake asitake hivyo wanampika ili asilalame. Kisha wakamlambisha asali ambayo aliambiwa ndiyo zindiko. Akamwombwa Mungu amjalie, ghiliba za dunia zisimkute au azionje kidogo tu, kisha aone tamu ya dunia moja kwa moja.

Sawa na ilivyo katika riwaya hiyo katika wimbo wa Allah Akulinde, mbinu ya jazanda ilitumiwa katika kusawiri kiviga ambacho watoto hufanyiwa punde tu wanapozaliwa, katika jamii mtotoalilambishwa shubiri na kwa sababu ni kali mtoto huyo lazima angelia. Bi. Pendo alieleza kuwa shubiri hiyo ilitumiwa kumkumbusha mtoto kuwa duniani kuna shida na changamoto nyingi kama vile: vifo, magonjwa, njaa, vita na umaskini ila alistahili kuwa mstahimilivu. Katika mkondo wa pili, mtoto huyo alilambishwa asali, kilio cha mtoto yule kilikuwa kinakatika ghafla kwa sababu asali ni tamu. Asali ilikuwa ishara ya mazuri ambayo angeyapata maishani na yakija aliambiwa ayafurahie kadri ya uwezo wake. Mbinu ya mtindo iyolitumiwa kufanikisha utamaduni huu ilikuwa ni mbinu ya jazanda ambapo asali na shubiri zilitumiwa kuashiria tamu na chungu ya maisha mtawalia.

Mwanangu usiyapapie maisha
Tulikupa asali na shubiri
Kumbuka utakuwa na siku za huzuni
Ila siku hizo zitapita

Siku za furaha zikifika zifurahie
Zisherehekee mwanangu

Bi. Fadhili alieleza kuwa baada ya siku ya saba, sherehe ndogo iliandaliwa. Sherehe hii ilikuwa na malengo mbalimbali. Kwanza mtoto alipewa jina, jina la kwanza kimsingi lilstahili kuwa la dini. Jina la pili lilikuwa muhimu sana kwa sababu liliweza kudhihirisha ukoo wa mtoto (jina la babu au nyanya au jamaa wao wa karibu aliyeaga dunia). Watoto pia walipewa majina kutokana na viongozi maarufu kwenye jamii ambao walichangia katika kuiendeleza jamii. Siku hizi utamaduni huo unaenda ukififia kwa sababu wengi wanafuata tamaduni za watu wa Magharibi.

Kando na kumpa jina, mtoto alizungushwa katika kila chumba kule nyumbani mwao huku akielezwa umuhimu wa kila chumba. Waliamini kuwa kumzungusha mtoto kwenye kila chumba kungemfanya ahisi kuwa yeye ni mwenyeji wa pale na kufukuza hisia zozote za woga. Shuguli hii iliendelezwa na wazee wa dini, akina mama teule na wakunga. Siku hiyo pia kafara ilitolewa ya kumwomba mtoto awe na afya njema na pia kuwatakiwa wazazi wa mtoto huyo mema wanapoendelea kumlea kwa sababu wanaamini kuwa *‘Kuzaa si kazi kazi ni kulea.’*

Bi. Mwanaisha alieleza kuwa mama na mtoto walistahili kupumzika kwa muda miezi miwili hivi. Muda huu ulitumiwa na akina mama wa kijiji kumwelekeza mama huyo kuhusu njia bora za kumlea mtoto na pia jinsi ya kuishughulikia familia yake hasa yule ambaye amejifungua kwa mara ya kwanza. Muda huu pia ulitumiwa na wazazi wa mtoto (baba na mama) kuimarisha uhusiano wao na mtoto wao. Wazazi hao hasa mama walipewa jukumu la kumfunza na kumwelekeza mtoto wao. Miezi hiyo miwili pia ilitumika katika kumkinga mama na mtoto kutoka kwa mahasidi na watu wenye wivu kwa sababu watu wa aina hiyo waliweza kuwaendea kwa waganga na kusababisha kifo au ugonjwa kwa mama au mtoto au kwa wote wili.

Mtoto alipozaliwa, jamii ilikuwa na matarajio mengi ambayo walimweleza mtoto huyo kupitia kwa nyimbo katika sherehe ya kuzaliwa. Kwa mfano, katika *Siku Njema* mbinu ya kisengere mbele ilitumiwa katika kuonyesha matarajio ya jamii kwa mtoto huyo has awa kiume. Bi. Hadija alisisitiza kuwa nyimbo ambazo ziliimbwa katika sherehe hiyo zilikuwa muhimu sana kwani zilitumiwa kumwelimisha mtoto huyo kuhusu majukumu yake na matarajio ya jamii kwake. Matarajio ya jamii kwa mtoto huyo yaliwasilishwa kupitia kwa kisengere mbele. Mtoto huyo alitarajiwa kushiriki katika shughuli mbalimbali kama vile: ukulima na uvuvi hasa kwa watoto wa kiume. Kilimo na uvuvi zilikuwa shughuli muhimu sana katika jamii hii katika kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Naingoja siku ambayo utakuwa dume
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavue ulete dagaa
Ila itabidi tuwe wavumilivu

Aidha, nyimbo za kuzaliwa kwa watoto zilitumiwa kuwafunza watoto hao umuhimu wa kudumisha maadili ya hali ya juu. Watoto hawa walistahili wawe wenye heshima kwa kila mtu. Wazingatie sheria za jamii na sheria za dini. Iliaminiwa kuwa mtoto alikuwa kioo cha wazazi. Kama wazazi walikuwa wazuri na wenye maadili, basi mtoto huyo angekuwa na hulka nzuri na ikiwa wazazi walikuwa na malezi mabovu, watoto hao wangekuwa na hulka mbovu. Kila familia ilitaka ipate sifa kutokana na hulka nzuri za watoto wao.

Kuwa mwanamume mnyenyekevu
Mwanamume mwenye maadili
Usimbague yeyote
Usiwe mwenye tamaa ya mali
Ridhika na vichache vyako
Nakuomba uzingatie haya kwa ajili yangu

2.2.5 Kanga/Leso

Kanga ni miongoni mwa vazi muhimu la Mswahili na limekuwa na dhima kubwa katika kutekeleza majukumu ya kiutamaduni. Vazi hili limekuwa kielelezo tosha cha usawiri wa matukio ya kijamii. Kulingana na Timmamy na Swale (2016), ulimwengu wa kanga au lesu ni ulimwengu wa uzuri, rangi za kupendeza, nakshi changamano, mavazi ya kusitiri na papo hapo kupitisha ujumbe fulani kupitia methali, misemo na misimu. Bi. Pendo alipoulizwa kuhusu dhima ya kanga ambazo zilikuwa maarafu sana miongoni mwa wanawake wa pwani, alieleza kuwa uvaaji wa kanga huzingatia rangi, maua na semi kwa kuangalia muktadha halisi wa mvaaji wa kanga hizo. Kanga zinazovaliwa msibani, ni tofauti kabisa na kanga zinazovaliwa harusini kwa semi, maua na hata rangi yake. Vyote hivyo hujenga taswira halisi ya mvaaji, kwa kufikiria lengo la uvaaji wa vazi hilo.

Kanga ina matumizi anuwai ya jamii, ni ya mapambo katika sherehe mbalimbali za kijamii. Kwa mujibu wa Yahya-Othman (1997), anaeleza kuhusu umbo la kanga, anasema kuwa lesu au kanga ni kitambaa cha umbo la mstatili kilichotengenezwa kwa pamba chenye urefu wa mita moja unusu na upana wa mita moja na sentimita kumi na ambacho hutarajiwa kumfunika mvaaji kutokea kifuni hadi karibu na jicho la mguu. Ijapokuwa siku hizi kuna nyingine ambazo ni kubwa zaidi na hujulikana kama lesu za 'kuswalia' miongoni mwa Waswahili kwa sababu hutumika na wanawake kujifunga wakati wa kuswali. Kanga chache zimeundwa kwa masuala maalum kama vile matukio muhimu ya kitaifa, kuinua jamii, ufahamu na masuala yanayohusiana na sherehe za kidini. Kutokana na kanga mbalimbali ambazo zilitumiwa wakati wa utafiti, iligunduliwa kuwa majina na kauli za kanga hufichua tamaduni na mambo mengine muhimu ya Waswahili. Pia, kanga hutumika kama sehemu ya fasihi simulizi kwa lengo la kuburudisha nyoyo za wavaaji na wavalijaji na kutoa ujumbe

uliokusudiwa na mvaaji huyo. Kama asemavyo Malangwa (2012), anaeleza kuwa fasihi inayowasilishwa katika muktadha huu wa kanga ni fasihi yenye maana pana na yenye kina kirefu na uhalisi zaidi, kutokana na kuwa ni fasihi ya maneno na vitendo. Bi. Amani alisema kuwa Waswahili hawatumii kanga kama vazi la kujistiri tu, bali hutumia kama ni sehemu ya kuenzi mila na utamaduni wa jamii hiyo. Anaendelea kueleza kuwa katika jamii hii, wanaume wanaweza kutumia kanga ili kuonyesha mapenzi yao kwa wake zao. Kwa mfano mwanamume anaweza kumnunulia mwanamke kanga inayosema kuwa ‘Mpende akupendaye’. Kupitia kwa kanga hii ujumbe unaopitishwa ni kuwa ili mapenzi au ndoa ifanikiwe wote wawili wana nafasi sawa, kila mmoja ampende mwenzake. Kanga nyingine yaweza sema ‘Japo kidogo chatosha kwa wapendanao’. Kauli hii ilitumiwa hasa kwa wanawake ambao walitoka kwa familia iliyo na mali mengi kisha akaolewa na mtu ambaye hana utajiri. Hivyo alikuwa anahimizwa kuwa akiridhika na kile kidogo ambacho wanamiliki kitaosha kwa sababu ya mapenzi.

Kabla ya mwanamke kuolewa alifunzwa mambo aliyostahili kuyafanya. Mtunzi alitumia taswira uoni katika wimbo huu ili kuonyesha majukumu ya kanga. Hali kadhalika, mbinu hii ilitumiwa kuonyesha kuwa kila mwanamke lazima amiliki kanga na lazima iwe safi ili kumvutia mume wake. Alisitiziwa adumishe usafi wa kimwili na mazingira. Mavazi yake yote kwa mfano kanga na mapambo kama vile shanga lazima yangedhihirishe usafi wa hali ya juu. Mwanamke alipokuwa chumbani alikuwa anavalia kanga mbalimbali ambazo zilikuwa zikionyesha hisia zake. Kwa mfano, akiwa kuna jambo ambali lilikuwa limemkasirisha, mwanamke angevalia kanga ambayo iliyobeba ujumbe huo. Iwapo mwanamume ndiye alikuwa amemkosea, aliomba msamaha ili kudumisha amani. Kanga hizi zilikuwa muhimu sana hasa kwa wanawake kwani katika jamii hii, mwanamke hakuwa na nafasi ya kumgombeza

mume wake, alitarajiwa kumheshimu hata ikiwa mume huyo alimkasirisha. Wanawake pia walitumia kanga hizo kuonyesha mapenzi ambayo walikuwa nayo kwa waume zao. Kwa mfano kuna kanga ambayo ina msemu ufuatao, Nimepata la azizi dawa ya roho yangu'. Msemu huu ulikuwa ishara tosha kuwa mwanamke huyo alikuwa anampenda mume wake na ameridhika naye. Hata anamlinganisha kama dawa ya roho yake. Hivyo basi wanawake wenye hekima ya ndoa walisisitiza wanawake hao kuvaa kanga, wahakikishe kuwa ni safi na kanga zenyewe ziwe na ujumbe mwafaka kwa sababu hiyo ilikuwa njia moja ya kuwasiliana. Umuhimu wa kanga ulidhihirishwa hasa kupitia kwa sherehe zao, katika sherehe za arusi taswira uoni ilitumiwa katika kumwelekeza mwanamke huyo jinsi ambavyo angetumia kanga ili kutekeleza majukumu mbalimbali. Ili kanga yenyewe itekeleze majukumu yake, mwanamake huyo alikumbushwa kuwa lazima ingekuwa safi na yenye rangi za kuvutia.

Mwanamke lazima awe safi
Kanga alisugue
Mume akirudi sharti viatu kumvua

2.3 Hitimisho

Katika sura hii tulikuwa tukiangazia jinsi mbinu za mtindo zimetumiwa kuendeleza historia na tamaduni za jamii teule. Tuliweza kubaini tamaduni za jamii hizi mbili kama jinsi ambavyo taasisi ya ndoa inahitaji heshima. Mtu yeyote ambaye alikuwa anaingia kwenye taasisi hiyo, alikumbushwa kuwa hakuna nafasi ya talaka. Hali kadhalika, tulibaini kuwa kuzaliwa kwa watoto kulikuwa muhimu sana hasa watoto wa jinsia ya kiume. Watoto hawa waliandaliwa sherehe kubwa ya kuwakaribisha rasmi kwenye jamii. Pia tuliangazia uhasama uliokuwepo katika jamii ya Wakisii na majarani zao kama Wamaasai na Wakipsigis ambapo walikuwa wanapigania mifugo na hata maeneo ya kulisha mifugo wao hasa msimu wa kiangazi. Kutokana na

mgogoro huu, jamii hizi zilipoteza watu kwa wingi. Pia tuliangazia taarabu na hata asili yake na jinsi ambavyo jamii ya Waswahili ilienzi nyimbo hizo. Isitoshe, tuliangazia vita vya kwanza vya dunia na athari ya Vita vya Kwanza vya Dunia na athari za vita hivyo kwa jamii ya Wakisii. Vita hivi vilibadilisha mkondo wa maisha ya jamii. Katika sura inayofuata, tutaangazia jinsi ambavyo mbinu za kimtindo zimetumiwa katika nyimbo za jadi za jamii teule

SURA YA TATU

KUHAKIKI MBINU ZA MTINDO KWENYE NYIMBO ZA JADI ZA JAMII YA WAKISII NA WASWAHILI

3.0 Utangulizi

Lengo kuu la sura hii ni kushughulikia mbinu za lugha ambazo zimetumiwa katika kufanikisha uwasilishaji wa nyimbo teule za jadi za jamii husika. Kama tulivyoeleza awali wamitila (2018) anasema kuwa mtindo ni mbinu au sifa zote zinazoweza mtunzi kupitisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Anaendelea kusema kuwa mtindo hufafanua namna ambavyo mtunzi anavyoijenga kazi yake. Mbinu za mtindo ambazo zimeangaziwa katika sura hii ni kama zifuatazo: Jazanda, tashihisi, taswira, tashibihi, takriri/uradidi, kinaya, methali, kisengere nyuma, nidaa, chuku, maswali ya balagha, tabaini na tanakuzi.

Kwa sura hii mihimili mbalimbali ya nadharia ya kimtindo ilitusadia katika kutambua, kuelewa na kuchambua mbinu mbalimbali za kimtindo zilizotumiwa kwenye nyimbo teule za jadi. Kwanza kiwango cha utambuzi ambacho kilishughulikia jinsi ya kutamka na kuandika mitindo mbalimbali ya lugha. Kupitia kwa mhimili huu, tuliweza kushughulikia mbinu kama vile takriri, maswali ya balagha, nidaa na kadhalika. Pili, kiwango cha umbo ambapo msamiati uliangaziwa na jinsi msamiati huo ulitumia kutunga sentensi sahihi. Katika mhimili huu mbinu za lugha kama vile jazanda, methali, chuku ziliwekwa wazi. Mwisho kabisa, ni mhimili wa kiwango cha semantiki ambacho kinashughulikia maana inayoibuliwa na lugha ambayo mtunzi ameamua kutumia. Ujumbe ambo uliwasilishwa na mbinu kama vile taswira, kisengere nyuma, jazanda, maswali ya balagha ulieleweka.

3.2 Mbinu za Mtindo Katika Jamii ya Wakisii

Nyimbo za mtindo katika jamii hii ambazo zimedhihirika katika nyimbo za jadi ni kama zifuatazo:

3.1.1 Jazanda

Kulingana na Rioba (2022), anasema kuwa jazanda ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kutumia viungo ‘ni’ ama ‘kuwa’. Anaendelea kueleza kuwa jazanda humchorea mtu picha/taswira fulani akilini ili alinganishe vitu viwili au hali mbili kabla ya kupata jibu. Kulingana na kamusi ya TUKI (2019), jazanda ni picha inayomwingia mtu kichwani naye King’ei na Kemoli (2001), wasema kuwa jazanda ni ulinganishi wa moja kwa moja wa vitu viwili bila matumizi ya vilinganisho. Kwa jumla, jazanda ni kulinganisha vitu au hali moja kwa moja bila kutumia vilinganishi.

Eng’enang’eni yabarire, eee-yabarire eee-yabarire

Tafsiri

Nyota imeng’aa, naam imeng’aa naam imeng’aa

Wimbo huu ni wa kusherehekea kuzaliwa kwa mtoto katika jamii ya Wakisii. Jazanda imetumiwa katika mshororo huu *eng’enang’eni yabarire* (nyota imeng’aa), mtoto ambaye amezaliwa alirejelewa kama nyota. Mtoto huyo aliaminiwa kuwa angeleta mwanga kwa familia yao na hata kwenye ukoo mzima. Alionwa kuwa ishara ya mambo mazuri ambayo yangetokea hasa katika kuendeleza kizazi na ukoo wao. Ikiwa ni mtoto wa kiume wazazi walipata mtu wa kuridhi mali yao, ikiwa ni mtoto wa kike wazazi wangepata mali kupitia kwa mahari wakati msichana huyo atakapolewa. Pia

jamii ya jadi ya Wakisii ilithamini kuwa na watoto wengi kwa sababu wangewasaidia wazazi wao katika kazi kama vile kulima na kuchunga mifugo.

Nyaboke orure omote igoro

Tafsiri

Nyaboke ametoka juu ya mti

Wimbo huu ulitumiwa kumpongeza mama aliyejifungua na kusherehekea mtoto aliyezaliwa. *Nyaboke orure omote igoro* (Nyaboke ametoka juu ya mti) haimaanishi kuwa Nyaboke alikuwa juu ya mti hivyo basi akashuka bila shida yoyote. *Koba omote igoro* (kuwa juu ya mti) ina maana kuwa mwanamke alikuwa mja mzito. *Orure omote igoro* (ametoka juu ya mti) ina maana kuwa mama amejifungua salama bila shida yoyote; mama na mtoto wa salama. Kipindi chote cha kuwa mja mzito ni kipindi hatari sana kwa mama na kwa mtoto aliye tumboni. Kutokana na hatari hiyo, walirejelea kipindi hicho kama ‘kuwa juu ya mti.’ Katika hali ya kawaida mtu anapokuwa juu ya mti anaweza akataleza na kuanguka hivyo basi kuumia au kuaga dunia. Katika kipindi hiki jambo lolote lingetokea na kupelekea mama huyo kupoteza ujizo wake au yeye na mtoto kuumia. Katika kipindi hicho mama huyo alitunzwa vizuri na familia yake ikiwemo mume wake na mama mkwe. Mama huyo hakutarajiwa kufanya kazi ngumu ambazo zingeweza kuhatarisha maisha yake au maisha ya mtoto wake. Kulingana na NIH (2019), kipindi kile cha miezi tisa ya uja uzito chaweza kuwa na athari nzuri au athari mbaya kwa maisha ya mama na mtoto wake. Hivyo basi mama huyo anapaswa kula chakula chenye virutubisho bora, anywe maji mengi, anapaswa kufanya mazoezi ya kila mara kama vile kutembea ili kumzuia mama huyo kuwa na uzito kupita kiasi na kupata pumziko na usingizi wa kutosha. Hivyo katika jamii hii, baada ya mama kujifungua salama, jamii ilimpongeza mama

huyo kwa kutunza ujauzito wake kwa kumuandalia sherehe kubwa. Sherehe hii pia ilinuia kumkaribisha mtoto huyu nyumbani.

Etwani rende yara

Tafsiri

Nilidhani nimekuwa jogoo

Huu ni wimbo ambao ulioimbwa wakati wa harusi. *Etwani* (jogoo) ilikuwa maana ya kijana ambaye ametahiriwa na amekomaa na amepitia mafunzo mbalimbali kuhusiana ndoa na utu uzima hivyo basi alikuwa tayari kuanza familia yake kupitia kwa ndoa. Wimbo huu ulikuwa unaelekezwa kwa mwanamume yeyote aliyekuwa na pupa katika kuingia taasisi ya ndoa na kupuuza ushauri wa kubwa wakubwa wake. Jambo kuu ambali lilikuwa linaifanya familia hiyo kuipinga ndoa ni kuwa hakuwa amefikia umri wa kuoia hivyo basi hakuwa na mafunzi ya kutosha ya ndoa. Hali hii ilidhihirika ifuatavyo:

Obeire buna eheri, aegwe obweri bwaye

Tafsiri

Yeye ni kama fahali sasa, hivyo basi apewe zizi lake

Wimbo huu ni wa jandoni. Mojawapo ya tamaduni za jadi ambazo jamii ya Wakisii iliendeleza ni ya kuwapeleka wavulana jandoni. Sherehe hii iliandaliwa mwezi wa Agosti na Disemba kila mwaka. Nyimbo ambazo ziliimbwa jandoni zilikuwa za kuwatayarisha wavulana hao kwa maisha ya utu uzima na pia kukumbusha familia ya waliotahiriwa kuhusu mambo waliyostahili kuwafanyia waliotahiriwa. *Aegwe obweri bwaye* (apewe zizi lake) zizi hapa ina maana ya kumbi au makao yao. Nyumba hii kwa jamii ya Wakisii inaitwa *esaiga*. Baada ya wavulana kutiwa jandoni hawakupaswa kuishi kwenye nyumba moja na wazazi au dada zao na hawakupaswa

kuingia katika chumba cha malazi cha wazazi kwa sababu ni mwiko. Mvulana huyo alistahili kuishi kwenye nyumba yake ambayo ilijengwa mbali na wazazi wake. Kuishi katika nyumba yake kulimpa mvulana huyo nafasi muhimu ya kuwa jasiri na hata ya kujitegemea. Nyumba hii ilichukuliwa kama mbinu moja ya kumkomaza mvulana huyu. Hivyo kupitia kwa huu wimbo wazazi na walezi walikumbushwa kuwa huyo mvulana amekuwa fahali hivyo anastahili kupewa zizi lake.

3.1.2 Tashihisi/Uhaishaji

Kulingana na Rioba (2022), tashihisi ni mbinu ya kukipa uhai na sifa za kibinadamu kitu kisicho na uhai. Mbinu hii hujumuisha kupeana sifa za kibinadamu haswa matendo ya binadamu kwa viumbe kama vile wanyama, wadudu na ndege. Naye Wamitila (2004), anaeleza tashihisi kuwa ni kitu kisichokuwa na uhai au uwezo wa kuhisi (urazini na kumsalimu) wa kibinadamu kinapewa sifa hiyo. Kwa njia hii mvuto wa kisanaa unapatikana. Huweza pia kutumiwa ili kuleta athari fulani ya kihisia. Kwa mfano: *miti ilimwinamia na kumsalimu*. Kulingana na kamusi ya TUKI (2019), tashihisi imeelezwa kuwa ni usemi wenye kukipa kitu kisicho uhai sifa ya kitu chenye uhai. Kwa mfano:

Egesaku giato bono giatenenire, eee giatenenire eee giatenenire

Tafsiri

Ukoo wetu umesimama, eee umesimama eee umesimama

Wimbo huu uliambwa baada ya mtoto kuzaliwa. Kulingana Mama Bangweso, wimbo huu ulitumiwa kuonyesha furaha ambayo wanakijiji walikuwa nayo kutokana na kuzaliwa kwa mtoto. Katika mshororo huu, ukoo ulipewa sifa ya kibinadamu ambayo ni kusimama. Kusimama kulileta dhana ya kuwa ukoo wao ungeendelezwa kwa sababu mtoto aliyezaliwa ambaye angeendeleza kizazi chao hivyo basi hofu

waliokuwa nayo imeondoka kabisa. Kutokana na kuendelezwa kwa kizazi chao, watu walifurahia sana.

Obori bwa baba matogoro

Tafsiri

Wimbi ambao uko shambani unakodoa macho.

Obori bwa baba keande, ni wimbo ulioimbwa wakati wa mavuno hasa ya wimbi uliponawiri shambani. Wimbo huu uliimbwa kuwakumbusha wakulima wamakinike hasa katika kulinda mavuno hayo ili yasiharibiwe na nzi au ndege. Kulingana na Mama Mokeira, *matogoro* (kukodoa macho) hii ni tabia ya binadamu kwa sababu binadamu ana macho. Hii dhana ya *matogoro* (kukodoa macho) ina maana kuwa wimbi ulikuwa umenawiri na kukomaa vizuri hivyo basi wakulima walistahili kujitayarisha kwa mavuno.

Enchara nembe, yaitire Omogusii

Tafsiri

Njaa ni mbaya, imeuwa Mkisii

Wimbo huu ulikuwa unaimbwa msimu wa mavuno. Ulinuia kuwakumbusha wakulima watumie chakula chao vizuri kwa sababu wakati wa msimu wa njaa, watu walikufa kwa sababu hawakuwa na msaidizi. Ulitumiwa kuwatahadharisha kwa sababu hata majirani wao walioishi Kisumu hawakuwafaa wakati wa kipindi hicho kwani kuna baadhi ya Wakisii waliofia pale Kisumu. *Yaitire* (imeua) mbinu hii ilitumiwa kuonyesha madhara ya njaa. Njaa ilipewa uwezo wa kuu binadamu. Mbinu hii ilisisitiza kuwa njaa si kitu kizuri kwa sababu jamii inaathiriwa vibaya sana. Mbinu hii inatumiwa ifuatavyo katika wimbo huu:

Makweri aeteire emerango
Makweri aeteire chitirisa
Mkaweri aeteire ebirama

Makweri tamanyeti omogaka
Makaweri tamanyeti omog'ina
Makweri tamanyeti abana

Makweri tamanyeti omotaka
Makaweri tamanyeti omonda
Makweri tamanyeti omorai

Tafsiri

Kifo kimepitia kwenye milango
Kifo kimepitia kwenye madirisha
Kifo kimepitia kwenye paa

Kifo hakitambui mzee
Kifo hakitambui mama
Kifo hakitambui watoto

Kifo hakitambui maskini
Kifo hakitambui tajiri
Kifo hakitambui kiongozi

Mzee Onyancha alieleza kuwa mtu alipoaga dunia kwenye jamii yao, sherehe kubwa ya kuomboleza kifo hicho iliandaliwa. Katika wimbo huu *Amakweri* (Kifo) mbinu ya tashihisi ilitumiwa kwa kiasi kikubwa sana katika kuuendeleza. Katika ubeti wa kwanza tashihisi ilidhihirika pale ambapo kifo kilipewa uwezo wa kutembea au kutoka sehemu moja hadi nyingine. Walipoimba kuwa kifo kinapitia kwenye dirisha, milango na hata kwenye paa tashihisi hiyo ilidhihirika wazi. Hali kadhalika, tashihisi ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo idadi ya vifo kwenye jamii ilizidi kuongezeka kila kuchao jambo ambalo lilisababisha uchungu mwingi kwani watoto wengi walibaki mayatima na wengi kwenye jamii waliwapoteza wapendwa wao. Katika ubeti wa pili na wa tatu, tashihisi pia ilitumiwa kwa kiasi kikubwa sana. Kifo kilipewa uwezo wa kutotambua watu mbalimbali au kutobagua watu kwenye jamii kwa sababu kinachukua wazee, akina mama, watoto, matajiri, maskini na viongozi.

3.1.3 Taswira

Dhana ya taswira imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kama ifutavyo; kulingana na Wamitila (2018), taswira ni picha ambazo humjia msemaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Je, picha hizo hutokana na nini? Picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi. Anaeleza pia taswira ni kule kuitumia lugha ambayo inamfanya msikilizaji au hadhira iweze kuunda picha akilini. Mtambaji anaweza kuitumia lugha au tamathali za semi kwa mfano, sitiari, kuunda picha hizi. Kwa mujibu wa Ntaragwi (2004), taswira ni picha zinazojengeka akilini mwa mtu baada ya kusoma, kutazama au kusikiza maelezo fulani. Maelezo hayo yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni tu lakini huathiri hisia za hadhira. Anaendelea kusema kuwa taswira hutokana na tajriba pamoja na mazingira ya msimulizi na hadhira

Kama wasemavyo Njogu na Chimerah (1999), taswira humsaidia mhakiki kuelewa kazi ya fasihi kwa kina kwa kutambua maana mbalimbali zinazowasilishwa kwa kutumia aina mbalimbali za taswira. Kulingana na kamusi ya TUKI (2019), taswira kama picha au mambo au vitu inayomjia mtu akilini mwake. Wataalamu hawa wote wanakubaliana kuhusu aina za taswira ambazo ni: *taswira mwendo*, *taswira uoni*, *taswira sikivu*, *taswira hisi*, *taswira mwonjo*, *taswira mguso* na *taswira mnuso*. Kulingana na Senkoro (2011) ni kuwa, matumizi mazuri ya taswira hutegemea utunzi wa msanii wa kuweza kuchota mambo yanayomzunguka, yale yanayoizunguka jamii yake na pia kutoka katika historia na sehemu nyingine za maisha azijuazo. Taswira imedhirika kwa njia zifuatazo;

Taswira hisi

Kwa mujibu wa Senkoro (1988), anaeleza taswira hisi kuwa ni taswira ambazo zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kufanya ujumbe kunata kwa wasikilizaji au wasomaji wa shairi. Ijapokuwa taswira hii huingiliana na zile zinazoonekana, taswira hisi hushughulikia hisi za ndani. Hisia zaweza kuwa za furaha, uchungu, woga na hasira. Kulingana na Kuvuna na wenzake (1992), wanafafanua zaidi kuhusu taswira hii wanaposema kuwa taswira zinaweza kuibua hisia mbazo humfanya mhusika kuwa na msukumo wa kutenda kitu fulani. Anaweza kuamua kuteta, kupigana au kujiepusha. Kwa mfano;

Oiboirwe omwana omoke
Baminto rero no'mogoko, ee no'mogoko, ee no'mogoko

Tafsiri

Amezaliwa mtoto mchanga
Watu wetu leo ni siku ya furaha, ee ni furaha, ee ni furaha

Mama Onchari alisema kuwa wimbo huu uliimbwa wakati mtoto alipozaliwa. Watu hawa walikuwa na hisia za furaha kwa sababu ya mtoto aliyezaliwa ndio sababu walikusanyika ili kusherehekea. Kuzaliwa kwa mtoto katika familia ilikuwa ishara ya baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mababu zao kwa sababu jamiii iliamini kuwa kizazi cha familia hiyo kingeendelezwa.

Makweri aeteire emerango
Mkaweri aeteire chitirisa
Makweri aeteire ebirama
Akoira abanto ebitongo

Tafsiri

Kifo kimepitia kwenye milango
Kifo kimepitia kwenye madirisha
Kifo kimepitia kwenye paa
Kinasababishia watu kovu!

Kupitia kwa ubeti huu, hisia za uchungu na huzuni zilidhihirika kwa sababu ya vifo ambavyo vilitokea. Hisia hizi zilisisitizwa hasa kwa kuorodhesha mahali mbalimbali ambapo kifo kimepitia ikiwa ni ishara ya kifo kutokea kila mara. Jambo ambalo liliwaletea majonzi ya kila mara hivyo kuwafanya wakose furaha maishani.

Ng'ai ndarusie omwana onde?
Ng'ai ndarusie omwana onga onde?

Tafsiri

Nitatoa mtoto mwingine wapi?
Nitatoa mtoto mwingine wapi?

Katika ubeti huu, mzazi aliyefiwa na mtoto wake na alikuwa hisia za huzuni na uchungu. Swali kuu alilolijiuliza hapa ni kuwa angepata mtoto mwingine wapi? Kwa sababu kulingana na mzazi huyo hakuna mtu ambaye angeweza kuziba pengo au hakuna mtoto angeweza kuchukua nafasi iliyoachwa na mtoto wake aliyeaga dunia.

Enchara nembe, yaitire Omogusii
Enchara nembe, enchara nembe

Tafsiri

Njaa ni mbaya imeua Mkisii
Njaa ni mbaya njaa ni mbaya

Hisia za huzuni zinadhihirika kupitia kwa mishororo hii. Hisia hizi zinatokana na janga la njaa ambalo liliikumba jamii ya Wakisiii ambapo watu wengi waliaga dunia,

si watoto, si vijana, si wazee. Maafa hayo yalisabibisha vilio na huzuni miongoni mwao. Baada ya janga hilo, jamii hii ilijaribu juu chini ili kuepuka janga kama hilo kutokea tena kupitia kwa kilimo, kuhifadhi mazao yao vizuri na kuwakumbusha watu kile kilichotokea.

*Obeire omomura, obeire omomura ee-yoo!
Bono mambia, bono mambia ee-yoo!
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo.*

Tafsiri

*Amekuwa mwanamume amekuwa mwanamume ee-yoo
Sahizi asubuhi sahizi asubuhi
Anolewe mkuki pamoja na ngao*

Wimbo huu wa jandoni ulidhihirisha furaha ya wanajamii kuhusiana na wavulana ambao walipashwa tohara. Walifurahia kwa sababu sasa walikuwa watu zaidi ambao wangedumisha usalama kijijini. Kando na kudumisha usalama wanajamii walifurahia kwa sababu wavulana hawa wangewasaidia katika kurejesha mifugo ambao waliibwa na majirani wao kwani wizi wa mifugo ulikuwa donda sugu kwao.

Obori bwa baba keande
Ee keande, obori bwa baba keande

Tafsiri

Wimbi wa nyanya wamependeza
Ee wapendeza wimbi wa nyanya pendeza

Wanajamii walidhihirisha hisia za furaha. Watu hawa walifurahia kutokana na mazao yao ambayo yalinawiri shambani. Mtu anapopanda mbegu si lazima apate mazao mazuri, wakati mwingine mimea hiyo yaweza kuvamiwa na wanyama au ndege au yakakumbwa na magonjwa. Hivyo basi, mazao yao yaliponawiri wanajamii hao hawakuwa na budi ila kuyafurahia mazao yao.

Taswira Sikivu

Kulingana Wamitila (2018), anasema kuwa katika taswira hii msanii analenga kusikia kwa kujenga picha zinazohusiana na sauti. Kwa mfano;

Ekebwe ngiakura Manga nse!

Tafsiri

Mbweha analia kule chini Manga!

Huu ni wimbo huu ulikuwa unaimbwa wakati wa mvuno. Nia kuu ya wimbo huu Ilikuwa ni kuwakumbusha wakulima kuwa wavune mazao kwani yamekomaa na pia kuwakumbusha kuhusu changamoto za njaa ambazo walipitia awali hivyo basi walistahili kuyahifadhi mazao yao vizuri. Taswira sikivu ilidhihirika katika mshororo huu. Waimbaji walipata taswira ya kilio kinachotoka kwa mbweha. Kilio au sauti hii ya mbweha ilidhamiria kuwakumbusha kuwa mazao yao yamekomaa hivyo walipaswa kuyavuna kwani vyakula hivyo vingevamiwa na nzige wakati wowote ule.

Taswira Uoni

Kwa mujibu wa Wamitila (2018), anasema kuwa ni picha inayojengwa ambayo inalenga mtazamo wa macho. Naye Nzilu (2018), anakubaliana na maelezo haya kwa kusema kuwa hizi ni taswira ambazo hutumiwa na mwandishi ili kuchora picha inayoonekana wazi na msomaji. Taswira hii hunuia kupambanua maudhui kwa njia wazi zaidi kwa kulenga chochote kinachoonekana kwa macho. Kwa ujumla taswira hii inalenga kutupa picha ya kitu, hali au mtu akilini kupitia kwa macho yetu. Kwa mfano;

Rigesa riabeire ang'e
Endagera yaamire buya
Endagera yarabire mono
Chibando chiamire buya
Chibando chiakong'ire

Tafsiri

Mavuno yamekaribia
Chakula kimekuwa vizuri
Chakula kinang'aa kote
Mahindi yamekuwa vizuri
Mahindi yamekomaa

Wimbo huu wa jamii ya Wakisii ulitumiwa wakati ambapo kipindi cha mvuno kimekaribia. Ulinuiwa kuwakumbusha wakulima wajitayarishe kwa mavuno. Wajamii wanapata taswira ya shamba ambalo vyakula kama vile: wimbi, mahindi, na maharagwe vi tayari kuvunwa na vyakula vyenyewe vimenawiri vizuri na vilikuwa vinang'aa sana

3.1.4 Tashibihi

Wasanii na watunzi mbalimbali hutumia mbinu ya tashibihi ili kufanikisha uwasilishaji wa kazi zao za fasihi. Kulingana na Mberesia (2021), anasema kuwa tashibihi ni tamathali inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; 'kama', 'mithili ya', 'sawa' na 'ja'. Kwa mfano: *Wawili hao waliruka mithili ya chui walipomwona nyoka*. Naye Wamitila (2018), anaeleza tashibihi kuwa ni ulinganishi wa moja kwa moja. Kwa mfano: Juma ni *makali kama simba*. Anaendelea kusema kuwa ulinganishi huu unadhamiriwa kusesitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya iana fulani akilini. Ulinganishi huu unaonyeshwa kwa matumizi ya viungio: kama, mfano wa, sawa na, kama vile, mithili ya, tamthili ya na ja (katika shairi).

Ulingansiho huu hutokea baina ya vitu, hali, watu au mambo mawili ambayo hayahusiani kamwe. Wasanii au watunzi wengi wa fasihi hutumia tashibihi katika kazi zao ile kusaidia wasikilizaji, wawasilishaji na wasomaji wa kazi hizo kuelewa kile kinachozungumziwa kwa kukilinganisha na kile kitu wanachokifahamu. Kwa mfano: Tembo ni mrefu *kama twiga*. Katika sentensi hii, yule mtu ambaye hajui Tembo ni

nani na urefu wa Tembo kupitia kwa tashbihi hii atapata taswira kamili ya urefu wa Tembo. Mfano wa pili ni: Baba alinguruma *kama simba*. Katika mfano huu unapata taswira sikivu kamili wakati unapoambiwa kuwa baba alikuwa anapiga kelele. Kulingana na mifano hii ni wazi kuwa tashbihi inamsaidia mtu yeyote kuelewa kile kinachozumziwa kwa kina kwa sababu kitu hicho hulinganishwa na mazingira. Katika nyimbo za jadi za jamii hii watunzi walitumia mbinu hii ili kufanikisha uwasilishaji wao. Kwa mfano:

Rero nomogoko abaminto
Omwana oyo nigange esimba.

Tafsiri

Watu wetu leo ni siku ya furaha
Mtoto huyu ni kama simba.

Wimbo huu ulikuwa unaimbwa wakati mtoto alipozaliwa kwenye familia hasa mtoto wa jinsia ya kiume. Kulingana na jamii ya Wakisii, mtoto ni baraka. Mtoto wa jinsia ya kiume alikuwa anathaminiwa sana kwa sababu jamii iliamini kuwa mtoto huyo angeendeleza kizazi cha baba yake. Pia mtoto wa kiume aliaminika kuwa angeilinda familia yake kutokana na hatari yoyote ile. Katika wimbo huu mtoto ambaye alizaliwa alilinganishwa na simba. Sababu ya kulinganisha mtoto huyo na simba ni kuwa simba ni mnyama mwenye nguvu, jasiri na hupenda ushirikiano. Hivyo mtoto huyu wa kimue alidhamiriwa kuwa atapokomaa angechangia katika kudumisha usalama kijijini hasa katika kupigana dhidi ya maadui na pia kuchangia katika ushirikiano na utangamano kijijini.

Ng'ina amosike, ng'ina amosike eee-yoo
Tomotoma rochee, tomotoma rochee oyoo-oyoo
Obeire buna eheri, aegwe obweri bwaye

Tafsiri

Mama yake amuheshimu, mama yake amuheshimu eee-yoo
Usimtume mtoni, usimtume mtoni oyoo-oyoo
Yeye ni kama fahali, apewe zizi

Wimbo huu ni wa jandoni. Kulingana na TUKI (2019), jando ni kumbi la watoto wanaume walipotahiriwa na kufundishwa mambo ya utu uzima. Mama wa kijana alionywa kuwa asimtume mvulana huyo mtoni kwa sababu sasa amekuwa mwanaume. *Obeire buna eheri, aegwe obweri bwaye* (yeye ni kama fahali, apewe zizi). Mtoto wa kiume alilinganishwa na fahali ambaye amekomaa. Hivyo basi hakupaswa kufanya kazi ambazo zilichukuliwa kuwa za wanawake kama vile kuenda mttoni au kuteka kuni. Mvulana huyu alipaswa kupewa majukumu ya wanaume bali si ya vijana wadogo.

Toimoke tokarwane ooo
Togende na koiruruka buna chinyoni

Tafsiri

Tuende tukapigane ooo
Tuende na kupaa kama ndege

Wimbo huu uliimbwa wakati wavulana walipokuwa jandoni. Togende na *koiruruka buna chinyoni* (tuende na kupaa kama ndege). Vijana hawa walihimizwa waipigania na kuikinga jamii yao hasa kutoka kwa jamii ya Wamaasai na Wakipsigis ambao walikuwa na mazoea ya ng'ombe wao. Hivyo basi walihimizwa waende pale kuzichukua. Wavulana hao waliambiwa waende na wapae kama ndege waende kule kwa Wamaasai ili wakachukue mifugo wao.

3.1.5 Takriri

Kulingana na Mwirigi na Kamithi (2019), takriri ni mbinu ya kuradidi au kurudia sauti, neno au fungu la maneno kwa nia ya kusisitiza kinachozungumziwa. Naye

Rioba (2022), anasema ni mbinu ambayo kwayo mzungumzaji au mwandishi hurudiarudia neno lile lile au maneno yale yale ili kutulia mkazo/msisitizo zaidi juu ya jambo lisemwalo. Kulingana na wataalamu hawa takriri hutumiwa kusisitiza ujumbe, kujenga rithimu na kuonyesha umarihi wa lugha wa mtunzi.

Enchara nembe, enchara nembe
Enchara nembe, yaitire omogusii
Enchara nembe, enchara nembe

Tafsiri

Njaa ni mbaya, njaa ni mbaya
Njaa ni mbaya, imeua Mkisii
Njaa ni mbaya, njaa ni mbaya

Wimbo huu uliimbwa wakati wa mavuno. Ulinuia kuwakumbusha watu umuhimu wa kuyatunza mazao ambayo walikuwa wanakaaribia kuvuna au ambayo walikuwa wamevuna. Mbinu ya takriri ambayo ilitumiwa hapa ilionyesha jinsi ambavyo njaa ilikuwa na madhara mabaya. Njaa ilileta maafa mengi hivyo walikumbushwa wayatunze mazao yao ili wasiangamie. Takriri hii pia ilitumiwa katika kujenga rithimu kwenye wimbo huu.

Makweri! Amakweri! Amakweri!
Makweri! Amakweri! Amakweri!
Makweri! Amakweri! Amakweri!
Akoira abanto ebitongo

Makweri aeteire emerango
Mkaweri aeteire chitirisa
Makweri aeteire ebirama
Akoira abanto ebitongo

Tafsiri

Kifo! Kifo! Kifo!
Kifo! Kifo! Kifo!
Kifo! Kifo! Kifo!
Kinasababishia watu kovu!

Kifo kimepitia kwenye milango
Kifo kimepitia kwenye madirisha
Kifo kimepitia kwenye paa
Kinasababishia watu kovu!

Wimbo huu uliimbwa wakati mtu alipoaga dunia ama wakati wa makumbusho. Takriri imekithiri sana katika wimbo huu. Kwa mfano: Makweri! Makweri! Makweri! Tafsiri yake ni Kifo! Kifo! Kifo! Mama Mokeira aliema kuwa kauli hii ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo kifo kilileta machungu kwenye jamii. *Makweri aeteire emerango! Makweri aeteire chitirisa! Makweri aeteire ebirama!* Tafsiri yake ni kuwa Kifo kimepitia kwenye milango, kifo kimepitia kwenye dirisha, kifo kimepitia kwenye paa. Inaonyesha jinsi ambavyo kifo kimezidi kwani kinatokea kila wakati na kila mahali bila kumhurumia mwanadamu hivyo kumfanya mwanadamu kuishi kwa hofu kuu. Hali kadhalika, ilionyesha jinsi ambavyo kifo kilikuwa kikitokea kila mara.

Baba ng'ina Kwamboka, notana korera okure
Baba ng'ina Kwamboka, notana korera

Tafsiri

Mama Kwamboka, haina haja ya kulia amekufa
Mama Kwamboka, haina haja ya kulia

Kauli hii ilitumiwa kuwafaraji wale ambao walifiwa kwa sababu kifo kilileta dhiki nyingi kwa familia na kwa ndoa. Kando na kuwafaraji waliofiwa mishororo hii pia ilidhihirisha haja ya familia na jamii kwa jumla kuridhia kifo ambacho kilitokea kwa sababu hawana uwezo wa kukabiliana au kukizuia kifo.

Bororo mbori goita, kanga bwaitire abange
Bororo mbori goita, kanga bwaitire abange.

Tafsiri

Uchungu hauui, ungekuwa umeua wengi
Uchungu hauui, ungekuwa umeua wengi

Mishororo hii ilitumiwa kuwafariji waombolezi. Ilisisitiza umuhimu wa kutokuwa na uchungu mwingi kwa sababu huo uchungu haukuwa na athari yoyote nzuri kwa maisha yao. Ingawa baadhi ya waombolezaji walitaka kumfuata mwenda zake, jambo hilo halingewezekana hata wangelia sana kwa sababu uchungu waliokuwa nao hungeweza kuwaua hivyo basi walistahili kutulia.

Makweri na makoro
Makweri na makoro

Tafsiri

Kifo ni cha kitambo
Kifo ni cha kitambo

Mishororo hii ilitumiwa kuwakumbusha waliofikwa na mauti kuwa wao si kwanza kufiwa na hawangukuwa wa mwisho kwa sababu kifo kilikuwa tangu binadamu alipoumbwa. Hivyo basi walistahili kujipa moyo na kustahimili uchungu. Takriri pia katika wimbo huu ilitumiwa kuleta mtiririko ili kujenga rithimu kwenye wimbo huu.

3.1.6 Chuku

Kulingana na Wamitila (2018), chuku ni hali ambapo sifa fulani hukuzwa kupita kiasi. Kukuzwa huko kunaweza kuwa kwa udogo au ukubwa. Nia hasa ya kuitumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani au kumfikirisha msomaji kwa kuuona uzito uliopo.

Obeire omomura, obeire momura
Bono mambia, bono mambia
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo
Nguba boigo na nguba boigo
Arwane sigisi, arwane bosoba

Tafsiri

Amekuwa mwanamume, amekuwa mwanamume
Leo asubuhi, leo asubuhi
Anolewe mkuki, anolewe mkuki
Na mshale pia na mshale pia

Mzee Mayaka alisema kuwa wimbo huu uliimbwa baada ya wavulana kutoka kutahirishwa. Mbinu ya chuku ilidhihirika katika ubeti huu. Kwani wavulana hao baada ya kupashwa waliaminiwa kuwa ni watu wenye nguvu kupita kiasi hivyo basi wanajamii waliambiwa wawatayarishie wavulana hao silaha. Silaha ambazo wavulana hao walipaswa kutayarishiwa zilikuwa ni za kuwasaidia kwenda kupigana na jamii ya Wakipsigis pamoja na jamii ya Wamaasai kwa sababu jamii hizi zilikuwa uhasama mkubwa na jamii ya Wakisii.

Makweri aeteire emerango
Makweri aetire chiritisa
Makweri aeteire ebirama

Tafsiri

Kifo kimepitia kwenye milango
Kifo kimepitia kwenye madirisha
Kifo kimepitia kwenye paa

Wimbo huu uliimbwa baada ya kifo kutokea au wakati wa makumbusho ya mwenzake. Ubeti huu ulitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo kifo kilizidi kuongezeka kila kuchao. Watu walikufa kila siku, watu waliaga dunia kila wakati na kila mahali. Hivyo basi watu walikuwa na huzuni mwingi sana.

Ng'ai ndarusie omwana onga oyo
Ng'ai ndarusie omwana onga oyo

Tafsiri

Nitatoa mtoto mwingine kama huyu
Nitatoa mtoto mwingine kama huyu

Wimbo huu uliimbwa baada ya mzazi kufiwa na mtoto wake. Ingawa wimbo huu uliimbwa na jamii kwa jumla, ubeti huu uliimbwa na mzazi au mlezi aliyefiwa na mtoto. Kulingana na ubeti huu ni kuwa mzazi huyu ametamauka kwani aliona hawezi kupata mtoto mwingine kama huyo. Chuku katika ubeti huu ulitumiwa kuisitiza mapenzi ambayo mzazi huyu alikuwa nayo kwa mtoto wake. Chuku hii pia ilidhihirisha uchungu ambao mzazi huyu alipitia kutokana na kifo hicho.

3.1.7 Kisengere Nyuma/ Mbinu Rejeshi

Kulingana na TUKI (2019), mbinu rejeshi ni mbinu ya uandishi hasa wa kazi za kubuni ambapo kazi huanzia mwisho kurudi mwanzo. Hali kadhalika, Mwirigi na Kamithi (2019), wanasema ni mbinu ya kimuundo ambayo huhusisha hali ya kusimulia matukio yaliyotokea kabla ya wakati wa kuanza kwa hadithi. Hivyo basi kwa jumla hii ni usimulizi wa matumio yaliyotendeka awali au ya nyuma.

Enchara nembe yaitire Omogusii
Enchara nembe, enchara nembe
Baminto aaria Kisumu

Tafsiri

Njaa ni mbaya kwani iliua Mkisii
Njaa ni mbaya, njaa ni mbaya
Watu wetu pale Kisumu

Wimbo huu uliimbwa hasa wakati wa mavuno. Kutokana na mishororo hii, mbinu rejeshi ilitumiwa ili kuwakumbusha watu wa jamii ya hii kuhusu athari za njaa. Athari mojawapo ya njaa ilikuwa kifo ambacho kiliua Wakisii waliokuwa wakiishi katika eneo la Kisumu na wengine waliokuwa wakiishi katika eneo la Kisii. Waliutumia wimbo huu kuwakumbusha watu umuhimu wa kuhifadhi mazao yao vizuri na kuwaonya dhidi ya kutumia mazao yao vibaya.

Enchara nembe banto baito
Banto baito bakairwa
Abatureti bagatorwa buna ebing'wanso
Abanto baito bakagenda korwanera abasongo
Megondo kabora abaremi
Abasae bakagenda korwana
Endagera egatobora mwanyagetinge
Gaki abaminto renda rigesa

Tafsiri

Njaa ni mbaya watu wengi
Watu wetu wakachukuliwa
Wazee wakatutoa kama kafara
Watu wetub wakaenda kupigania wazungu
Shamba zikakosa wakulima
Vijana wakaenda kupigana
Chakula kikakosa Mwanyagetinge
Jamani watu wetu linda mavuno

Ubeti huu ulirejelea kipindi cha vita vya kwanza ambapo wanajamii walisalitiwa na wazee wa kijiji wakati walipoamua kuuza vijana na watu wenye nguvu kwa wazungu ili waende kupigana. Kutokana na usaliti huu kutoka kwa viongozi wao, wanajamii hao walikumbwa na janga la njaa ambalo liliangamiza watu wengi sana.

Abagusii bakare bagakwana
Bagakwana bagateba ng'a
Oyotabwati omwana no'mote omwomo
Oyobwate omwana okoboko kwaye gwaochoire

Tafsiri

Wazee wa zamani walisema
Wakasema hivi
Asiye na mtoto ni mti mkavu
Aliye na mtoto mkono wake umejaa

Ubeti huu ulitumiwa kuwakumbusha wanandoa kuhusu maswala ambayo yalidhaminiwa katika ndoa na mababu zao. Kulingana na mababu zao, ili ndoa yao idumu ni lazima wawe na watoto kwa sababu mtu asiye na watoto hawezi akaheshimiwa kamwe. Yeyote ambaye ana mtoto amebarikiwa. Yeyoye yule anayepanga kuo au kuolewa ni lazima awe na mtoto.

3.2 Mbinu za Mtindo Kwenye Nyimbo za Jadi za Jamii ya Waswahili

Mbinu mbalimbali za kimtindo zilitumiwa katika nyimbo za jadi za jamii hii ili kuziendeleza kama ifuatavyo:

3.2.1 Taswira

Kulingana na maelezo yaliyotangulia, taswira ni mbinu ambayo mwandishi hutumia maelezo yanayomfanya msomaji wa kazi ya fasihi kuchora picha fulani akilini. Kuna aina mbalimbali za taswira kama vile; taswira uoni, taswira mguso, taswira hisi, taswira mnuso, taswira mwonjo n.k.

Taswira Uoni

Hii ni taswira ambayo picha inayojengwa inalenga mtazamo wa macho. Kwa mfano;

Mume akirudi sharti
Viatu kumvua
Kitandani marashi
kumkanda kumchua

Wimbo huu ni wa ndoa. Wimbo huu uliimbwa kwa nia ya kumshauri mwanamke jinsi alivyostahili kuishi na mume wake. Bi. Hadija alisema kuwa taswira za aina mbalimbali zilitumiwa ili kufanya ujumbe wa nyimbo ueleweke vyema na walengwa. Taswira hizi zilidhihirika ifuatavyo: taswira uoni ni ya kwanza: viatu kumvua. Mshororo huu ulitumiwa kumwambia mwanamke awe tayari kumlaki mume wake akitoka kazini kwa sababu baada ya shughuli za siku kazini mwanamume huyo anastahili kupokelewa kwa mapenzi ya dhati anapoingia nyumbani. Kitandani marashi; katika mshororo huu *taswira mnuso* ilitumiwa hapa. Mshororo huu ulimkumbusha mwanamke wa Waswahili umuhimu wa kijirashia marashi kila wakati. Kwa sababu alistahili kunukia; iwe mchana au usiku. *Taswira mguso* pia ilidhihirika katika ubeti huo; kumkanda na kumchua. Mwanamke alihimizwa kumkanda mume

wake kila jioni anapotoka kazini. Kulingana na Jamii Forums (2013), mtu anapokandwa misuli hunyooka, damu husambazwa vizuri mwilini na husaidia kupunguza uchovu. Iliaminiwa kuwa baada ya siku, mwanamume alirudi nyumbani akiwa amechoka sana kwa sababu ya shughuli za kuzumbua riziki hivyo basi mwanamke huyu ambaye ameolewa ana jukumu la kumsaidia mwanamume kupitia kwa kumkanda ili kupunguza machovu aliyo nayo. Kwa jamii ya Waswahili mwanamke anatarajiwa kumhudumia mume wake kama mtoto mdogo kwa sababu mwanamume ni mtu wa thamana sana.

Mambo ya kuzima taa
Si mahaba kabisa
Bali ni kuwanga
Washa japo mshumaa
Mumeo akaone angalau shanga

Katika ubeti huu mwanamke alishauriwa kuwa akiwa chumbani na mume wake alistahili kuzima taa na kuwasha mshumaa ili wasikae kwa giza. Kukaa kwa giza kulilinganishwa na mazingaombwe. Katika hicho chumba cha malazi kulihitajika angalau mwanga hafifu. Mwanga huu pia ungempa mwanamume huyo nafasi ya kumtazama mke wake na hata kumthamini mke wake kiumbo.

Tabasamu lako mwanangu
Linanirudisha kwenye siku zangu za utotoni
Wakati kila kitu kilikuwa kinang'aa
Kiang'aa kama jua angani
Nilipoutazama uso wako mwanangu
Wanirejesha kwenye enzi zetu za zama
Ila nikiendelea kukutazama kwa muda, mito ya machozi
inanitiririka

Kupitia kwa ubeti huu, mama anatazama uso wa mtoto wake, anapomtazama anafurahia kumwona mtoto wake kwa sababu uso wa mtoto wake umejaa tabasamu. Kutokana na tabasamu la mtoto huyo wake anazikumbuka enzi zake za kale

alipokuwa mtoto mchanga ambapo hakupitia changamoto zozote maishani.
Aliyafurahia maisha yake ya utotoni.

Mwezi unachomoza polepole
Mwanga wake wang'aa kule mtini
Mwanangu jitayarishe uingie baharini

Ubeti huu ulitumiwa kuonyesha wakati ambao shughuli za uvuvi zilifanyika. Uvuvi uliendelezwa usiku kwani wanasema *mwezi unachomoza polepole*. Mandhari ya usiku ndiyo mwafaka ya kuendeleza uvivu.

Taswira Hisi

Kama tulivyoeleza awali, hii ni taswira inayohusika na hisi za ndani. Taswira hii huweza kumfanya msomaji au msikilizaji awe na wasiwasi, aone woga, apandwe na hasira au ahisi kinyaa. Taswira hii huwa na nguvu kubwa ya kuganda akilini. Taswira hii ilitumiwa kwenye nyimbo mbalimbali kwa mfano;

Ah! Leo furaha chereko
Mwanenu nimekomaa
Zile kuringa na umbea vitapunga

Wimbo huu wa sherehe ya ndoa ulidhihirisha hisia za furaha. Katika jamii, si kila mtu aliyefanikiwa kuingia katika ndoa na kuna wale ambao walibahatika kuingia katika ndoa ila ndoa zao hazikufanikiwa. Hivyo basi wanandoa walifurahia siku hiyo ambayo walikuwa wakiisubiri sana. Kutokana na furaha isiyo ya kifani pia wanaleta dhana ya kuringa. Katika furaha hiyo, pia walimwomba Mungu ili ndoa yao idumu milele.

Shangwe vigelegele na nderemo zasikika kote
Bwana na bibi harusi wamefunga pingu za masiha

Wanajamii walidhihirisha hisia za furaha kutokana na wanandoa kufunga pingu za maisha. Kutokana na heshima ambayo taasisi ya ndoa ilipewa, wanajamii walipewa nafasi ya kushiriki katika sherehe hiyo ambapo walikula aina mbalimbali za vyakula

za kitamduni kama vile: pilau, biriani, samaki, mvinyo na kadhalika. Aidha, walicheza nyimbo za taarabu ili kuwasherekea. Sherehe hizi zilichukua siku kadhaa.

Kifo kinaleta huzuni, eee huzuni!
Kifo kinaleta majonzi, eee majonzi!
Hatujui tujifiche wapi, tujifiche wapi?

Ubeti huu ulidhihirisha hisia za huzuni kutokana na kifo ambacho kilitokea. Huzuni huo ulitokana na mapenzi ya dhati ambayo walikuwa nayo kwa mwendazake. Mbali na hayo, kifo hicho kiliwaletea majonzi. Watu hawa hawakuwa na furaha yoyote kwa sababu hawangemwona mpendwa wao milele.

Wanasema siku njema huonekana asubuhi
Ni kweli mtoto wangu
Kijana wangu mtanashati
Ingawa bado nina zingizi la uzazi
Zingizi hilo lafanya nitabasamu bila kikomo.

MamaBangweso alieleza kuwa mama ya mtoto alidhihirisha furaha kwa sababu alijifungua salama. Huyu mtoto wake alimletea raha maishani. Kwani jamii ingemheshimu kwa sababu familia hiyo ilikuwa na mtu wa kuendeleza kizazi chao. Kando na hayo, mama huyo alidhihirisha uvumilivu kwa sababu alikuwa anapitia uchungu kupitia kwa zingizi la uzazi. Ingawa kutokana na furaha ya kujifungua salama salmini mama huyo alionyesha furaha.

Shangwe, vigelele na nderemo
Zasikika kote kote

Wimbo huu uliimbwa wakati wa harusi, ulitumiwa kuashiria furaha ambayo wanajamii wanaliokuwa nayo kwa sababu ya ndoa iliyounganishwa. Taswiria sikivu ndiyo ilidhihirika katika mishoro hii. Wanajamii wanashangalia, wakipiga vigelele pia wana nderemo kutokana na harusi ambayo wamehudhuria. Mbali na taswira sikivu, taswira hii ilidhihirika hapa kwa sababu wanajamii wana furaha kwa sababu ya ndoa ambayo imeunganishwa.

3.2.2 Tashihisi

Kulingana na Wamitila (2003), anaeleza tashihishi kama hali ya kukipa kitu kisicho hai sifa za kiumbe aliyehai. Katika nyimbo za Waswahili, mbinu ya tashihisi imetumiwa katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo hizo.

Kifo cha vama boma zetu
Kinawachukua wazazi wetu
Kinatuacha mayatima
Je, tutawezana vipi na kifo?

Wimbo huu uliimbwa wakati kifo kimetokea ama wakati wa sherehe za mazishi. Mzee Hamisi alisema kuwa watoto waliofiwa na wazazi wao ndio walioimba huu. Watoto hawa walilalamikia kuhusu madhara ya kifo ambacho kiliwaacha mayatima. Kauli ‘Kifo cha vama boma zetu’ kifo kilipewa uwezo wa kuvamia boma. Kule kuvamia watu kwenye boma hilo ni hali ya watu wengi kuaga dunia. Kauli ‘Kinawachukua wazazi wetu’ kifo kilipewa uwezo wa kuchukua watu, hivyo ilikuwa na maana kina mikono ya kubeba na kuwachukua kutoka kwa boma zao. Kule kuaga kwa watu ndiko kunaleta dhana kuwa watu walichukuliwa. Kwa sababu baada ya watu kuaga dunia na kuzikwa hawakuwa na nafasi tena ya kurudi ulimwenguni.

Ooh kifo! Mbona watutesa hivi,
Ooh kifo! Ni lini utatuachia,
Ooh kifo! Hata tujifiche wee!
Ooh kifo! Unatusanya kotekote.

Katika ubeti huu, mtunzi alitumia mbinu ya tashihisi ili kuonyesha madhara yaliyotokana na watu kufikwa na kifo. Kwanza, kifo kilipewa uwezo wa kusababisha mateso kwa waathiriwa. Kilisababisha uchungu usio na kifani, kiliwapitishia maumivu na taabu kwa watu hao hawangekuwa na nafasi ya kuonana na mwezao

tena. Kifo pia kilipewa uwezo wa kutafuta watu kila mahali. Katika ubeti huu ni kuwa hata watu wakijaribu kujificha kifo kiliwatafuta na kuwapata.

Mwezi umepoteza razini yake?
Nahisi kwamba unanichukia

Mishororo hii ni katika wimbo wa *Kwaheri*. Mishororo hii ilitumia tashihisi kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake. Kwanza ni kuwa mwezi ulipewa uwezo wa kufikiria vizuri. Kufikiria ni sifa ya binadamu kwa sababu binadamu ndiye ana akili. Katika mshororo huu ni kuwa mwezi ulipoteza uwezo wake wa kufikiria vizuri kwa sababu ya kifo ambacho kimetokea. Katika mshororo unaofuata mwezi ulipewa uwezo wa kuwa na hisia. Kutokana na kifo ambacho kilitokea, waathiriwa walihisi kuwa mwezi ulipoteza mapenzi kwao au ulikasirishwa na wao na ndio sababu walipatwa na maafa. Hali hii yote ilidhihirisha uchungu unaosababishwa na kifo.

Kuwa tayari kukutana na kisu cha ngariba
Kisu cha ngariba ukidhihaki

Kisu cha ngariba ni kisu cha mtu alikuwa na jukumu la kuwapasha wavulana tohara au aliyetahirisha wavulana. Katika wimbo huu, wavulana ambao walipelekwa jandoni waliambiwa ili kuwatayarisha kihisia kuhusu uchungu wangepitia pale jandoni. Kisu cha ngariba kilipewa uwezo wa kutisha na kusababisha maumivu mengi kwa wavulana hao na ndio sababu waliambiwa wawe tayari kukutana na kisu hicho. Katika mshororo unaofuata, wavulana waliambiwa wakidhihaki kisu hicho. Mzee Abdi alisema wavulana hao waliambiwa wakifanyie kisu hicho kejeli au wakifanyie mzaha. Binadamu aliweza kumkejeli binadamu mwenzake lakini hawangeweza kukejeli kitu kisichokuwa na uhai. Kimsingi wavulana hao walihimizwa kuwa wasionyeshe woga wowote watakapopitia mchakato wote wa tohara. Kule kuonyesha

ujasiri kungedhihirishia wanajamii kuwa wavulana hao si watoto tena bali ni wanaume ambao walikuwa tayari kuihudumia jamii yao kwa hali yoyote ile.

3.2.3 Jazanda

Jazanda ni tamathali ya usemi inayotumiwa kumaanisha ulinganishi wa moja kwa moja bila kutumia vihusishi vilinganishi mathalani kama, ja, mfano, sawa na, kama vile, mithili, tamthili na kadhalika. Ulinganishi unaotumiwa katika jazanda au sitiri hulenga kuzua maana fiche/maana ya ndani.

Baba akasema kuomba chumvi ni mwiko
Raha ya chumvi ni kununua

Wimbo huu uliimbwa wakati wa sherehe za ndoa. Waliooana walipoambiwa kuomba chumvi ni mwiko, kimsingi waliambiwa kuwa hawapaswi kuwa ombaomba. Kuomba majirani vitu kama vile vyakula ni aibu kubwa sana na ingefanya wakose kuheshimiwa na wanajamii. Hali kadhalika, waliambiwa kuwa ili wafurahie maisha yao bila kuogopa kusemwasemwa na watu ilikuwa ni lazima wangewajibikia, wajitume ili waweze kukimu mahitaji yao ya kibinafsi bila kutegemea mtu yeyote.

Kisha anza sayansi kiuno kutengua

Bi. Mwanaisha alisema kuwa mshororo huu ulielekezewa mwanamke katika sherehe za ndoa au za kulipa mahari. Mwanamke alikumbushwa kuwa akiingia kwenye chumba cha malazi lazima angefanya juu chini ili kumshawishi mume wake. Jambo la kwanza alilostahili kufanya, ni kutumia miondoko na ishara za mwili ambazo zingemfanya mume afurahie. Wanawake wazee na wenye tajriba ya maisha ya ndoa walimfunza miondoko mbalimbali ambayo msichana huyu angetumia pale chumbani kwa ajili ya mume wake. Waliamini kuwa miondoko hiyo haikupaswa kuonwa na mtu yeyote yule isipokuwa mume wake tu.

Huu ni usingizi wa milele

Katika mshororo huu kifo kilirejelewa kama usingizi ila si usingizi wa kawaida kwa sababu katika usingizi wa kawaida mtu alitarajiwa kuamka. Katika usingizi wa milele au kifo mtu huyo hakutarajiwa kuamka tena. Wapendwa wake hawakuwa na nafasi tena ya kumuona au kuongea na yeye.

Kiza chaingia, kinazidi siwezi ona
Maisha haya hayana maana

Katika mishororo hii athari ya kifo ilidhihirika. Kiza ni hali ya kukosa mwangaza. Mzee Salim alisema kuwa mpendwa wao kuondoka duniani kulilinganishwa sawa kiza. Kifo cha mpendwa wao kimerejelewa kama kiza kwa sababu sasa maisha yao hayana raha, mtu yule waliyezoea kuona kila siku hayuko tena miongoni mwao tena maisha yao yamejaa huzuni tele. Hawakuwa wanaona chochote wala lolote kuwa na maana au umuhimu maishani mwao. Kwa mfano ikiwa ni watoto ambao waliwapoteza wazazi wao, maisha yao yalifananishwa na giza kwa sababu hawatakuwa na mtu na kuwalea au kuwatimizia mahitaji yao ya kimsingi. Kwa upande mwingine wazazi walipompoteza mtoto, wao maisha yao yalikosa mwanga kwa sababu hawangekuwa na mtu wa kuendeleza kizazi chao.

Mwanangu usiyapapie maisha
Tulikupa asali na shubiri

Wimbo huu uliimbwa baada ya watoto kuzaliwa. Kulingana na TUKI (2019), shubiri ni utomvu mchungu unaotokana na mshubiri ambao hutumiwa kama dawa ya tumbo na asali nini maji matamu mazito ambayo hutengenezwa na nyuki. Kwanza, mtoto alirambishwa shubiri, kimsingi shubiri huwa ni chungu sana ingawa ni dawa ya tumbo. Mtoto aliporambishwa shubiri alilia sana kwa sababu ya uchungu huo. Hiyo shubiri ilitumiwa kumfunza mtoto kuwa maishani kuna wakati ambapo angekumbana

na changamoto au shida nyingi sana kama vile: umaskini, magonjwa na vifo ambazo zingemfanya alie na kumletea huzuni maishani. Ila kutokana na changamoto hizo, alitarajiwa kujifunza mengi hasa kuwa mvumilivu maishani. Baada ya kupewa shubiri, mtoto huyo alipewa asali. Asali huwa tamu sana. Mtoto huyo alipopewa asali aliacha kulia na kuanza kutabasamu kwa sababu uchungu wa shubiri ungeyeyushwa na asali. Asali ilinuiwa kumkumbusha mtoto huyo kuwa kungekuwa na siku za furaha na mafanikio. Siku hizo zingekapofika alitarajiwa azifurahie.

Njiwa mwerevu hujenga
Hujenga kiota chake vizuri
Ili mvua inaponyesha anajikinga

Katika wimbo huu wa kazi Mzee Kombo alisema kuwa watu walikumbushwa umuhimu wa kufanya kazi na kuhifadhi au kuwekeza vizuri kwa siku zijazo. Kule kujenga kiota na kujikinga mvua inaponyesha ilikuwa na maana kuwa kuweka vizuri mali au mazao waliyochuma ili yawafae kwa siku ambazo zingekuja. Ulimwenguni kuna aina mbili za watu, kuna watu ambao ni wapevu na pili kuna watu ambao si wapevu. Watu wapevu hufanya kazi kwa bidii na pia hujitayarishwa kwa siku zijazo. Kwa mfano, baada ya kuvuna mazao yao watayahifadhi vizuri kwa siku zijazo hivyo basi hawawezi kukumbwa na njaa. Ikiwa walikuwa na pesa wangezitemia na kuziwekeza ili waweze kupata pesa zaidi hivyo kuishi vizuri baadye. Kwa upande mwingine, watu ambao walichukuliwa kuwa si wapevu ni wale ambao hawapendi kufanya kazi na ikiwa wangefanya kazi, chochote wangepata wangetumia kwa wakati huo na kumaliza bila kujali siku zijazo. Baada ya miezi au miaka kadhaa watu hao wangeteseka kwa sababu hawa pa kushikilia au pa kukimbilia.

Sasa ndo wamefika, simba kutoka mwituni
Wao si watoto tena, bali wamekuwa simba

Wimbo huu wa jandoni ulimrejelea mvulana aliyepashwa tohara kama simba. Kimsingi simba ni mnyama hatari sana. Porini, simba hurejelewa kama mfalme wa pori. Baada ya mvulana kupashwa toraha mabadiliko mengi yalitokea. Kwanza, mvulana huyo alitoka utotoni na kuingia utu uzima. Mvulana huyo hakustahili kufanya mambo ya kitoto tena. Mvulana huyo alitarajiwa kufanya kazi kama vile uvuvi. Pili, mvulana huyo alitarajiwa kudumisha ulinzi wa familia yake jambo ambalo lilimhitaji mvulana huyo kuwa jasiri na mkali kama vile simba kwa yeyote ambaye angepanga kuivamia familia yake. Tatu, mvulana huyo alitarajiwa kujitegemea kwa sababu sasa alikuwa amekomaa.

Kijana kuingia jandoni si lelemama
Leo hii tutajua tofauti kati ya jogoo
Naam jogoo na kifaranga
Mekuwa mwanamume, mekuwa dume
Ukoo wetu si wa kunguru

Katika ubeti huu, wavulana walitayarishwa kihisia na kuhusu hali ambayo wangekumbana nayo pale jandoni. Walipoambiwa *jandoni si lelemama* yaani ina maana kuwa hali wangekumbana nayo pale haingekuwa rahisi. Kulingana na TUKI (2019), lelemama ni ngoma ya wanawake inayochezwa juu ya mabao na kwa kutumia mbiu. Waliambiwa kuwa haingekuwa rahisi kama lelemama hivyo basi lazima wangevumilia uchungu ambao ulikuwa unawasubiri. Hali kadhalika, waliambiwa kuwa pale jandoni tofauti ya jogoo na kifaranga ingedhihirika. Jogoo ni kuku dume ilhali kifaranga ni mtoto wa kuku. Kijana ambaye angekuwa jasiri katika kukabiliana na kisu cha ngariba na asionyeshe hisia zozote za uchungu, yeye ndiye angerejelewa kama jogoo kwa kuwa ujasiri wake ungedhihirisha kuwa amekomaa. Ukomavu wake ungekuwa ishara ya mvulana huyo kuwa tayari kujitwika majukumu magumu zaidi kwenye jamii bila kuonyesha udhaifu. Kwa upande mwingie, mvulana au wavulana ambao wangedhihirisha woga na hata kulia kwa sababu ya uchungu waliopitia pale

jandoni wavulana hao ndio watarejelewa kama vifaranga. Kule kuonyesha hisia za woga ni wazi kuwa bado hawakuwa wamekomaa na wana udhaifu hivyo basi walihitaji kukaa na wazazi wao zaidi ili wawaelekeze. Kila kijana alijitahidi kukabiliana na uchungu huo ili asiitwe kifaranga kwa sababu kurejelwa kama kifaranga ni jambo la aibu na hata lingepelekea wanarika kumkosea heshima. Mwisho waliposema kuwa “*ukoo wetu si wa kunguru*”, ina maana kuwa ukoo wao si watu waoga. Wanajamii walielewa fika kuwa mchakato wote ulihusisha uchungu mwingi sana, lakini waliwatia moyo na kuwakumbusha kuwa walitoka kwa ukoo ambao ni wa mashujaa. Ili mtu awe shujaa hapaswi kutishwa na chochote kile. Kwa jumla vijana walikumbushwa kuwa lazima wawe jasiri na si kwa sababu yao tu bali kwa sababu ya ukoo wao.

3.2.4 Kisengere Nyuma/Mbinu Rejeshi

Kulingana na Mwirigi na Kamithi (2019), kisengere nyuma huhusisha hali ya kusimulia matukio yaliyotokea kabla ya wakati wa kuanza kwa utungo wa fasihi. Ni usimulizi wa matukio yaliyotendeka awali au ya nyuma. Mbinu hii imetumika katika tungo mbalimbali. Kwa mfano:

Ahsante mama, ulinifunza nikajua
Baba akasema, kuomba ni mwiko
Raha ya chumvi, ni kununua

Mbinu hii ilidhihirika katika wimbo huo. Wanandoa walikumbushwa kuhusu mafunzo waliyoyapokea kuhusu maisha ya ndoa kabla ya siku yenyewe. Wanaume walifunzwa na wazee wenye heshima kwenye jamii na baba mzazi akiwepo kuhusu umuhimu wa kufanya kazi na kukidhi mahitaji ya familia bila kuombaomba majirani. Naye mwanamke alipokuwa akisingwa na wanawake wenye maarifa kuhusu masuala ya ndoa alikumbushwa kumsaidia mume wake katika shughuli za kila siku ili

wasiwategemee watu wengine. Mtu yeyote aliyejitegemea aliheshimiwa na wana jamii na hata kufurahia maisha yake kwa sababu hakuwa na deni la mtu na alihitaji kuomba radhi kutoka kwa mtu yeyote ili kufurahia. Kwa mfano:

Tabasamu lako mwanangu
Lanirudisha kwenye siku zangu za utotoni
Wakati kila kitu kilikuwa kinang'aa
Kinang'aa kama jua angani
Ninapoutazama uso wako mwanangu
Wanirejesha kwenye enzi zetu za zama

Wimbo huu uliimbiwa katika sherehe za kuzaliwa kwa watoto. Mbinu hii ilitumika kuonyesha kuwa mzazi au watu ambao walikomaa kwenye jamii mara nyingi walitamani siku zao za utotoni. Kulingana na wao siku za utotoni zilikuwa nzuri, zilikuwa zenye furaha na kila kitu kilikuwa kikienda vizuri ndio sababu walizikumbuka na kuzitamani. Ukilinganisha maisha ya utotoni na utu uzima, maisha haya ni tofauti sana kwa njia nyingi kama vile: mtoto hafanyi kazi ili kukidhi mahitaji yake ila mtu mzima lazima afanye kazi, mtoto hana malezi kwa upande mwingine mzazi lazima awajaibikie malezi n.k. Kwa hivyo mtoto huyo alipotabasamu mzazi au mtu yeyote mzima alikumbuka siku zake za usoni ambazo zilijaa furaha na bila kuwazia jinsi ya kukidhi mahitaji yake ya kibinafsi au mahitaji ya familia.

Mwanangu usiyapapie maisha
Tulikupa asali na shubiri

Katika mishororo hii mbinu hii ilitumiwa kuonyesha miviga ambayo mtoto alifanyiwa punde tu alipozaliwa. Katika jamii hii ya Waswahili baada ya mtoto kuzaliwa, alipokea funzo lake la kwanza kuhusu maisha yaliyomsubiri siku ambazo zilikuwa usoni. Mtoto huyo alipewa shubiri ambayo ni kali sana, kutokana na ladha ya shubiri mtoto alilia sana kwa sababu hajawahi kuonja kitu kichungu hivyo. Shubiri hii ilikusudiwa kumfunza mtoto huyo kuwa kuna wakati angekumbana na shida nyingi

sana ambazo zingemletea huzuni maishani. Baada ya hapo, mtoto huyo alipewa asali ambayo kimsingi ni tamu. Kutokana na ladha tamu ya sukari, kilio cha mtoto huyo kilikomaa. Ishara ya kuwa kungekuwa na siku ambazo maisha yangukuwa mazuri na yakiwa mazuri alistahili kuyafurahia.

3.2.5 Takriri

Kulingana na Wamitila (2018), anasema kuwa takriri ni mbinu ya kuradidi au kurudia sauti, neno au fungu la maneno kwa nia ya kusisitiza kinachozungumziwa. Kwa mfano:

Shangwe vigelegele na nderemo zakika kote
Shangwe vigelegele na nderemo zakika kote

Katika wimbo huu kuna urudiaji wa mshororo. Urudiaji huu ulitumiwa kuonyesha hisia za furaha ambazo zilitanda kwenye eneo ambalo sherehe hiyo iliandaliwa. Kwa mfano, kama ni kijijini watu wote kwenye kijiji cha mwanamume na mwanamke walishangilia kwa vifijo na nderemo kwa sababu ya hatua hiyo muhimu ambayo ilichukuliwa na maharusi.

Sisi sote tumekuwa mashahidi kwenu mkitoa ahadi
Sisi sote tumekuwa mashahidi kwenu mkitoa ahadi

Mshororo hii inaweka wazi kuwa sherehe ya ndoa au ya harusi si sherehe ambazo hazikufanyika kwa siri. Ni wazi kuwa familia na wanajamii kwa jumla walishuhudia wawili hawa wakitoa ahadi za ndoa. Iwapo chochote kingetokea kati ya watu hao wawili wanajamii wangetoa ushahidi wa yale ambayo walishuhudia siku hiyo.

Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kitawatenga
Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kitawatenga

Mshororo huu uliwakumbusha wanandoa kuwa hawakupaswa kufirikia kuhusu talaka. Iwapo jambo lolote lingetokea na litishie ndoa yao walistahili kutmia mbinu zozote

zile ili kulisuluhisha mgogoro huo. Iwapo wangekumbana na shida zozote kama vile magonjwa na umaskini wawili hawa walistahili kuvumiliana.

Mapenzi yawe daima yasiingiliwe na mtu
Mapenzi yawe daima yasiingiliwe na mtu

Ni wazi kuwa, kwenye jamii hapakosi mahasidi ambao watafanya juu chini ili kuisambaratisha ndoa au familia. Takriri kwenye mishororo hii ilitumiwa kuwaambia wawili hao kuwa wasiwaruhusu watu hao kuingilia ndoa yao. Walipaswa kutafuta ushauri na usaidizi kutoka kwa watu ambao waliwatakia mema.

Leo mnaanza masiha nendeni mkaishi salama
Leo mnaanza masiha nendeni mkaishi salama
Tunawatakia mema na kuwaombea baraka za Allah
Tunawatakia mema na kuwaombea baraka za Allah

Takriri katika mishororo hii inadhahirisha jinsi ambavyo jamii hii inaheshimu ndoa. Mbali na wao kushuhudia wawili hao wakiungansihwa, wanajamii wanaombea kila la heri. Pia inadhahirishajinsi ambavyo wanajamii wanaamini kuwa ili ndoa yoyote ifanikiwe dini ni kiungo muhimu sana kwani wanawatakia baraka za *Allah* katika safari yao mpya.

Njiwa mwerevu hujenga
Hujenga kiota chake kizuri
Ili mvua inaponyesha anajikinga
Njiwa mwerevu hujenga
Hujenga kiota chake kizuri
Ili mvua inaponyesha anajikinga

Kwenye mishororo hii mbinu hii ilitumiwa kuwakumbusha watu kuwa walistahili kutia bidii maishani. Kando na kutia bidii walistahili kuwa werevu kuhusiana na jinsi ambavyo walivyotumia mali walizochuma kwa sababu walistahili kuwekeza vizuri ili mambo yakienda mrama siku za usoni (*ili mvua inaponyesha, anajikinga*) upate wana uwezo wa kukidhi mahitaji yao.

O mwanadamu uliyekamili
O mwandamu uliyekamili
Fanya kazi yako
Fanya kazi yako

Wanajamii walikumbushwa umuhimu wa kufanya kazi kupitia kwa takriri kwenye mishororo. Mzee Mkombozi alisema kuwa baadhi ya watu kwenye jamii walikuwa wavivu, walipenda kukaa lakini mwisho wa siku walitarjia walishwe na wale waliofanya kazi. Wimbo huu wa kazi ulimkumbusha kila mwandamu aliyetimamu na mwenye afya nzuri alistahili kufanya kazi. Ulionya watu dhidi ya kuwa wategemezi na pia dhidi ya kubadhiri mali walizochuma.

Sasa ndo wamefika, simba kutoka mwituni
Sasa ndo wamefika, simba kutoka mwituni

Wimbo huu wa jandoni ulitumiwa kuonyesha mabadiliko ambayo wavulana walipelekwa jandoni walipitia. Walipotoka nyumbani walikuwa ni watoto lakini baada ya kuenda jandoni na kukaa mwituni kwa wiki kadhaa, wavulana hao walikomaa na woga kupotea. Wavulana walikuwa tayari kujitwika majukumu yao mapya ikiwemo kulinda jamii yao dhidi ya uvamizi wa maadui wao.

Ukoo wetu ni wa majagina
Ukoo wetu si wa kunguru

Usambamba ulitumiwa kuwakumbusha wavulana walioenda jandoni kuwa chochote wangepanya kingewakilisha ukoo wao. Waliambiwa kuwa ukoo wao ni wa majagina, yaani watu ambao walitenda matendo ya kishujaa. Kwa mfano kuna majagina maarufu sana kwenye jamii kama vile: Fumo Liyongo wa jamii ya Wapate, Luanda Magere wa jamii ya Waluo, Wangu wa Makeri wa jamii ya Wakikuyu na hata kwenye Biblia tuna Samsoni. Kimsingi, vijana hawa wanakumbushwa kuwa jasiri na wasiwe waoga kamwe.

3.2.6 Chuku

Wanasema kuwa chuku ni tamathali ya usemi inayoelezea hali ya sifa ya kitu kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida. Mbinu hii ya kimtindo ina maana kuwa kukuzwa huku kwa jambo fulani huweza kuwa kwa ukubwa au kwa udogo. Kwa mfano;

Shangwe vigelegele na nderemo zasikika kote

Chuku kwenye mshororo huu ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo sherehe hii ya ndoa ni kubwa sana. Ilihusisha watu wengi sana hasa kijiografia na pia watu hao waliifurahia na ndio sababu vigelegele na nderemo zilisikika kila mahali.

Maisha haya hayana maana
Nataka nibishe milango ya mbinguni

Katika wimbo huu kauli “*maisha haya hayana maana*” ni ishara ya kuwa aliyefiwa hakutaka kuishi tena kwani yule ambaye alimfanya kuonea fahari maisha yake aliaga dunia kwa hivyo haoni haja ya kuishi. Kando na hilo kauli hii pia ilidhihirisha mapenzi ya dhati ambayo yalikuwa baina ya watu hawa wawili na ndio sababu alikuwa na uchungu mwingi sana. Alikosa kuonea fahari maisha yake.

Lanirudisha kwenye siku zangu zile za utotoni
Wakati kila kitu kilikuwa kinang’aa

Mtunzi alionyesha jinsi ambavyo siku za utotoni zilikuwa na mambo mengi mazuri ya kufurahia kila wakati ukilinganisha na siku za utu uzima. Mtoto mdogo hakuwa anawazia jambo lolote, hakuwa na jukumu lolote wala hakuwa na shinikizo la kufanya kazi ili kikimu mahitaji yake ya kila siku. Kwa sababu ya mambo haya, siku za utotoni zilijaa furaha ambayo watu wazima walikuwa wanazitamani hasa walipokumbwa na hali ngumu maishani.

Sasa ndo wamefika, simba kutoka mbituni

Wavulana ambao walitoka jandoni walirejelewa kama ‘*simba*’ walitumia mbinu ya chuku kuonyesha kuwa wavulana ambao walienda jandoni walirudi wakiwa wanaume jasiri na wenye nguvu. Wanaume ambao walistahili kuheshimiwa na kuogopwa na kila mtu kwani wao si watoto tena. Wanaume hawa walikuwa tayari kukabiliana na jambo au hali yoyote ile hata ingawa ilikuwa ngumu au ilikuwa ya kutisha kutisha sana.

Kuwa tayari kukutana na kisu cha ngariba

Kilicho na makali kuwili

Mbinu ya chuku ilitumiwa kumtahadharisha mvulana aliyeenda kupashwa tohara kuhusu uchungu angepitia pale jandoni. Kauli hii ilikuwa muhimu sana kwa vijana hao kwa sababu walitarajiwa kuonyesha ujasiri wa hali ya juu, hivyo basi chuku ilitumiwa kuwatayarisha kisaikolojia kuwa mambo ambayo wangekumbana nayo hapo mbele hayatakuwa rahisi. Hali hii ilidhihirika pia pale mwanzoni wimbo unapoanza kwa mshororo ufuatao ‘kijana kuingia jandoni si lelemama’.

3.2.7 Tashbihi/Tashbiha

Tashbihi ni tamathali ya usemi inayotumiwa kulinganisha kitu kimoja na kingine kwa kumtumia vihusishi vilinganishi mathalan kama, mfano wa, ja, mithili ya, tamthili ya, kama vile, sawa na na kadhalika. Mbinu hii ilitumiwa kwa nyimbo mbalimbali kama vile;

Kifo ni adui mkubwa wa binadamu
Kinakuja kama mwizi

Kulingana na TUKI (2019), mwizi ni mtu mwenye tabia ya kuchukua kisicho chake bila ya ruhusa au bila mwenyewe kumwona. Mwizi anapoanza kupanga jinsi ya kuiba na mwishowe kutekeleza kitendo cha wizi, huwa hamfahamishi yule anayeenda kumwibia. Kifo katika wimbo huu kililinganishwa na mwizi kwa sababu hakuna mtu

yeyote aliyefahamu kitatokea wakati upi. Kifo kilimvamia mtu yeyote wakati wowote awe mtoto, kijana, mtu wa makamo au mzee. Kutokana na hali hii, kilisababisha uchungu mwingi kwa jamaa na marafiki wa aliyeaga.

Wakati kila kitu kilikuwa kinang'aa
Kinang'aa kama jua angani

Kwenye wimbo huu, mzazi au wazee walikumbuka siku zao za utotoni kupitia kwa tabasamu la mtoto aliyezaliwa. Kulingana na wao ni kuwa siku zao za utotoni zilikuwa siku zenye mambo mengi mazuri na walizifurahia sana kama vile; kucheza, kukula, kulala na kadhalika ukilinganisha na maisha yao ya sasa ambapo wana majukumu mengi ambayo yaliwanyima tabasamu.

Nakuombea umpate mwanmke
Mwanamke atakayekuenzi
Kama mboni la jicho lake

Wakati jamii hii ya Waswahili waliposherehekea kuzaliwa kwa mtoto, Bi. Saida alisema kuwa walitumia fursa hiyo kuanza kumwelekeza kuhusu maisha ambayo angekumbana nayo akiwa mtu mzima. Mafunzo hayo yalitolewa kwa njia za nyimbo. Kando na mafunzo hayo, walitumia nafasi hiyo kumwomba mtoto huyo na kumwepusha na mabaya yote. Katika wimbo huu ambao uliimbiwa watoto wa kiume, wanajamii walitarajia kuwa mvulana huyo akikomaa ni lazima angeoa. Walimwomba mvulana huyo apate mke ambaye angempenda kwa roho yake yote na ambaye angemheshimu kama mboni la jicho lake. Ili mtu aweze kuona lazima atumie mboni ya jicho, kwa hivyo mboni ni kiungo muhimu sana katika sehemu ya macho yetu. Alistahili kutuzwa kwa hali ya juu. Wanajamii hawa walimwomba mvulana huyo ampate mke ambaye angemthamini kuliko chochote kile, mke ambaye hangeweza kufikiria kuenda kinyume na yeye.

Fanya kazi yako
Kama mchwa ajengaye kichuguu

Kulingana na Ngugi (2017), anasema kuwa mchwa ni mmojawapo ya wanyama ambao ni wadogo sana lakini ana sifa kedekede kutokana na kazi yake. Japo mchwa hafanyi kazi pekee yake, bidii yao wakiwa kwenye vikundi ndio funzo kwetu. Anaendelea kusema kuwa hakuna chochote ambacho utaweza kufikia maishani bila bidii. Mungu aliumba dunia kwa bidii, hivyo yeye pia anatazamia kuwa tuwe wenye bidii.

Wimbo huu wa kazi uliwakumbusha watu wafanye kazi kwa bidii kwa kuwa unapokuwa na bidii maishani utafanikiwa. Kando na hayo, tashbihi hii ilitumiwa kuwahimiza watu kufanya kazi kwa ushirikiano kwa sababu ukiwa peke yako hungeweza kufanikiwa sana kwani Waswahili husema ‘umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu au kidole kimoja hakivunji chawa’. Mbali na hayo watu walikumbushwa kuwa na msukumo wa kibinafsi katika kuyatekeleza majukumu yao ya kila siku kwa sababu mchwa hana kiongozi, anatekeleza wajibu wake kwa sababu ana uwajibikaji.

3.2.8 Kinaya

Kwa mujibu wa Wamitila (2018), anaeleza kinaya kama tamathali ambapo usemi fulani unaotumiwa una maana ya kinyume. Maana ya juu siyo inayokusudiwa. Msingi wa matumzi ya kinaya ni kucheka au kuonyesha kinyume kwa njia isiyokuwa wazi. Kulingana na Mbatiah (2008), anasema kuwa kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya insi ambavyo mambo yanaonekana na jinsi yalivyo sasa. Kwa ujumla kinaya ni tamathali ya usemi inayotumiwa kuelezea kauli ambayo ni kinyume na anachomaanisha. Kinaya pia huweza kuelezwa kama hali ya mtu kutenda kinyume na matarajio ya jamii. Kwa mfano;

Ni kweli mtoto wangu
Kijana wangu mtanashati
Inagawa bado nina zingizi la uzazi
Zingizi hili lafanya nitabasamu nikwonapo

Kauli hii ni kinyume na matarajio kwa sababu maumivu ambayo mwanamke hupitia baada ya kujifungua huwa mengi sana hivyo basi hatarajiwi kutabasamu. Mama huyu alitabasamu alipomwagalia mvulana wake mtanashati alitabasamu kwani mtoto huyo wake akamfanya asahau ana zingizi la uzazi.

Ingawa uchungu ni mwingi sana
Huna nafasi ya kumwaga tone la chozi

Mtu alipodungwa na sindano au kukatwa huwa nahisi kulia sembuse kukatwa kwa kisu cha ngariba chenye makali kuwili? Ilikuwa kuna kuwa kinaya wavulana walioenda kupashwa tohara kuonywa dhidi ya kumwaga hata tone la chozi wakati ambapo wangekabiliana na kisu cha ngariba. Kutokana na wimbo wenyewe, kisu hicho ni wazi ni kikali sana ila walitahadharishwa. Kwa mwili wa mwanadamu kijana huyo alitarajiwa ahisi uchungu, aonyeshe kuwa ana maumivu na pia angeweza kulia ila kutokana na tamaduni za Waswahili ilikuwa hatia mvulana huyo kuonyesha hisia zozote za uchungu kwa sababu alitarajiwa kukidhihaki kisu hicho na kudhibitisha kuwa amekuwa jogoo.

Jifanye ngozi yako imekufa ganzi
Kisu cha ngariba ukidhihaki

Ni kinaya mvulana aliyeenda jandoni kuambiwa kuwa akidhihaki kisu cha ngariba kwa sababu zifuatazo: Kwanza sifa ya kudhihaki ni ya kibinadamu, kijana huyo hawezi kukejeli kisu hicho na pili kisu hicho kina lengo moja mtu ambalo ni kumletea mvulana huyo maumivu mwilini. Maumivu hayo yangemfanya mvulana huyo kuogopa na kukosa nafasi ya kukifanyia kisu hicho mzaha au kejeli.

3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tulihakiki mbinu za mtindo ambazo zilitumiwa katika nyimbi teule za jadi ambapo tuliangazia mbinu kama vile: jazanda, taswira, tashihisi, kisengere nyuma, chuku na kinaya. Mbinu hizi zilitumiwa kujenga nyimbo hizi. Mbinu kama vile ya jazanda ilitumiwa kuwafunza wavulana tamaduni na matarajio ya jamii zao walipokuwa jandoni na hata kabla ya ndoa. Wanawake katika jamii ya Waswahili walifunzwa jinsi ya kurutubisha ndoa yao. Mbinu kama vile: takriri, taswira hisi na chuku zilitumiwa katika kuonyesha hisia mbalimbali katika sherehe tofautitofauti. Kwa mfano, katika sherehe za ndoa na kuzaliwa kwa watoto, wanajamii walidhihirisha kuwa na furaha isiyo na kifani. Kwa upande mwingine kifo kilipotokea, jamii ilipatwa na huzuni mwingi kiasi kwamba wengine walihisi kuaga dunia ndio suluhu tu kwa maisha yao. Mbinu kama vile kisengere nyuma ilisaidia katika kuelewa historia ya jamii ya Wakisii kama vile njaa iliyowakumba ikasababisha vifo vya watu wengi, madhara ya Vita vya Kwanza vya Dunia kwao na hata migogoro kati ya Wakisii na majirani zao kama Wamaasai na Wakipsigis. Isitoshe, mbinu ya kinaya ilitumiwa kuwakumbusha wavulana wawe jasiri wakati walipokuwa wakiingia jandoni. Wavulana hao waliambiwa wakidhihaki kisu cha ngariba. Katika sura inayofuata tutaangazia jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilitumiwa kuendeleza maudhui katika nyimbo teule za jadi.

SURA YA NNE

KUCHUNGUZA JINSI AMBAVYO MBINU ZA MTINDO ZILIVYOTUMIWA

KUFANIKISHA UWASILISHAJI WA MAUDHUI NA DHAMIRA YA

NYIMBO TEULE

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tutashughulikia maudhui ambayo yamedhihirika katika nyimbo za jadi za jamii teule. Maudhui ambayo yamejitokeza katika nyimbo hizo ni kama vile: bidii, mabadiliko, nafasi ya mwanamke kwenye jamii, taasubi ya kiume, dini, malezi, ndoa, tanzia, utamaushi na utamaduni.

4.1 Dhana ya Maudhui

Wataalamu mbalimbali wameeleza dhana ya maudhui. Kulingana na kamusi ya TUKI (2019), maudhui kuwa ni mambo muhimu yanayoelezwa kwenye kazi yoyote ya fasihi. Kwa mujibu wa Wamitila (2018), maudhui kuwa ni yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Maudhui yanaibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya kazi ya fasihi. Mtazamo huu unaifanya dhamira kuwa sehemu ya maudhui.

Kama asemavyo Rono (2013), maudhui ni mawazo ya jumla, mawazo mapana yanayowasilishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelezwa. Utoaji wa muhtsari wa masimulizi ni hatua ya mwanzo tu. Kauli za jumla ziunganishe mada na kipengele maalum cha usimulizi. Kauli za jumla lazima zifungamanishe na kazi yenyewe. Vilevile Kimani na Chimera (1999), wanaeleza maudhui kama ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha ya watu. Maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa na mwandishi hujitokeza. Kutokana na wataalaumu

hawa kinachodhihirika ni kuwa, maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Sura hii ilifanikishwa kupitia kwa mhimili miwili. Kwanza, kiwango cha semantiki ambacho kinashughulikia maana inayoibuliwa na lugha ambayo mtunzi ameamua kutumia. Mhimili huu ulitusaidia kuelewa maudhui ambayo yaliwasilishwa na watunzi mbalimbali kupitia kwa mbinu za mtindo. Mhimili wa pili ni kiwango cha utendakazi. Katika uchanganuzi huu, mhimili wa kiwango cha utendakazi unahusishwa na tathmini ya ufanisi wa mbinu za kimtindo katika kuwasilisha maudhui katika nyimbo teule za jadi za jamii ya Wakisii. Mhimili huu unazingatia kwa kiwango gani vipengele vya lugha ya kisanaa, kama vile kurudia, tanakali, tashbihi na methali, vinatimiza lengo la kuibua maudhui. Kwa mfano, mbinu ya kurudia inapotumika kwa mafanikio kusesitiza migogor, kazi au hata mabadiliko, inadhihirisha kiwango bora cha utendakazi wa lugha ya kisanaa katika nyimbo husika. Vilevile, matumizi ya methali au sitiari yanaposaidia kubeba maana fiche zinazorejelea imani, mila, au historia ya jamii, huwa ni kiashiria cha ufanisi wa mbinu hizo katika muktadha wa kifasihi. Kwa hivyo, mhimili huu hutumika kupima jinsi mbinu za kimtindo zinavyochangia kwa ufanisi katika kuwasilisha maudhui katika nyimbo za jadi za jamii ya Wakisii na Waswahili.

4.2.0 Maudhui Katika Nyimbo za Jadi za Jamii ya Wakisii

Kupitia kwa nyimbo za jadi za jami ya Wakisii maudhui mbalimbali yamechimuzwa kama vile: kazi, mabadiliko, ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii, taasubi ya kiume, utamaushi na tanzia.

4.2.1 Kazi

Dhana kazi imekuwa hata kabla ya binadamu kuumbwa, hivyo basi imejikita katika historia yake. Mwanzo wa kazi umeelezwa katika Biblia takatifu. Katika kitabu cha Mwanzo :1-15 tunaelezwa kuwa Mungu alifanya kazi ya kuumba dunia kwa siku sita,

hivyo basi Mungu anakuwa kielelezo bora cha kufanya kazi. Pia katika kitabu cha Mhubiri 3:13 tunaambiwa kuwa “Kila mtu anapaswa kula na kunywa na kufurahia kazi yake yote ngumu. Ni zawadi kutoka kwa Mungu.”. Kulingana na Mardon na wenzake (2021), kazi ni chochote kile ambacho mtu hufanya kwa lengo la kuwa na tija au umuhimu katika kuafikia mahitaji ya mwanadamu. Kulingana na Huvila (2006), kazi ni shughuli mbalimbali za binadamu zinazohusiana ambazo zina lengo wazi au lililofiche. Kwa jumla kazi ni shughuli zozote ambazo binadamu anatekeleza ambazo zaweza kuwa za kimwili au kiakili ili kuafikia lengo fulani. Jamii hii ilifanya kazi mbalimbali kama vile: kilimo, ufugaji wa wanyama, uwindaji, biashara na kadhalika.

Kupitia kwa wimbo wa *Obori bwa Baba* mbinu ya taswira uoni ilifanikiwa katika kuwasilisha ujumbe wake ambapo inataumiwa kufafanua jinsi mazao yalivyonawiri pale shambani hivyo basi walipaswa kuenda kuyavuna. Mama Ruth Mokeira alipohojiwa alisema kuwa asilimia kubwa ya jamii ya Wakisii ilijishughulisha na upanzi wa viazi vitamu. Kulingana na wenzake (2013), wameeleza viazi vitamu kuwa ni mboga ya mizizi yenye wanga, yenye ladha tamu. Ngozi yake ya nje ni nyembamba na kahawia na nyama yake ina rangi angavu, mara nyingi ya machungwa, lakini pia nyeupe, zambarau au njano. Unaweza kula viazi vitamu vikiwa vizima au vikimenywamenywa na majani ya mmea huo pia yanaweza kuliwa. Vyote viwili vinaweza kuitwa “viazi”, lakini viazi vitamu na viazi vyeupe vya kawaida havihusiani. Viazi vitamu ni chakula cha kiasili cha katika jamii hii. Kilienziwa kizazi cha jadi na hata kizazi hiki. Viazi vitamu vilikuwa vinaliwa wakati wowote: waliweza kuvitumia kama kiamsha kinywa, chakula cha mchana au chakula cha jioni

Amarabwani abana baido
Aamire buya mono
Gesaku giato tikegosira aseng'encho ye'nchara

Tafsiri

Viazi vitamu wana wetu
Vimekomaa vizuri sana
Ukoo wetu hauwezi kuangamia kwa sababu ya njaa

Wimbi pia mojawapo ya chakula ambacho ni maarufu miongoni mwa jamii ya Wakisii tangu jadi. Ilikuwa dhahiri kuwa wimbi ulienziwa na wakulima na wakati ulinawiri na kutoa mazo mengi mazuri walisherehekea. Kupitia kwa mbinu ya takriri na mbinu ya taswira, jamii ilionyesha furaha kwa sababu mwisho wa siku kazi ya mikono yao ilizaa matunda. Anna Onchari alifanunua mbona wimbo ni zao muhimu kwa jamii hii kwani kupitia kwa wimbi, wao hutayarisha ugali na uji pia. Kwa sababu hii kila familia ilijishughulisha na upanzi wake. Kabla ya kunawiri wimbi ulipiitia mchakato ambao ulimhitaji kila mkulima auzingatie ili usiharibike. Kando na kupanda, mkulima alihitaji kuupaliliana kuongeza mbolea baada ya kupalilia. Wimbi huo ulipoanza kukomaa alihitaji kuweka sanamu karibu na wimbi wenyewe na kuzuia ndege wasiuvamie kisha mwisho kabisa ni kuvuna. Ili mtu apate mazao ya kupendeza lazima mkulima angefuata mchakato huo wote ambao ungemgharimu muda mwingi, nguvu pamoja na pesa. Kutokana na maelezo ya wali ni kuwa, kuna kipindi ambacho jamii hii iliteseka kwa sababu ya njaa hivyo walipoona mazao yamenawiri shambani, hawangeweza kuificha furaha yao kwa sababu walikuwa wanajua watoto wao wako salama.

Obori bwa baba keande
Ee keande, obori bwa baba keande
Enyangweso yacha yaboria
Ee yaboria, enyangweso yacha yaboria

Tafsiri

Mtama wa nyanya umekomaa
Ee umekomaa, mtama wa nyanya umekomaa
Nzige watavamia
Ee watavamia, nzige watavamia

Kando na wimbi kuvamiwa na ndege, pia nzige walikuwa ni tishio kubwa kwa wimbi. Mbinu ya taswira sikivu ilitumiwa kuwasilisha ujumbe huu, milio ya mbweha iliposikika ilikuwa ni tahadhari kwao. Mzee Maoga alifafanua kuwa mlio wa mbweha ulitumiwa kama onyo kali kwa wakulima kuwa walistahili kuvuna wimbi kwa sababu ulikuwa umenawiri na ungevamiwa na nzige wakati wowote ule kama hawangeuvuna haraka sana na kuwarejesha katika janga la njaa ambalo walikuwa wamesahau.

Ekebwe ngiakura Manga nse
Ee Manga nse, ekebwe ngiakura Manga nse
Ee Manga nse, ee Manga nse
Baba motegere nyangweso ndi! ndi! ndi! ndi! ndi!

Tafsiri

Mbweha analia Manga chini
Ee Manga chini, Mbweha analia Manga chini
Ee Manga chini, ee Manga chini
Jamani tegeeni nzige ndi! ndi! ndi!

Jamii hii pia ilishiriki katika ufugaji wa mifugo mbalimbali kama vile: ng'ombe, mbuzi na kondoo. Mzee Ombuya alipoulizwa kuhusu manufaa ya mifugo alisema kuwa waliitumia katika kufanikisha sherehe zao za kitamaduni kama vile kulipa

mahari, kutoa kafara kwa Mungu wakati wa kuombea mvua inyeshe au kumshukuru Mungu kwa yale aliyoyatenda. Katika harakati zao za ufugaji walikabiliana na changamoto kuu ambayo ilikuwa ni wizi wa mifugo. Walivamiwa na jamii ya Wakipsigis na jamii ya Wamaasai, hivyo basi wavulana waliopelekwa jandoni walipewa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na wizi wa fugo. Ili kuonyesha thamani ya mifugo kwa jamii hii, mbinu ya taswira hisi ilitumiwa kuonyesha hasira ambayo wanajamii walikuwa nayo kutokana na wizi wa mifugo wao. Kwa upande mwingine waliwaibia Wakipsigis na Wamaasai mifugo ili kujitajirisha.

Abamanyi batochandire kera engaki, ee-yoo
Abasigisi batosamirie ee-yoo
Banto aba bairire chitugo chiaito ee-yoo
Toimoke bono iga tochiiranie ee-yoo

Tafsiri

Wamaasai wametusumbua kila wakati ee-yoo
Wakipsigis wametuibia ee-yoo
Watu hawa wamechukua mifugo wetu ee-yoo
Tuende sasa hivi tuwarudishe ee-yoo

Chiombe chachire Bomanyi
Inwe moracherite

Tafsiri

Ng'ombe ambao wameenda kwa Wamaasai
Ni nyinyi mtakao waleta

4.2.2 Mabadiliko

Mabadiliko ni aushi, huu ni msembo ambao ni maarufu sana kwenye jamii. Aristotle anasema kuwa mabadiliko ni mchakato ambao kitu au jambo fulani hufikiwa. Kulingana na Armstrong (2009), mabadiliko yoyote yanayotokea katika uongozi, waajiriwa na katika shughuli zozote zinazohusiana. Kwa mujibu wa Warraich na Bhardwas (2007), dhana mabadiliko inarejelea mabadiliko ambayo taasisi, shirika au

mtu anayofanya ili kuweza kushughulikia urekebishaji wa jambo lolote lile. Kwa jumla mabadiliko ni mageuzi ambayo mtu au jamii hushuhudia.

Kupitia kwa mbinu ya taswira uoni, maudhui ya mabadiliko yanaendelezwa. Mabadiliko hay oni yale ambayo vijana walikuwa wanashuhudia baada ya kutoka jandoni kwa sababu sasa hawakuwa watoto tena. Mzee Maoga alisema kuwa kwenye sherehe za miviga hasa za wavulana kupelekwa jandoni, wavulana hao waliimbiwa nyimbo ambazo zilidhihirisha kuwa wamekuwa watu wazima hivyo basi tabia za kitoto walistahili kuzitupilia mbali. Kando na tabia hizo wavulana hawa walikumbushwa kuhusu majukumu yao na pia na matarajio ya jamii kwao. Kitu cha kwanza ni kuwa baada ya sherehe hiyo, wavulana hao walichukuliwa kuwa wamekuwa wanaume. Kutokana na kupanda hadhi, sasa walipewa majukumu mengi mapya kwa sababu awali kazi yao kuu ilikuwa ni kupeleka ng'ombe malishoni ila baada ya kupashwa tohara vijana hao walitakiwa kuenda vitani hasa kupigana dhidi ya wizi wa mifugo wao na pia kudumisha usalama kijijini. Wavulana huo pia hawakupaswa kukaa karibu na mama zao kwa sababu sasa wamekuwa wanaume. Akina mama wa wavulana waliopashwa tohara pia walikumbushwa kuwaheshimu wavulana hao kwani kuna kazi ambazo hawakustahili kufanya tena kama kuenda mtoni ama kuingia jikoni kupika kwa sababu hizo zilichukuliwa kama kazi za wanawake au wavulana ambao hawakuwa wametahiriwa. Hali hii inadhihirika kupitia kwa ubeti ufuatao:

Obeire omomura, beire omomura eee-oyoo
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo
Nguba boigo, na nguba boigo eee-yoo
Ng'ina amosike, ng'ina amosike eee-yoo
Tomotoma roche, tomotoma rochee oyoo oyoo

Tafsiri

Amekuwa mwanamume, amekuwa mwanamume eee-oyoo
Atayarishiwe mkuki, atayarishiwe mkuki eee-oyoo
Pia msisahau mshale, na mshale pia eee-oyoo
Mama mheshimu, mama mheshimu eee-oyoo
Usimtume mtoni, usimtume mtoni oyoo oyoo

Mabadiliko mengine yaliyoshuhudiwa ni baada ya mama kujifungua. Katika wimbo wa *Sindigisa*, mtunzi alitumia mbinu ya jazanda katika kueleza maudhui ya mabadiliko. Anarejelea mabadiliko haya kama kutoka juu ya mti. Mama Bangweso alieleza kuwa kipindi cha ujauzito kwenye jamii ya Wakisii kilichukuliwa kuwa kipindi kigumu sana. Katika kuonyesha ugumu wa kipindi hicho, mbinu ya jazanda ilitumiwa kufafanua zaidi ambapo kipindi hicho kilirejewa kuwa juu ya mti. Kwani mtu akiwa juu ya mti hakuna na starehe kwa sababu mti unaweza kukatika wakati wowote ule. Yaani jambo lolote laweza kufanyika na mama huyo akapotezza ujauzito wake au akaaga dunia. Hivyo basi baada ya mama kujifungua salama walianda sherehe kubwa kusherehekea mafanikio hayo ambayo ni sawa na kuteremka kutoka juu ya mti. Mbinu inadhihirika katika ubeti ufuatao:

Nyaboke orure omote igoro
Ekiomogoko no'mwana otoire

Tafsiri

Nyaboke ameteremka kutoka juu ya mti
Tuna furaha kubwa sana kwa sababu ametuletea furaha

4.2.3 Migogoro

Kwa mujibu wa Coser (1956), anaeleza migogoro kama mapambano kati ya makundi yanayopingana kuhusiana na maadili na kutaka kutwaa hadhi, nguvu hasa za uongozi na raslimali. Kulingana na Levi na Weber (1968), ni kuwa uhusiano wa kijamii unarejelewa kama mgogoro hasa matendo ya mtu fulani yanapochukuliwa kuwa ya kusudi la kibinafsi na yanayoenda kinyume na kikundi au makundi. Kwa jumla,

mgogoro ni hali ambapo watu au makundi fulani ya watu yanaona na kuhisi kuwa wengine wanafanya matendo ambayo yana athari hasi kwa jamii.

Nyimbo hizi za jadi zilitumiwa kuonyesha migogoro mbalimbali kwenye jamii. Mbinu ya takriri na mbinu ya taswira uoni zilitumiwa katika kuweka wazi mgogoro kati ya Wakisii na majirani zao. Migogoro hii ilisababishwa na mambo mbalimbali. Katika jamii ya Wakisii tangu jadi hadi sasa hivi kuna migogoro kati yao na jamii ya Wamaasai pamoja na jamii ya Wakipsigis. Migogoro hii ilisababishwa na wizi wa mifugo, chemchemi za maji na mbuga za malisho ya mifugo wao. Walifanikiwa kutumia mbinu hizo kueleza silaha ambazo zilihitalika ili kufanikisha shughuli hiyo.

Mzee Onyancha alieleza kuwa kutokana na wizi wa mifugo, wavulana kwenye jamii ya Wakisii walipotahiriwa, mojawapo ya jukumu lao ni kulinda mifugo ili wasiibwe na majirani wao. Kando na hayo, wavulana hao walitarajiwa kushiriki katika vita vilivyotokana na wizi wa mifugo. Hali kadhalika, walitarajiwa kuzuia majirani wao wasilishe mifugo kwenye mbuga zao na kulinda chemchemi za maji. Wavulana hawa pia walihitalika kushiriki katika wizi wa mifugo na ndio sababu baadhi ya nyimbo zilizoimbwa pale jandoni zilibeba ujumbe huu ili kuonyesha matarajio ya jamii kwao baada ya kutoka jandoni. Nyimbo zifuatazo zinadhihirisha maudhui haya ifuatavyo:

1.Obeire omomura, obeire momura ee-oyoo
Bono mambia, bono mambia ee-yoo
Aturerigwe ritimo, aturerigwe ritimo
Na nguba boigo, na nguba boigo
Arwane Sigisi, arwane bosoba ee-oyoo

Tafsiri

Amekuwa mwanamume, amekuwa mwanmume ee-yoo
Sasa hivi asubuhi, sasa hivi asubuhi ee-yoo
Atayarishiwe mkuki, atayarishiwe mkuki
Na mshale pia, na mshale pia
Aende apigane kwa Wakipsigis, apigane kwa Wamaasai

2.Bamura ooo, bamura ooo

Binto mbikone, naende mbirende
Chiombe chachire Bomanyi
Intu torachirente

Tafsiri

Wavulana ooo, wavulana ooo
Vitu sasa hivi ni maajabu na vinatisha
Ng'ombe wetu waliochukuliwa na Wamaasai
Sisi ndio tutawaleta

Mzee Onyancha aliendelea kueleza kuwa mgogoro mwingine ambao ulidhihirika kupitia kwa nyimbo za jadi ni kati ya wanajamii na wanyama pamoja na ndege. Mgogoro huu ulitokana na kuvamia mimea ambayo ilikuwa imekomaa pake shambani. Athari ya uvamizi wa mimea na mazao shambani ni kuwa jamii iliathirika kwa sababu ya njaa. Mojawapo ya visababishi vya njaa katika jamii hii kati ya mwaka wa 1888 na mwaka wa 1892 ilikuwa ni vyakula vilivyokuwa shambani kuvamiwa na nzige. Hivyo basi ili kuzuia njaa walihimizana kupitia kwa nyimbo umuhimu wa kukinga mimea yao kutokana na uvamizi wa wanyama na ndege. Shambani walihimizwa kuweka sanamu kando na sanamu pia wailinde mimea yao kwa zamu mchana na usiku. Mnyama yeyote angepatikana akivamia mimea angeuliwa papo hapo. Katika beti hizi mbili zifuatazo maudhui ya mgogoro yalijengwa kupitia kwa taswira mwendo ambayo ilionyesha jinsi ambavyo nzige walikuwa safarini ili kuvamia mimea na taswira sikivu ambapo kilio cha mbweha kilisikika ishara ya kuwaonya wanajamii kuhusu hatari iliyowasubiri.

Ekebwe ngiakura Manga nse
Ee Manga nse, ekebwe ngiakura Manga nse
Ee Manga nse, ee Manga nse
Baba motegere nyagweso ndi! Ndi! Ndi!

Enyangweso yacha yaboria,
Ee yaboria, enyangweso yacha yaboria
Ee yaboria, ee yaboiria
Baba motegere nyangweso ndi! Ndi! Ndi!

Tafsiri

Mbweha analia kule Manga
Ee kule Manga, mbweha analia kule Manga
Ee Manga, ee Manga
Jameni tuweni macho kwa sababu ya nzige

Nzige wanakuja na kuila (mtama)
Ee yaila, nzige wanakuja kuila
Ee yaila, ee yaila
Jameni tuweni macho kwa sababu ya nzige

Kutokana na wimbo huu wanajamii walitahadharishwa wawe macho kwa sababu nzige wameanza kuja kuvamia mtama ambao umenawiri shambani. Na nzige wakivamia mtama huo ungepelekea jamii kuvamiwa na janga la njaa ambalo lingepelekea vifo vya wanajamii wengi. Ili kujikinga dhidi ya janga hili la njaa ilibidi wanajamii wapigane na nzige mchana kutwa na usiku kucha.

4.2.4 Ndoa

Kulingana na Crossman (2019), ni kuwa katika jamii nyingi ndoa inachukuliwa kama maafikiano ya kijamii ambayo ni ya milele. Anaendelea kusema kuwa ndoa ni uhusiano kati ya watu wawili ambao umekitwa katika haki sawa na mjukumu sawa kati yao. Ndoa ina mizizi kwa uhusiano wa kimapenzi ila si kwa ndoa zote. Kama wasemavyo Russel (1959), ndoa ni uhusiano wa kibinafsi kati ya mwanamke na mwanamume na uhusiano wao wa kibayolojia. Ndoa kama taasisi ya kijamii kisheria na kidini imeshuhudia mabadiliko mengi sana. Kwa kijumla ni makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke.

Mbinu ya kisengere nyuma ilitumiwa ili kuwakumbusha wanandoa kuhusu imani ya jamii kuhusu ndoa. Mbinu ya jazanda pia ilitumiwa kuisitiza umuhimu wa watoto kwenye ndoa. Katika jamii yoyote ya Kiafrika ndoa ni taasisi muhimu. Kutokana na umuhimu wa taasisi hii ndio sababu jamii ya kale hata sasa inaandaa sherehe kubwa

sana ili kusherehekea hatua hiyo ambayo ilichukuliwa na watu hao wawili. Nyimbo hizi za ndoa zilitumiwa kuwaelimisha wanandoa kuhusiana na masuala ya ndoa. Mama Kwamboka alieleza kuwa kupitia kwa nyimbo hizi, wawili hawa walifahamishwa kuhusu matarajio ya jamii kwao. Mojawapo ya matarajio ya wanajamii kwa wanandoa ilikuwa ni lazima wapate watoto ili kuendeleza kizazi chao. Ikiwa wanandoa wangekosa kufanikiwa kupata watoto walipelekwa kwa madaktari wa kienyeji na kwa waganga ili watibiwe. Iwapo wangekosa kupata watoto baadaya matibabu hayo, mwanamume alishinikizwa kuo a mke mwingine ili amzalie watoto. Katika jamii ya Wakisii kupata watoto wengi hasa wa kiume ilikuwa ni fahari, kwa sababu watoto hawa wangewasaidia wazazi wao kufanya kazi za shambani. Na pia wasichana wakiolewa familia ingetajirika kwa sababu ingepata mali nyingi kutoka na mahari ambayo yalilipwa kwa kutumia mifugo kama vile: ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Abagusii bakare bagakwana
Bagakwana bagateba ng'a
Oyotabwati omwana no'mote mwomo
Oyobwate omwana okoboko kwaye gwaichoire
Nyasaye abakonye monyore abana

Tafsiri

Wakisii wa kitambo wakaongea
Wakaongea wakasema kuwa
Asiye na mtoto ni mti mkavu
Aliye na mtoto mkono wake umejaa
Mungu awasaidie mpate watoto

Nyimbo za ndoa pia zilitumiwa kukashifu matendo hasi ambayo yaliendelezwa na wanaume. Tendo la kwanza lilikashifiwa sana kupitia kwa nyimbo hizo ni talaka, mume alipotoa talaka ni ishara ya kuwakosea mababu heshima. Kulingana na TUKI (2019), talaka ni idhini ya kisheria ya kumwacha mume au mke. Kando na talaka

nyimbo hizi zilitumiwa kukashifu kitendo cha kumpiga bibi na kwa jumla kukemea mwanamume ambaye ni katili kwa mke wake. Kwa sababu mwanamume aliyempiga mke wake angeweza kuchangia katika kutoroka kwa mwanamke huyo na kurudi kwao. Wanaume hao katika jamii ya Wakisii walirejelewa kama ‘*abaisia*’ kumaanisha mwanamume au mvulana ambaye hajatahiriwa na hajakomaa kiakili. Wanaume kama hao walifukuzwa kutoka kwenye jamii na kuchukuliwa kama wasikwao. Maudhui haya yanadhihirika katika ubeti ufuatao:

Nkamoseria genda! Genda! Eee nkamoseria pi!
Agantebia oikire, tari kogenda ande pi
Abanto bakabora, eee negesaku gekabora
Kwabeire kironchi yara, kironchi otarochi
Nkorutwa ore omware, otabwati mochiande

Tafsiri

Nikafukuza enda! Enda! Eee nikamfukuza kabasa!
Akaniambia maefika, haendi mahali kabasa
Watu wakasema, eee na ukoo ukasema
Umekuwa msikwao, msikwao asiyeona
Utatupwa mbalmbali, asiyekuwa na boma mahali

Mzee Nyakweba alieleza kuwa wanandoa walikumbushwa kuhusu umuhimu wa kufanya kazi. Mwanamke na mwanamume walitarajiwa wote waende shambani wakalime ili familia yao isianganie kwa sababu ya njaa. Iliaminiwa kuwa ikiwa wawili hao wangewajibika, familia yao itajitosheleza na ingeheshimiwa na kila mtu. Wanajamii walikuwa na furaha sana, walimwambia mwanamume huyo alime shamba la wazazi wake ili wasife kwa sababu ya njaa. Walimwambia kuwa huyo mwanamke ambaye ameoa walistahili washirikiane katika kufanya kazi zote za shambani. Ili kuonyesha nafasi ya mwanamume katika ndoa, mtunzi alituma mbinu ya jazanda ambapo alimfananisha mwanamume na fahali. Hali hii pia ilitumiwa kujenga mwanamume kama mwenye nguvu na anastahili kuonyesha hilo katika maisha yake

ya kila siku ya ndoa. Mbinu ya tashabihi pia ilitumiwa kumsawiri mwanmume kuwa mwenye nguvu kama vile: ‘aliye na nguvu kama simba’. Mzee Nyakweba alisisitiza kuwa jamii iliamini kuwa kutokana na uwezo wa mwanamume, alitarajiwa kuwa kiongozi kama simba alivyo kiongozi wa porini na kuheshimiwa na kila mtu.

Eee eheri ya tata ereme embonga
Eheri ebwate chinguru buna esironi
Eee bono yaretire emanwa nka
Eheri ereme, ereme buya

Tafsiri

Naam fahali ya baba ilime shamba la baba
Fahali aliye na nguvu kama simba
Naam ameleta ndama nyuma
Fahali alime vizuri, ilime vizuri

Katika wimbo *Abagusii Bakabora*, mbinu ya taswira uoni ilitumiwa kumkumbusha yule mwanamke anayeolwa kuwa anajukumu la kukidhi mahitaji ya familia yake. Mtunzi alichora taswira ya jembe ambalo mwanamke huyu alihitaji na kwa wale ambao ni wavivu alichora taswira ya shamba ambalo walipaswa kupewa ili nguvu zao wazitumie pale. Mama Bangweso alieleza kuwa katika ndoa, wanawake ambao ni wavivu walisutwa. Wengi wa wanawake hao walikusanyika katika vikao vidogo ambavyo lengo kuu lilikuwa ni kupigana vijembe. Baadhi yao pia walipenda kuzurura kwenye nyumba za watu wengine kwa sababu hawakutaka kufanya kazi. Familia husika zilihimizwa kumpa mwanamke huyo jembe ambalo lilinelewa vizuri aende akalime. Kwa kuwa mwanamke huyu alikuwa na nguvu na muda mwingi wa kupoteza katika uzururaji wake, walitakiwa wampee shamba lenye magugu ambalo lingemfanya atumie nguvu kupita kiasi hivyo akose muda wa kuzurura na kupiga watu vijembe. Kwa jumla wimbo huu ulitumiwa kuwakumbusha wanandoa umuhimu wa kutia bidii maishani. Hali hii inadhihirika ifuatavyo:

Omong'ere obokombe, nekebago egesera
Nekebago egesera, agende kwabusera omogondo
Omokungu sioma siomi nkayi akomanya
Nkayi akomanya bwarugirwe aegwe obokombe
Moe oboremo bwekenyambi areme abwate omotwe

Tafsiri

Mpini safi, aende kufagia shamba
Na jembe lenye mpini mzuri, aende kufagia shamba
Mwanamke anayependa kuchungulia, anajua aje
Anajua aje kumepikwa, apewe shamba
Apewe shamba lenye magugu alime ashike kichwa

4.2.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Kulingana na Birke (1986), pamoja na Lovenduski na Randall (1993), wanakubaliana kuwa hii ni hali inayoeleza tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hawa. Kwa mujibu wa Matteru (1982), taswira ya mwanamke inayojitokeza katika vipera vingi vya fasihi simulizi ni ile inayomuonyesha kuwa ni mama wa nyumbani, chombo cha starehe, anayezaa na mwenye heshima katika jamii. Miongoni mwa jamii za Kiafrika, kila jinsia ilikuwa jukumu lake. Mama Onchari alisema kuwa wanamke hakustahili kutekeleza majukumu ya mwanamume na mwanamume hakustahili kutekeleza majukumu ya mwanamke. Majukumu haya yalidhihirishwa kupitia kwa nyimbo zao.

Katika wimbo wa *Abagusii Bakabora*, mbinu ya jazanda na taswira uoni ilitumiwa katika kuwafunza wanandoa kuhusu umuhimu wa kuwa na watoto kwenye ndoa kwa sababu bila watoto has awa kiume iliaminiwa kuwa familia hiyo ingekosa mrithi. Hivyo basi ilitarajiwa kuwa baada ya mwanamke kuolewa alistahili kupata watoto. Mama Onchari alisema kuwa baadhi ya nyimbo ambazo zilitungwa zilikuwa na nia ya kuwatisha na kuwashinikiza wanandoa kupata watoto. Kwa mfanao katika wimbo wa '*Abagusii Bakabora*' katika mshororo ufatao: 'yule ambaye hana mtoto ni mti mkavu' hii nijazanda inayomaanisha kuwa watu ambao hawana mtoto hawana manufaa

yoyote maishani. Hivyo basi wengi wao walikuwa wanajipata katika shinikizo la kupata watoto.

Wasichana au wanawake walipokuwa wanatayarishwa kwa ajili ya ndoa jukumu lao muhimu sana lilikuwa ni kupata watoto ili wasaidie katika kuendeleza kizazi. Kutokana na umuhimu wa watoto, wanandoa walipokosa kufanikiwa kupata watoto hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuwasaidia wapate watoto na wakati mwingine mwanamume alilazimishwa kuoana tena kwa sababu wengi waliamini kuwa mwanamke ndiye alikuwa na shida. Nyimbo za ndoa zilipoimbwa, mwanamke alikumbushwa kupata watoto kwani hilo ndilo jukumu lake kuu, iwapo hangepata watoto angerejelewa kama mti mkavu ambao hauna maana yoyote kwa jamii. Nafsi hii inadhihirika ifuatavyo:

Bagatotebia amang'ana aya
Oyotabwati omwana no mwomo
Oyobwate omwana okoboko kwaye gwaichoire
Nyasaye abakonye monyore abana

Tafsiri

Wakatuambia maneno yafuatayo
Yule ambaye hana watoto ni sawa na mti kavu
Yule ambaye ana watoto mikono yake imejaa
Mungu awasaidie mpate watoto

Mama Moraa alieleza kuwa jukumu lingine la mwanamke lilikuwa ni kuteka maji mtoni au kisimani na pia kuandaa chakula. Hii ni kazi ambayo mtu wa jinsia ya kiume hakustahili kutekeleza kamwe, kwani kuteka maji au kuingia jikoni kupika kungekuwa ni kujidhalilisha na ni jambo ambalo lingeleta aibu kwa wanajamii. Mvulana alipopelekwa jandoni, mama yake alikumbushwa kuwa mvulana huyo sasa hivi amekuwa mwanamume kamili hivyo basi alistahili kuheshimiwa, na heshima hii ingedhihirika kwa kutotumwa mtoni na mama yake. Hivyo mama alistahili kufanya kazi hiyo. Mbinu ya takriri ilitumiwa katika kuisitiza jukumu la mwanamke katika

jamii, mojawapo ya kazi hiyo ilikuwa ni kuenda mtoni. Mbali na hilo, taswira hii inatumiwa kuwakumbusha akina mama kuwa hapaswi kuwatuma wavulana hao mtoni kwani wamekomaa na wana majukumu mengine muhimu ya kutenda na wali si kuonekana na mtungi wakienda mtoni. Maudhui haya yanaendelezwa ifuatavyo:

Arwane Sigisi, arwane Bosoba eee-yoo
Ng'ina amosike, ng'ina amosike eee-yoo
Tamotoma roche, tamotoma roche eee-yoo
Obeire buna eheri, aegwe obweri bwaye eee-yoo

Tafsiri

Apigane kwa Wakipsigis, apigane kwa Wamaasai eee-yoo
Mama yake amuheshimu, mama yake amuheshima eee-yoo
Asimtume mtoni, asimtume mtoni eee-yoo
Yeye ni ndume, apewe zizi lake eee-yoo
Katika nyimbo za jadi mwanamke anachorwa kama pambo.

Katika wimbo wa *Tiga Korera Okure* mwanamke alichorwa kama kiumbe dhaifu au mnyonge aliyeathiriwa sana kutokana na kifo cha mpendwa au jamaa yake. Mtunzi alitumia mbinu ya taswira hisi katika kuonyesha kuwa manamke alikuwa mwepesi wa hisia. Kupiia kwa wimbo huu mwanamke anaambiwa kuwa asilie kwa sababu kilio chake hakiwezi kumrejesha mtoto yule aliyeaga. Mama Onchari wakiwa na Mokeira walieleza kuwa nyimbo nyingi za mbolezi zina beti ambazo zilimfariji mwanamke asilie wala asihuzunike wala asiwe na uchungu mwingi kwa sababu hakuna manufaa yoyote pale. Walikumbushwa kuwa kifo kimekuwapo kutoka kitambo na kingeendelea kuwepo hivyo basi walistahili kukubali yaliyotokea na kuendelea na maisha yao. Kwa upande mwingine, ilikuwa hatia kubwa sana machozi ya mwanamume kuonekana. Katika mazishi, wanawake ndio walionekana wakilia hata wengine wakazirai huku wanaume wakiwa wametulia tu. Nafasi hii inadhihirika ifuatavyo:

Baba ng'ina Kwamboka, notana korera okure
Baba ng'ina Kwamboka, notana korera okure
Bororo mbori goita, kanga bwaitire abange
Amakweri namakoro, notana korera baba

Tafsiri

Mama ya Kwamboka, haina haja ya kulia
Mama ya Kwamboka, haina haja ya kulia
Uchungu huwezi kukuua, ungekuwa umeua wengi
Kifo ni cha kale. Haina haja ya kulia

Kupitia kwa baadhi ya nyimbo za jadi, mwanamke alichorwa kama tu ambaye ni mvivu na aliyekuwa akipenda udaku. Jamii yoyote ile ilitamini watu ambao ni wachapakazi iwe mwanamke au mwanamume, mtoto au mzee. Kutokana na kuthamini bidii, Mama Ruth Mokeira alieleza kuwa jamii hii ilitenga kazi ambazo zingefanywa na watoto, vijana, wanawake na wanaume. Ili kuelewa umuhimu wa kazi, mtunzi aitumia mbinu ya taswira mwendo na taswira uoni katika kuelezea hulka ya wanawake wavivu na wanaopenda kuzurrura jambo ambalo linapelekea familia zao kuumia kwa sababu ya njaa. Katika jamii ya Wakisii wasichana na wanawake walistahili kuenda mtoni kuteka maji na hata kuenda shambani. Ila kuna wakati mwingine ambapo baadhi ya wanawake walikusanyika kwenye vikao ili kuendeleza masengenyo na kuwapiga watu wengine vijembe. Kutokana na hulka kama hizi wanawake hawa walisahau kufanya kazi hivyo kupelekea familia zao kuumia kwa sababu ya njaa. Wanawake hao walipogundua kuwa hawana chakula walizunguka katika kila boma ili kutafuta chakula. Tabia hii ilikashifiwa kupitia kwa nyimbo za ndoa.

Mwanamke alihimizwa kuwa baada ya kuolewa angetafuta jembe nzuri aende shambani ili familia yake isife kwa sababu ya njaa. Mwanamke alikumbushwa kuwa

jukumu la kuhakikisha kuwa hakukuwa na njaa ni lake. Kwa wale ambao ni wavivu, jamii ilihimizwa iwape jembe na shamba ambalo lilikuwa na magugu mengi sana waende wakalime. Sababu ya kupewa shamba lenye magugu ilikuwa ni kuwakumbusha umuhimu wa kutia bidii hasa shambani. Iliaminiwa kuwa iwapo wangukuwa na mazoea ya kulima shamba lao kila mara, shamba lao halingekuwa na magugu yoyote hivyo basi kuandaa shamba lenyewe kwa ajili ya upanzi wa vyakula ingekuwa rahisi sana.

Omokungu sioma, siomi nkayi akomanya bwarugirwe
Omokungu sioma siomi moe oboremo bwekenyambi
Areme abanto mbaku nenchara

Tafsiri

Mwanamke anayependa kuzururazurura, amejuaje kumepikwa hapa
Mwanamke anayependa kuzururazurura, apewe shamba lenye magugu
Alime ili jamaa yake isife kwa sababu ya njaa.

4.2.6 Taasubi ya Kiume

Kulingana na Harrison na Michelson (2019), taasubi ya kiume ni hali ya mwamume kutwazwa katika jamii huku mwanamke akitwezwa. Anaendelea kueleza kuwa mwanamume hunyanyuliwa au huwekwa mbele au juu kwa mambo mbali kwenye jamii huku mwanamke akidharauliwa na kuchukuliwa kama kiumbe ambaye ni mnyonge. Taasubi ya kiume pia hujulikana kama ubabedume. Katika jamii za Kiafrika mtoto wa kiume au watu wa jinsia ya kiume walikuwa wametwazwa sana ikilinganishwa na mtoto wa kike au watu wa jinsia ya kike kiasi kwamba wanandoa walipokosa kujaliwa mtoto wa kiume, jamii ilimshinikiza mwanamume aoe tena ili huyo mwanamke mwingine amzalie mtoto wa kiume.

Watoto kwenye jamii ya Wakisii walithaminiwa sana. Kwa sababu waliaminiwa kuwa ndio wangeendeleza kizazi cha ukoo wao. Mtoto wa kiume alithaminiwa sana ikilinganishwa na mtoto wa kike. Wakisii husema ‘*Nsinyo etari momura yachandekire*’ yaani ‘ua ambao hauna mtoto wa kiume kutakuwa na shida’. Mtoto wa kiume alipozaliwa, shangwe, nderemo na vigelegele vilikuwa vikihanikiza kote. Sherehe kubwa iliandaliwa ambayo ilidumu wa siku tatu au nne ili kufurahia baraka hiyo. Sababu ya kumsherehekea mtoto wa kiume sana ni kwa sababu iliaminiwa kuwa akikomaa aliaminiwa kuwa angedumisha usalama bomani na hata kijijini. Mvulana huyu angezuia wizi wa mifugo na hata hakuna mtu ambaye angejaribu kunyakua shamba lao. Kwa upande mwingine msichana hakusherekewa sana kwa sababu waliamini kuwa msichana akikomaa angeolewa aende kuendeleza kizazi cha familia ingine hivyo basi walikuwa wanamwona kama mgeni. Mtoto wa kiume alirejelewa kama nyota ambayo ingeleta mwanga kwa wanajamii kando na kuwa nyota mtoto huyu walisema kuwa kiumbe muhimu sana na kila mja alialikwa aje ashuhudie. Katika ubeti huu, mbinu ya jazanda ilitumiwa katika kuonyesha thamani ya mtoto wa kiume kwa jamii. Ambapo mtoto huyu anaitwa nyota. Kando na hapo mbinu ya chuku ilitumiwa kuonyesha furaha ya watu kwani watu kutoka pembe zote wanaalikwa kuja kujionea nyota hiyo

Eng’enang’eni yababrire, eee yabarire eee yabarire
 Omonto bweng’encho oikire, eee oikire eee oikire
 Koru Mocha inchwo morore eee morore eee morore
 Korwa maate inchwo morore eee morore eee norore
 Egesaku giato bono giatenenire eee giatenenire

Tafsiri

Nyota imeng’aa, eee imeng’aa eee imeng’aa
 Mtu wa maana amefika, eee amefika eee amefika
 Kutoka mashariki njoo muone, eee muone eee muone
 Kutoka chini njoo muone eee muone eee muone
 Ukoo wetu sasa umesimama eee umesimama

Kutokana na maelezo ya Mayaka ni kuwa mwanamume hakustahili kuonyesha hisia zake. Mwanamume hakustahili kutikiswa na chochote kile, iwe kifo, maradhi au janga lolote lile. Kwa mfano mtu alipoaga dunia, wanaume walikumbushwa kuwa wao ni ‘*chiheri*’ yaani wao ni dume. Dume ni mnyama jasiri kwa hivyo sawa na fahali wanaume walikumbushwa kuwa machozi yao hayakupaswa kuonekana. Kulingana na Matei (2020), katika riwaya ya Chozi la Heri tunakutana na mhusika anayejulikana kama Ridhaa. Baada ya Ridhaa kuipoteza familia yake kupitia kwa mkasa wa moto, alijipata machozi yamefurika machon mwake. Katika hiyo hali ya majonzi, Ridhaa anakumbuka maneno ya nyanya yake,” Ridhaa mwanangu, mwanamume hufumbika hisia. Machozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha. Hukuna kujimbua hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi. Ulitunukiwa makoo.” Ni wazi kupitia kwa maneno ya nyanya yake Ridhaa kuwa mwanamume hapaswi kulia, kilio ni cha wanawake ambao wanachukuliwa kuwa ni wanyonge. Hawapaswi kuonyesha kuwa wao ni wanyonge kwa sababu ikiwa mwanamume ni mnyonge basi hakuna mtu atakayeilinda familia hatari yoyote itakapotokea.

Imani hii inadhibitishwa na Sowah (2019), ambaye alifanya utafiti katika jamii ya Waghana ambapo wanamini kuwa machozi ya mwanamume hayakupaswa kuonekana. Katika utafiti wake aliambiwa kuwa “Wanaume halisi hawalii.” Huu ndio mkondo ambao wavulana katika jamii hiyo walikutana nao na ndio mkondo wanaoufuata. Mwanamume kulia ilichukuliwa kuwa ni mnyonge hivyo basi kukosa kuheshimiwa na wanajamii.

Mtunzi wa *Tiga Korera* alitumia mbinu ya jazanda katika kuonyesha nafasi ya mwanamume. Jamii ilimlinganisha mwanamume na dume, hivyo basi iliamini kuwa mwanamume alikuwa na nguvu na hakupaswa kuonyesha hisia zozote haza za huzuni. Mzee Mayaka alidhibitisha haya kwa kufafanua kuwa wanaume waliambiwa kuwa

kulia ni kwa wanawake na unyonge hukuumbiwa jogoo bali uliumbiwa makoo. Kutokana na imani hii wanaume wengi waliathirika kutokana na msongo wa mawazo kwa sababu waliogopa kujieleza kwani waliona wakidhihirisha hisia zao wangeonekana kama viumbe ambao ni wanyonge.

Mariga ye'chiheri tarikororekana pi!
Mosacha tana korera, eye ne eheri
Okorera nokwa'bakungu, remereria amakweri

Tafsiri

Machozi ya dume hayaonekani kabsa!
Mwanamume haina haja ya kulia, kwani wewe ni dume
Kulia ni kwa wanawake, vumulia kifo

4.2.7 Utamaushi

Maisha aishiyo mwanadamu ni mafupi. Mwanadamu anao uhuru wake binafsi, kuna kukata tamaa kunakosababishwa na masuala ya mapenzi, kifo, kupoteza kazi na mikasa mbalimbali. Kulingana na Wamitila (1998), anaeleza kuwa Kezilahabi anayaona maisha kama dubwana lisilo na maana na kwamba mwanadamu amekuja duihani kuteseka. Wahusika wa kazi nyingi za Kezilahabi wamesawiriwa wakiwa wamechanganyikiwa au kukata tamaa kutokana na hali ngumu ya maisha. Hali hii ndiyo inafanya wahusika wengi wakuu waishie kwa vifo hasa kupitia kwa kujitia kitanzi. Kwa jumla utamaushi ni hali ya kukosa kuwa na tamaa au matarjio ya kupata kitu; kata tamaa. Watu wengi kwenye jamii hutamauka kwa sababu mbalimbali. Sababu mojawapo ya kutamauka ni kifo. Kifo kinapoifika familia fulani jamaa hiyo huona kuwa wanatembea katika giza. Mwanga ambao ulikuwa kwenye familia hiyo huzimika ghafla, haijalishi kama ni kifo cha mtoto au mzazi.

Katika wimbo wa *Tiga Korera*, ubeti wa kwanza umetumia mbinu mbalimbali katika kujenga maudhui ya utamaushi. Kwanza, alitumia maswali ya balagha ambayo yanaonyesha kuwa mzazi huyu hatapata mtoto mwingine ambaye atafanana na yule

ambaye Aliaga. Hali kadhalika, mtunzi alitumia mbinu ya takriri aktia kuonyesha kuwa mtoto huyo ameenda kabisa na hakuna ambaye angelizaja pengo lilioachwa. Mwisho kabisa, alitumia mbinu ya taswira hisi kuonyesha hisia za huzuni zilizotokana na kifo hicho. Ubeti huu uliimbwa na mzazi aliyefiwa na mtoto wake mpendwa. Alidhihirisha uchungu mwingi kutokana na kifo kilichomfika. Hakuwa na matumaini ya kupata au kujaliwa mtoto mwingine ambaye angeweza kujaza pengo ambalo liliachwa na binti yake. Mzazi huyu alifikia ukingoni ishara ya kuwa alitamauka. Sababu ya utamaushi wake ni kuwa: ingawa alikuwa na watoto wengine na pia hata angejaliwa na watoto wengine, watoto hao kisura, kiumbo au kitabia hawangeweza kufanana na yule aliyeaga sababu nyingine ni kuwa mzazi huyu na hofu kwa sababu umri wake umezidi ule unaotarajiwa kupata mtoto. Kutokana na mambo haya mzazi huyu alikuwa na huzuni na alidhihirisha hali yake ya kutamauka kupitia kwa wimbo huu wa mbolezi. Maudhui ya utamaushi yalidhihirika ifuatavyo:

Ng'ai ndarusie omwana inga Kwamboka?
Ng'ai ndarusie omwana onge Kwamboka?
Kwamboka ototigire ochire pi!
Kwamboka ototigire ochire pi!

Tafsiri

Nitatoa mtoto mwingine wapi aliye kama Kwamboka?
Nitatoa mtoto mwingine wapi aliye kama Kwamboka?
Kwamboka ametuacha ameenda kabisa!
Kwamboka ametuacha ameenda kabisa!

Inkanywoma kinde ekegori , omoisia yara
Nkamwancha buna oboke, Onyacha akabora, gwaisanire?
Agancha agaikaransa, ee agaikaransa
Nkamoseria genda! Genda! Genda! Eee nkamoseria pi!
Agantebia oikire, tari kogenda ande pi!

Tafsiri

Nikaaoa nikiwa mdogo, mwanamume ambaye hajakomaa
Nikampenda kama asali, Onyancha akauliza, umekomaa?
Akakubali akakaa, akakaa
Nikamkuza aende! Aende! Aende! Eee nikamfukuza kabisa!
Akaniambia amefika, haende kokote!

4.2.8 Kifo/Tanzia

Kifo ni hatua ya mwisho ya maisha. Baada ya mtu kuaga dunia iwe mtoto au mtu mzima, sherehe kubwa iliandaliwa ili kusherehekea hatua hiyo ya mwisho. Nyimbo mbalimbali pia ziliimbwa ambazo zilitumiwa kuashiria uchungu na uzuni unaotokana na kifo chenyewe, zingine ziliimbwa kukashifu kifo, zingine ziliimbwa ili kummiminia sifa aliyeaga.

Mbinu ya takriri, chuku na mbinu taswira zilitumiwa kwa ufanifu mkubwa katika kuonyesha athari ya vifo kwa jamii hii. Chuku ilitumiwa katika kuonyesha jinsi ambavyo vifo vilikuwa vimeongezeka kinyume na ilivyokuwa awali. Wimbo huu ulidhihirisha jinsi ambavyo wanajamii walilemewa na kifo. Kwani vifo vilitokea kila kuchao. Mzee Maoga alieleza kuwa walipoimba kuwa kifo kilikuwa kinapitia kwenye milango, dirisha na hata kwenye paa ilileta dhana ya kuwa vifo vya wanajamii vilizidi kuongezeka jambo ambalo liliwakera sana kwa sababu watoto waliachwa mayatima na wazazi waliwapoteza watoto wao wachanga. Maudhui haya yalidhihirika ifuatavyo:

Makweri aeteire emerango
Makweri aeteire chitirisa
Makweri aeteire ebirama
Akoira abanto ebitongo

Tafsiri

Kifo kimepitia kwa milango
Kifo kimepitia kwa dirisha
Kifo kimepitia kwa paa
Kinapeleka watu pabaya

Makweri tamanyeti omogaka
Makweri tamanyeti omong'ina
Makweri tamanyeti abana
Akoira abanto ebitongo

Tafsiri

Kifo hakitambui mzee
Kifo hakitambui mama
Kifo hakitambui watoto
Kinapeleka watu pabaya

Hali kadhalika, mbinu ya taswira hisi ilitumiwa katika beti hizi ili kuonyesha hisia zao za huzuni zilitotokana na vifo vya wapendwa wao. Mbali na hayo mbinu tashihishi na mbinu ya takriri ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo asilimia ya watu waliokuwa wakiaga dunia ilivyoongezeka ilikilinganishwa na awali. Mzee Nyakweba alieleza kuwa vifo vya watoto wachanga au vijana vilipotokea wanajamii waliomboleza zaidi ikilinganishwa na mtu mkongwe. Sababu kuu ya kuomboleza vifo vya watoto au vijana zaidi ni kwa kuwa hao ndio walitegemewa kuendeleza ukoo wao na jamii kwa jumla, hivyo basi kuaga kwao kulilinganishwa na taa kuzimika au ukoo kukosa mwelekeo kwa sababu hakuna mtu angeuendeleza. Pia waliamini kuwa mtoto au kijana hakustahili kufa kabla ya mzazi wake kwa sababu mzazi alikuwa ameishi kwa miaka mingi na kujionea mengi hivyo mtoto au kijana akiaga dunia ilikuwa sawa na kumnyima mtoto au kijana huyo nafasi ya kukua. Kando na hayo kifo kilichukua akina mama na akina baba, kwa hivyo watoto wengi waliishia kuachwa mayatima na wapweke hasa baada ya wazazi wao kufariki. Jambo lingine ni kuwa, kifo hakikuwa kinatambua jinsia. Watu wa jinsia zote wanaaga dunia.

Kulingana na Onyancha ni kuwa watu kwenye jamii waligawika katika matabaka mbalimbali. Kulikuwa na tabaka la juu, tabaka la kati na tabaka la chini. Watu hawa mara nyingi hawakutangamana kwa sababu ya tofauti zao. Watu wa tabaka la chini walihisi kuwa wamebaguliwa na watu wa tabaka la juu. Pia kuna tofauti zilizotokea

kati ya watu wenye mamlaka(viongozi) na watu wa kawaida(wananchi). Ila katika ubeti huu ni wazi kuwa katika kifo hakuna ubaguzi. Matajiri kwa maskini, viongozi kwa wananchi wote walikuwa kwenye chombo kimoja. Baadhi ya wanajamii walisema kuwa kama mwanadamu angekuwa na uwezo wa kuzuia kifo kwa kutumia pesa, matairi kwenye jamii hiyo wangetumia utajiri wao ili kuzuia kifo. Katika kufanikisha maudhui haya, mtunzi alitumia mbinu ya tanakuzi katika kuonyesha watu ambao walikuwa wanaaga dunia. Mtunzi alisema kuwa watu maskini kwa Tajiri na viongozi kwa raia wote waliaga dunia. Hii ilitumiwa kuonyesha kuwa katika kifo hakukuwa na ubaguzi wowote. Maudhui haya yanadhihirika ifuatavyo:

Makweri tamanyeti omotaka
Makweri tamanyeti omonda
Makweri tamanyeti omorai
Akoira abanto ebitongo

Tafsiri

Kifo hakitambui maskini
Kifo hakitambui tajiri
Kifo hakitambui kiongozi
Kinapeleka watu pabaya

Ubeti huu uliashiria jinsi ambavyo wanajamii walikuwa na huzuni kutokana na kifo. Katika kuendeleza maudhui haya ya tanzia, mtunzi alitumia mbinu ya kinaya katika kuwafaraji na kuendelea na maisha. Alisema kuwa haina haja ya wao kulia kwa sababu mtoto wao amekufa na pia kilio chao hakiwezi mrejesha na mwisho mwisho kabisa ni kuwa kifo kimekuwao tangu awali hivyo basi walipaswa kukiridhia. Kulingana na maelezo ya Mayaka ni kuwa katika kifo bado taasubi ya kiume ilidhihirika kwani watu wa jinsia ya kike ndio waliofarijiwa katika wimbo huu. Hii ni kwa sababu wanajamii waliamini kuwa hisia za wanaume hazikustahili kuonekana. Wanawake pekee ndio walikua nafasi ya kulia na hata kudhihirisha hisia zao kwa

sababu ya kifo. Ila mwanamke huyu ambaye alimpoteza mtoto wake alikumbushwa kuwa hata akilia vipi au ahuzunike vipi hawezi akabadilisha jambo lolote lile. Aliambiwa kuwa huzuni au uchungu huwezi ukamuua kwani kama ungekuwa na uwezo wa kuua ungekuwa umeua wengi. Mzazi huyu alikumbushwa kuwa kifo ambacho kilimkumba hakikuanza juzi, kutoka zamani watu walikuwa wakifa na mtoto wake hakuwa wa mwisho kuaga dunia. Jamii ya Wakisii ni wakristo ambao walizingatia mafunzo ya Biblia, kulingana na Biblia ni kuwa kifo cha kwanza kilikuwa cha Habili mtoto wake Adamu na Hawa aliyeuliwa na Kaini. Hivyo mzazi huyo alihimizwa ajipe moyo kwani yangepita. Mbinu ya takriri na mbinu ya taswira ilitumiwa kuonyesha huzuni ambao ulitokana na kifo. Waliofiwa walikumbushwa kuwa kifo kilianza kitambo ila ilikuwa vigumu kwao kuiridhia hali hiyo.

Baba ng'ina Kwamboka notana korera okure
Baba ng'ina Kwamboka notana korera ee ochire
Bororo mbori goita, kanga bwaitire abange
Bororo mbori goita, kanga bwaitire abange
Makweri namakoro, notana korera baba
Makweri namakoro, notana korera baba

Tafsiri

Mama ya Kwamboka, haina haja ya kulia
Mama ya Kwamboka, haina haja ya kulia
Uchungu huwezi kukuua, ungekuwa umeua wengi
Uchungu huwezi kukuua, ungekuwa umeua wengi
Kifo ni cha kale haina haja ya kulia
Kifo ni cha kale haina haja ya kulia

4.3.0 Maudhui Katika Nyimbo za Jadi za Jamii ya Waswahili

Kupitia kwa nyimbo za jadi za jamii hii, maudhui mbalimbali yameibuliwa ambayo yamesaidia kuendeleza nyimbo hizi. Maudhui haya ni kama vile: ndoa, kifo/tanzia, malezi, uwajibikaji, nafasi ya mwanamke katika jamii, dini, mabadiliko na nafasi ya vijana katika jamii.

4.3.1 Ndoa

Kulingana na Harrison na Michelson (2019), anafafanua ndoa kama muungano kati ya mwanamume na mwanamke mmoja au zaidi ambao wana haki ya kimapenzi. Taasisi ya ndoa ni takatifu. Waliichukulia ndoa kama baraka kutoka kwa Mungu. Kutokana na kuihusisha ndoa na Mungu wanandoa walistahili kuiheshimu. Wanandoa walipaswa kuwa waaminifu kwa wenzao. Tabia ya kuwa na jicho la nje ilikuwa ni mwiko kwa sababu ingepelekea kulaaniwa.

Katika wimbo wa *Leo ni Leo* na *Shangwe Vigelegele*, mbinu ya jazanda ilitumiwa na watunzi katika kusesitiza thamani ya ndoa. Pia mbinu hii ilitumiwa kuwakumbusha kuwa walikuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa ndoa imedumu milele. Kutoa talaka kulirejelewa kama kufuru. Mzee kombo alieleza kuwa Ingawa ndoa ilikuwa na changamoto nyingi sana walikumbushwa wawe wavumilivu. Hulka yao ya uvumilivu ingewasaidia kukabiliana na shida zote na kuifanya ndoa yao inawiri. Ndoa ilichukuliwa kama pingu za maisha. Neno pingu lilitumiwa kijazanda kumaanisha kuwa baada ya wao kuungansishwa hawapaswi kufikiria kuhusu talaka. Ndoa yao ilipaswa kudumu miliele na milele kwani kifo ndicho kinastahili kuwatenganisha. Kisengere nyuma pia kilitumiwa katika kufanikisha maudhui haya kwani wanandoa hasa walikumbuka yale waliyofunzwa walipokuwa wakiandaliwa kwa ajili ya ndoa. Beti zifuatazo zinadhihirisha maudhui ya ndoa ifuatavyo:

Kwetu talaka kuitoa ni kufukuru

Nimefunzwa nivumilie mshinde ujana

Ili kesho kusudi mahususi wasionong'one

Bw. na Bi.arusi wamefunga pingu za maisha

Bw. na Bi.arusi wamefunga pingu za maisha

Katika wimbo wa Shangwe Vigelegele, mbinu ya taswira hisi ilitumiwa katika kukuza maudhui ya ndoa. Wanandoa waliambiwa kuwa lazima wawe na mapenzi ya dhati baina yo ili ndoa yao ifanikiwe. Hali kadhalika, walikumbushwa kuwa kuna baadhi ya wanajamii ambao walikuwa na gere hivyo basi hakupaswa kuwapa nafasi. Mzee Bakari alisisitiza yahoo kwa kwa kueleza kuwa wanandoa walishauriwa kuwa wawe makini sana kwani si kila mtu aliyefurahia ndoa yao. Jamii ilijaa mahasidi ambao wangejaribu juu chini ili kusambaratisha ndoa hiyo. Hivyo basi walitarajiwa kuilinda na kuikinga kwa hali na mali. Walikumbushwa kuwa wamefunga pingu za maisha hivyo hawakupaswa kufikiria kuhusu talaka. Mbinu ya takriri ilitumiwa pia kuisitiza umuhimu wa kuitunza na kuilinda ndoa hiyo kwa lolote lile. Hali hii inadhihirika ifuatavyo:

Mapenzi yawe daima yasiingiliwe na mtu
Mapenzi yawe daima yasiingiliwe na mtu
Wataomba muachane ili waanze kuwacheka
Msiachane ili nyoyo zao ziwaume watoke patupu

Siku ya harusi, mwanamke aliimbiwa nyimbo nyingi ambazo zilitumiwa kama nasaha kwake hasa kwa maisha ya ndoa. Katika wimbo wa Leo ni Leo msichana alilelekwza kwa mengi. Ili kufanikisha ujumbe huo, mtunzi alitumia mbinu ta taswira uoni katika kuisitiza umuhimu wa kuwa safi ili kumvutia mume wake. Bi. Hadija alieleza kuwa msichana alipokaribia kuolewa alikuwa anapokea mafunzo ya jinsi ya kuitunza ndoa kutoka kwa wanawake wengine wakongwe, walio na tajriba kuhusu ndoa au walioheshimiwa katika jamii. Alikumbushwa kuwa jukumu la kuijenga au kuibomoa ndoa lilikuwa lake mwenyewe. Alifunzwa umuhimu wa kudumisha usafi wa mwili na wa nyumbani. Alistahili kuvalia kanga safi, ajirashie marashi yaliyonukia na ajifunge kanga ambazo zingemfanya apendeze machoni mwa mume wake. Iliaminiwa kuwa

ikiwa angevutia kila wakati, mume wake hangepata ari ya kutafuta wanawake wengine. Maudhui haya yalidhihirika ifutavyo:

Mwanamke lazima awe safi
Kanga alisugue
Mume akirudi sharti viatu kumvua

Kitandani rashia marashi
Kumkanda kisha kumchua
Kisha anza sayansi kiuno kutengua

Mambo ya kuzima si mahaba
Kuzima ta ani kuwanga
Washa mshuma unaonukia
Angalau mumeo aone shanga

Mwanamume pia alifunzwa na wazee kuhusu kutia bidii kazini ili aweze kukidhi mahitaji ya watoto wake na mke wake. Iliaminiwa kuwa mwanamume akishindwa kukidhi mahitaji ya familia yake mke wake angemdharau hata kuchangia mwanamke huyo kuwa na jicho la nje. Kuomba watu vitu kama vile vyakula ilikuwa ni mwiko, mbinu ya jazanda ndio ilitumiwa kufanikisha mafunzo haya. Mwanamume alisisitiziwa umuhimu wa kujitegemea. Asiwe ombaomba kamwe.

Ahsante mama ulinifunza nkajaua
Baba akasema kuomba ni mwiko
Raha ya chumvi ni kununua

4.3.2 Kifo/Tanzia

Maudhui makuu katika wimbo wa *Ooh Kifo* ni kifo au tanzia ambapo mtunzi alitumia mbinu ya tashihisi katika kuonyesha athari za kifo. Ambapo anasema kuwa ‘kifo kinachukua wazazi weto, kifo chakamia boma zetu’. Hali kadhalika, maswali ya balagha yalitumiwa ili kuonyesha hisia za huzuni zilizotokana na kifo hicho. Mzee Mkombozi alieleza kuwa, kifo kilikuwa kama adui mkubwa wa binadamu. Kila mara

kilipotokea kilitonesha jeraha la kifo kilichotangulia. Kupitia kwa tanzia, watoto waliachwa mayatima hawakuwa na mlezi au mtu wa kukimu mahitaji yao ya kibinafsi. Kifo kilisababisha wanaume kwa wanawake, vijana kwa wazee na raia kwa viongozi kuwa na huzuni mwingi. Walijiuliza ni wapi ambapo wangeweza kujificha ili waepuke kifo. Ila walijijibu wao wenyewe kuwa hawangeweza kujificha popote kwa sababu kifo chenye kiliwasaka kote. Maudhui haya yaliendelezwa ifuatavyo:

Kifo chakamia boma zetu
Kifo kinachukua wazazi wetu
Kinatuacha mayatima tu
Je, tutawezana vipi na kifo

Ooh kifo, mbona watutesa hivi?
Ooh kifo, ni lini utatuchia?
Ooh kifo, hata tujifiche wee
Ooh kifo unatusanya kote kote

Watu wengi baada ya kupoteza wapendwa wao walitamauka maishani. Katika wimbo wa *Kwaheri*, mbinu ya tashihisi ya tashihisi ilitumiwa kuonyesha hisia zao, waliofiwa walihisi kuwa mazingira hayana mantiki tena maishani mwao. Kutokana na huzuni ambao walishuhudia, wanatumia taswira uoni kuonyesha kuwa hawakuwa na matumaini yoyote. Wengine walihisi kuwa kifo ndicho suluhu kwa maisha yao ambapo walitumia jazanda ya kubisha milango ya mbinguni. Mzee Mkombozi alieleza kuwa wengi walijiuliza maisha yana maana gani. Wazazi walipowapoteza watoto wao walikosa matumaini ya kupata mtoto mwingine. Ingawa walikuwa na watoto wengine ilikuwa wazi kuwa pengo lililoachwa na mwendazake halingeweza kuzibwa na mtoto yeyote kwa sababu kila mtoto alikuwa na upekee wake. Isitoshe, mpenzi alipompoteza mwenzake, aliona giza maishani mwake. Kwa sababu ya upweke alioshuhudia. Wengine waliona ni heri wafe kama wenzao kwa sababu walikosa matumaini maishani. Mtu huyu alipoteza tamaa maishani. Alijiuliza maswali mengi ambayo hayakuwa na majibu. Alihisi kuwa alitembea barabara ndefu ambayo

haina kikomo. Kila kitu kilichomzingira kilipoteza razini, na amepoteza matumaini maishani.

Mwezi umepoteza razini yake
Nahisi kuwa unanichukia
Nimebakia mpweke sina kimbilio

Kiza chaingia kinazidi siwezi ona
Maisha haya hayana maana
Nataka nibishe milango ya mbinguni

4.3.3 Malezi

Kulingana na Gazeti la Sema (2024), malezi ni mchakato wa kumtunza, kumuelekeza, kumuongoza na kumuelimisha mtoto tangu angali tumboni hadi uzeeni. Mchakato huu unahusisha kuhakikisha mahitaji ya mtoto yanakidhiwa, kumfundisha stadi za kazi na maarifa muhimu yatakayosaidia kujenga na kukuza uhusiano mzuri na wanaomzunguka kuanzia ngazi ya familia, shuleni na kwenye jamii. Anaendelea kusema kuwa malezi ni kipande muhimu sana katika maisha ya mtoto. Kila mtoto anahitaji malezi bora ili kuwa na maendeleo kamili ya kiakili, kihisia, kijamii, kiuchumi na kiroho. Malezi sahihi huzaa matunda mazuri, yakimsaidia mtoto kuwa na utu na kuwa raia mwenye maadili mema.

Kwenye jamii, malezi yamekuwa msingi wa kukuza vijana wenye mchango kwa taifa na wale ambao wameharibikiwa. Malezi ni zaidi ya kumpa mtoto shibe na makaripio, ni mchakato unaohitaji kujitolea, upendo, huruma, uvumilivu na uelewa wa kina juu ya mahitaji ya maendeleo na makuzi ya mtoto. Malezi chanya unayompa mtoto angali mdogo ndiyo chanzo cha utu wake wa kesho anapokuwa mtu mzima. Hii inamaanisha kwamba kama mzazi, au mlezi, atakuwa anamlea mtoto katika mazingira ya kikatili inamaanisha hata mtoto atakapokuwa mkubwa atakuwa katili au atakuwa na tabia za kikatili kwa sababu ya Malezi aliyoyapata alipokuwa mdogo.

Katika jamii hii, baada ya watoto kukomaa na kukaribia kuingia katika taaasisi ya ndoa, waliwafundisha vijana wao umuhimu wa kufanya kazi. Hali hii ilidhirika katika wimbo wa Leo ni Leo, ambapo mbinu rejeshi ilitumiwa kuonyesha kuwa wawili hao walipokea mafunzo kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kabla ya siku ya ndoa. Hali kadhalia, mbinu ya jazanda ilitumiwa katika kuwahimiza kufanya kazi kwa bdi kwani kulikuwa na raha ya kula jasho lako mwenyewe. Hali hii ilidhihirika katika mshororo ufuatao, ‘Raha ya chumvi kunua’. Mzee Salim alisema kuwa mwanamume na mwanamke walihimizwa kushirikiana katika kila jambo. Wawili hawa waliposhirikiana iliaminiwa kuwa, wangeweza kukidhi mahitaji ya familia yao. Mwanamume alikumbushwa kuwa iwapo angetaka afurahie maisha yake, aheshimiwe na jamii pamoja na mke wake ilikuwa ni lazima akidhi mahitaji ya familia yake. Asiwe mtegemezi au ombaomba. Waswahili wanasema kuwa “*nguo ya kuazima haisetiri matako*”. Ubeti ufutao unadhihirisha maudhui haya:

Ahsante mama ulinifunza nikajua

Baba akasema kuomba mwiko kununua

Raha ya chumvi ni kununua

Baada ya mtoto kuzaliwa, nyimbo ambazo waliimbiwa katika sherehe hizo zilidhihirisha matarajio ya jamii kwao. Watoto hawa waliambiwa kuwa kufanya kazi ni lazima. Kwa mfano, watoto wa kiume walikumbushwa majukumu yao kama vile uvuvi na kilimo. Katika kazi zao walikumbushwa umuhimu wa kuwa wavumilivu kwa sababu kuna wakati ambapo wangeenda baharini kuvua na waambulie patupu hivyo basi kupitia kwa nyimbo hizo walikumbushwa wasitamauke kwa sababu *mvumilivu hula mbivu*. Watoto hawa walipokua walijua majukumu yao. Mafunzo haya yalifanikiwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile kisengerembele, ambapo jamii ilielezea mtoto huyo kuhusu majukumu ambayo yalikuwa yakimsubiri, pia

mbinu ya methali ilitumiwa hasa kuwahimiza wazazi na wanajamii wasiwe na pupa ya kuwasukuma watoto kuanza kufanya kazi. Hali hiyo inadhihirika ifuatavyo:

Naingoja siku ambayo utakuwa dume
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavua, ulete dagaa
Ila itabidi tuwe wavumilivu
Kwani mvumilivu hula mbivu
Kwa sababu wewe ni kitoto kibichi tutavumilia

Wazazi pia hasa akina mama walimpa mtoto funzo la kwanza la maisha punde tu baada ya kuzaliwa. Mtoto huyo alilambishwa shubiri kisha anapewa asali. Shubiri ilitumiwa kumbukumbusha mtoto huyo kuwa maishani angekabiliana na changamoto nyingi sana kama magonjwa, kukosa kazi, migogoro na kadhalika, ila jambo la muhimu ni kuwa alistahili kutumia mbinu mwafaka kukabiliana nazo. Kando na hayo alipewa asali ambayo ilikuwa na lengo la kumwambia kuwa wakati mwingine angeshuhudia au angekuwa na siku za raha. Mtoto huyo alipaswa kufurahia siku hizo za raha pia. Asali na shubiri katika ubeti zilitumiwa kijaznda. Hali kadhalika, kule kumpa mtoto arambe ilikuwa ni mbinu ya taswira muonjo. Taswira hisi pia ilitumiwa kuonyesha shida ambazo angekumbana nazo na furaha ambayo ingetokana na mambo mazuri ambayo yalitokana na kufanikiwa kwake. Kwa mfano:

*Mwanangu usiyapapie maisha
Tulikupa asali na shubiri
Kumbuka utakuwa na siku za huzuni
Ila siku hizo zitapita
Siku za furaha zikifika zifurahie
Zisherehekee mwanangu*

Mtoto wa kiume alikumbushwa kuwa mwadilifu na mnyenyekevu kwa sababu yeye ndiye mwakilishi wa familia yao. Katika wimbo wa *Allah Akulinde*, mbinu ya tashbihi

ilitumiwa kumshauri mvulana kuhusu maisha ya ndoa, anaambiwa kuwa amuo mwanamke atakayemuenzi kama mboni ya jicho lake. Hali kadhalika, mbinu ya kisengere mbele ilitumiwa kumkumbusha mvulana huyu kuhusu matarajio ya jamii kwake na jinsi alivyostahili kuishi. Mzee Abdi alisema kuwa mvulana huyu alikumbushwa kuwa akiingia katika ndoa, yeye ndiye angekuwa kichwa cha familia yake. Jamii iliamini kuwa lazima mtu adumishe maadili kila wakati. Mtu yeyote ambaye alikuwa mwadilifu aliheshimiwa na watu wote wakiwemo wazee na viongozi. Alihimizwa kutowabagua watu kwa misingi yoyote ile kwa sababu dini yao ilihimiza watu kupendana. Mtoto huyu alishauriwa kuwa wakati ambapo alipokomaa alistahili kumuoa mwanamke ambaye angempenda na kumuenzi kama mboni ya jicho lake. Hili lingepelekea kijana huyu kuishi maisha ya raha na starehe. Iliaminiwa kuwa bila mapenzi ya dhati kwenye ndoa, maisha yake yangekuwa na huzuni na angejipata akiwa na jicho la nje. Mbali na hayo, wazazi pia walimuonya mtoto wao dhidi ya kuwa na tamaa ya mali. Kutokana na tamaa ya mali angejiingiza katika hali ngumu ambayo ingeweza kuhatarisha maisha yake. Walisisitiza kuwa ni vyema aridhika na kile kidogo ambacho angepata. Kupitia kwa ubeti ufatao, maudhui haya yalidhihirika:

Kuwa mwanamume mnyenyekevu
Mwanamume mwenye maadili
Usimbague yeyote
Nakuombea umapte mwanamke
Mwanamke atakayekuenzi kama
Mboni la jicho lako
Usiwe mwenye tamaa ya mali
Ridhika na vichache vyako
Nakuomba uzingatie haya kwa ajili yangu

4.3.4 Uwajibikaji

Kulingana na TUKI (2019), kuwajibika ni hali ya kulazimika kutekeleza jambo. Wazazi au walezi waliwajibika walipowaongoza na kuwaelekeza watoto wao jinsi ya kukabiliana na maisha ya ndoa. Waliwasisitiza watoto wao umuhimu wa kula na kufurahia jasho lao. Hili lingetimizwa tu kupitia kwa bidii yao. Walikumbushwa raha

ya maisha ni kujitegemea wenyewe hasa kupitia kwa bidii yake mwenyewe. Waliambiwa kuwa wakiwa wategemezi au ombaomba hawangefurahia maisha yao. Kupitia kwa kisengere nyuma, wanandoa walidhihirisha jinsi ambavyo wazazi wao waliwajibika katika kuwaelekeza kuhusu maisha na pia wazazi hao kuwafunza kuhusu umuhimu wa kuwajibika maishani mwao. Kwa mfano:

Ahsante mama, ulinifunza nikajua
Baba kasema kuomba ni mwiko
Raha ya chumvi ni kununua

Mbinu ya chuku ilitumiwa katika kujenga maudhui ya uwajibikaji katika ndoa. Kwani waliambiwa kuwa wapendane hadi kifo, hivyo kila mtu alikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa ndoa hiyo imefanikiwa. Hali adhalika walisitiziwa kuwa wasimruhusu mtu yeyote aingilie ndoa yao kwa sababu kitendo hicho kingehatarisha ndoa yao. Hivyo walipaswa kuikinga kwa njia zote. Wanandoa walikumbushwa kuwa ili ndoa yao ifanikiwe ilikuwa lazima wawajibike na watie bidii katika kuilinda na kuikinga kutoka kwa mahasidi. Mzee Salim alisema kuwa jamii iliamini kuwa baada ya mtu kuingia kwenye ndoa kifo ndicho kingestahili kuwatenganisha. Mwanamke alistahili kutekeleza majukumu yake ambayo yangepiga jeki ndoa yao kama vile: kupika, kumsinga mume wake, kudumisha usafi nyumbani na kadhalika. Iwapo angewajibikia kazi hizi, mume wake hatakuwa na jicho la nje kwa sababu atakuwa amemtoshela. Kwa upande mwingine, mwanamume alipewa changamoto kubwa ambayo ni kuiongoza familia yake. Aliambiwa kuwa lazima akidhi mahitaji ya familia yake na pia aiongoze kwa misingi ya kidini kwani akishindwa kutekeleza majukumu haya hakuna mtu ambaye angemheshimu. Hivyo ilikuwa wazi kuwa wanandoa walikuwa na wajibu wa kuijenga au kuibomoa ndoa yao. Ubeti ufuatao unadhihirisha yafuatayo:

Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kingewatenga
Mapenzi yawe daima yasiingiliwe na mtu
Wataomba muachane ili waanze kuwacheka
Leo mnaanza maisha nendeni mkaishi salama

Katika sherehe za kuzaliwa kwa mtoto has awa kiume, kulikuwa na nyimbo mahususi ambazo waliimbiwa. Kwa mfano, wimbo wa *Siku Njema* mbinu ya jazanda ilitumiwa katika kumfunza mtoto huyo uwajibikaji. Mtoto huyo aliambiwa kuwa 'Naingoja siku ambayo utakuwa dume'. Kule kukuwa dume kuliashiria kuwa kijana mwenye nguvu na baada ya hapo kijana huyo alitarajiwa kuenda baharini kuvua kwa sababu hili likikuwa jukumu la wanaume. Mama Fadhili alieleza kuwa wakunga na akina mama wazee ambao walichukuliwa kuwa wenye busara walidhihirisha uwajibikaji katika malezi kwa kuwaelekeza watoto wachanga kuhusu majukumu yaliyowasubiri. Pia waliwaelezea kuhusu matarajio ya jamii kwa hasa watoto wa kime. Wavulan walikumbushwa kuwa jukumu la kuenda kuvua lilikuwa lao. Hivyo basi walitarajiwa kujifunzastadi za kuvua walipoendelea kukua. Maudhui haya ya uwajibikaji yalidhihirika ifuatavyo:

Naingoja siku ambayo utakuwa dume
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavue ulete dagaa
Ila itabidi tuwe wavumilivu

Mzee Hamisi alisema kuwa kazi ya uvuvi ilitengewa wanaume na ilifanywa wakati wa usiku. Ingawa walipitia changamoto nyingi bahaini kama vile mawimbi makali, kuvamiwa na wahuni na wanyama, baridi na mvua na wakati mwingine kukosa kunasa samaki, walihimizwa wasitamauke bali wawe wavumilivu na Jasiri kwa sababu familia ilitegemea kupata kitoweo kutoka kwao. Walikumbushwa kuwa bila wao kujikaza baharini, familia zao zingeangamia kwa sababu ya njaa. Ubeti ufuatao unaweka maudhui haya wazi:

Usiku huu twaenda kuvua
Usiwe na woga wowote
Dume lazima awe jasiri
Familia yangoja pweza
La sivyo watalala njaa

Katika kujenga maudhui haya, taswira sikivu ilitumiwa kupitia kwa kuwika kwa jogoo ambaye alikuwa akiwaamsha. Pia ili kuepuka joto la mchana, walitarajiwa kufika shambani mapema sana walime ili wamalize kabla ya viwango vya joto kupanda. Hali kadhalika, taswira uoni ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo minazi ilinawiri hivyo walipaswa kuenda kuivuna ili itumiwe katika kuandaa wali wa nazi. Mzee Abdi alisema kuwa jukumu linguine muhimu la wanaume lilikuwa ni kuvuna minazi. Jukumu la kupanda juu ya mti huo lilitengewa watoto wavulana, vijana na wanaume wa makamo, minazi hii hii ilikuwa muhimu sana kwa sababu walitumia maji ya nazi kuandaa wali. Wanaume pia walidhihirisha uwajibikaji walipohamasishana waende shambani wakalime. Wao walitarajiwa kuamka asubuhi na mapema kuenda shambani ili wamalize mapema kabla ya jua kuwa kali na viwango vya joto kupanda. Viwango vya joto vikiwa juu wangeshindwa kukaa shambani. Kwa upande mwingine, wanawake walisalia nyumbani ili kufanya kazi zote za nyumbani kama vile: kupika, kuosha vyombo na kudumisha usafi wa jumla kwa boma. Ubeti ufatao unadhihirisha majumu ya mwanamume:

Kumekucha jogoo tayari amewika
Tuende shambani tukalime
Kabla ya jua kuzidi
Tuende tukapalilie mahindi

Minazi nayo imekoma uwanjani
Yahitaji kuvunwa
Tutakulaje wali
Wali bila nazi
Kumbuka wewe ni mwanamume
Na hivyo mkono mtupu haurambwi

Katika wimbo wa *Jenga Kiota*, taswira uoni ilitumiwa ili kuwaambia wanajamii kuwa werevu kama njiwa kwa kujenga kiota. Hali kadhalika, kule kujenga kiota ilitumiwa kijazanda kwa kuwasisitizia watu watie bidii kazini. Kile kiota cha kujikinga wakati wa mvua ni vitu ambavyo vingewafaa wakati wa shida. Mwisho kabisa, mbinu ya takriri ilitumiwa ili kususitiza watu wafanye kazi. Mzee Kombo alieleza kuwa wimbo huu ulielekezwa kwa watu ambao ni wavivu. Walikumbushwa umuhimu wa kuwajibika na kutia bidii katika kazi yoyote ile waliyoifanya. Walihimizwa wafanye kazi kwa bidii kwani wangepata matunda ambayo yangewafaa wakati wa shida. Watu hao walikumbushwa kuwa walistahili kuwa kama njiwa ambaye hujenga kiota chake wakati wa jua, mvua inaponyesha anajikinga mle ndani. Binadamu alikumbushwa kufanya kazi kwa sababu ana nguvu na afya nzuri kwa sababu chochote kile angevuna alistahili kukihifadhi vizuri ili kimfae siku za usoni.

Njiwa mwerevu hujenga
Hujenga kiota chake kizuri
Ili mvua inaponyesha anajiknga

Naomba muige njiwa mwerevu
Jenga nyumba, wakati wa mvua mjikinge

Toka kitandani asubuhi na mapema
Usingizi ni wa watoto wachanga
Fanya kazi yako
Fanya kazi yako

4.3.4 Nafasi ya Mwanamke kwenye Jamii

Katika jamii hii mwanamke alipewa nafasi mbalimbali hasa katika ndoa na katika malezi kwa sababu aliaminiwa kuwa alikuwa na busara ya kufanikisha taasisi hizi mbili muhimu kwenye jamii. Mwanamke alichorwa kama pambo hasa kwenye jamii ya Waswahili. Kupitia kwa taswira uoni mambo ambayo mwanamke alistahili kufanya ili kuongeza ladha kwenye ndoa yake yalidhihirishwa. Alistahili kujiremba

na kujipamba kila wakati kwa kutumia mapambo kama vile hina ambayo ilipakwa miguuni na mikononi, shanga iliyovaliwa kiunoni, herini, bangili, kikuuu na marashi. Mapambo haya yote yalikuwa na lengo la kumfurahisha mwanamume. Mwanamke huyo alistahili kuvutia machoni mwa mume wake ili asivutiwe na wanawake wengine jambo ambalo lingeweza kupelekea mwanamke huyo kupewa talaka. Hivyo basi msichana alipotayarishwa kwa ajili ya ndoa na hata siku ya ndoa yenywe alikumbushwa umuhimu wa kuwa safi na kujipamba kila wakati. Hali hii ilidhihirika katika ubeti ufuatao:

Mwanamke lazima uwe safi
Kanga ulisugue
Mume wako akirudi sharti
Viatu kumvua
Kitandani rashia marashi
Kumkanda na kumchua

Mwanamke alitarajiwa akiingia kwenye ndoa awe ni mwenye mapenzi ya dhati kwa mume wake. Kupitia kwa jazanda, waliambiwa kuwa ndoa ni pingu za maisha, kwani hakukuwa na nafasi ya kutoka baada ya kuingia pale. Wanajamii walimhimiza kuwa ajaribu juu chini ili ndoa yake ifanikiwe. Akiwa katika ndoa alistahili kuvumilia hali yoyote ngumu ambayo ingemkabili pia alikumbushwa kumpenda mume wake kwa hali yoyote iwe njema au mbaya.

Bw. na Bi. arusi wamefunga pingu za maisha
Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kitawatenga

Mwanamke ni mlezi mwema. Bi. Mwanaisha alisema kuwa, mwanamke alipewa nafasi ya kumwelekeza mtoto kuhusu maisha punde tu alipozaliwa. Kupitia kwa mbinu ya jazanda kwenye nyimbo za kuzaliwa kwa watoto, wanawake walifanikiwa kuwafunza watoto wachanga kuhusu maisha yaliyowasubiri. Waliwaambiwa watoto kuhusu tamu na chungu ya maisha. Kumfunza mtoto huyu mambo haya mapema yalimwandaa kisaikolojia na pia kumsaidia kuibua mbinu-ishi za kukabiliana na hali

mbalimbali ambazo angekumbana nazo. Kupitia kwa wimbo huu, mtoto huyo alihimzwa kuwa mtu mnyenyekevu ambaye angewaheshimu watu wote bila kutumia vigezo vyovyote vile. Hali kadhalika, walimwambia mtoto huyo awe mwenye maadili mema. Alistahili kuongozwa na sheria za dini pamoja na sheria za nchi. Walimfunza mtoto huyu kutafuta mali kwa njia ambayo ni halali. Asitawalwe na tamaa ambayo ingeweza kumpeleka mahali ambapo ni pabaya.

Tulikupa asali na shubiri
Kumbuka utakuwa na siku za huzuni
Ila siku hizo zitapita
Siku za furaha zikifika zifurahie
Zisherehekee mwanangu

Kuwa mwanamume mnyenyekevu
Mwanamume mwenye maadili
Usimbague yoyote

Nyimbo hizo pia zilimsawiri mwanamke kama mtu ambaye ni mwenye matumaini. Alikuwa na matumaini kuwa mvulana huyo akikomaa angekuwa mtu ambaye ni mwajibikaji katika jamii. Alitarajiwa kuwa angechangia katika kuikimu familia yake kwa njia mbalimbali kama vile kuenda baharini ili kuvua samaki, kuenda shambani kulima na pia kuikinga familia yake kutokana na hatari yoyote ile. Katika nyimbo hizi, wanawake walitumia mbinu ya taswira uoni katika kuonyesha kazi ambazo walitarajiwa kufanya na pia kisengere mbele ambacho kilitumiwa kuwaambia watoto hao kuhusu kazi ambazo wangepanya.

Naingoja siku ambayo utakuwa dume
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavue ulete dagaa
Ila itabidi tuwe wavumilifu

Kupitia kwa nyimbo za jadi mwanamke alichorwa kama kiumbe ambaye ni mvumilivu. Kulingana Schnitker (2012), anasema kuwa uvumiivu ni hulka na mwenendo wa kusubiri kitu kwa utulivu katika hali ya kukatisha tamaa au katika

dhiki. Uvumilivu ni sifa ambayo inashikiliwa na wengi kama sifa yenye mvuto ya mtu ambayo inachangia katika binadamu kufanikiwa na kuwa katika hali njema. Kwa mujibu wa Worthen (2018), uvumilivu ni muhimu sana katika kukua na kupigwa msasa kimaadili. Anaendelea kusema kuwa uvumilivu ni msingi mkuu katika mabadiliko ambayo binaadamu hushuhudia maishani mwake. Mwanamke alidhihirisha uvumilivu hasa alipokuwa na zingizi la uzazi. Kulingana na TUKI (2019), wanaeleza zingizi kama maumivu ambayo mwanamke hupata baada ya kujifungua. Ingawa mwanamke alipitia maumivu hayo baada ya kujifungua salama alichukua muda kumkaribisha na kusherehekea mtoto wake. Mwanamke alipomwona mtoto wake akiwa na siha na afya nzuri ilimbidi avumilie maumivu hayo kusudi tu ambebe mtoto wake na kumwonyesha furaha yake. Hali kadhalika, mtoto wa kiume alipozaliwa akina mama walimwambia kuhusu matarajio yao kwake. Ila mtoto huyo hangeweza kutekeleza majukumu hayo punde tu alipozaliwa. Walimwambia kuwa ingebidi wawe wavumilivu, wampe muda akue na kujifunza jinsi ya kutekeleza majumu hayo. Wanawake hawa walikiri kuwa hawangemshinikiza au hawangemlazimisha mtoto huyo afanye kazi zozote zile kama hajatimiza umri uliostahili. Mbinu kubwa ambayo ilitumiwa katika kumjenga mwanamke katika ubeti huu ni taswira hisi. Ambapo mwanamke alikuwa na uchungu kutokana na zingizi la uzazi ila alimsherehekea mtoto wake. Hali kadhalika, mwanamke alipaswa kujifunza uvumilivu ili ampe mtoto nafasi ajifunze kazi mbalimbali kisha azitekeleze kwa muda au wakati uliofaa.

Mvulana wangu mtanashati
Ingawa bado nina zingizi la uzazi
Zingizi hilo lafanya nitabasamu bila kikomo

Naingoja siku ambayo utakuwa dume
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavue ulete dagaa
Ila itabidi tuwe wavumilivu

Kwani mvumilivu hula mbivu
Kwa kuwa wewe ni kitoto kibichi

Mwanamke alisawiriwa kama mtu aliyependa kuongea sana. Kulingana na Gazeti la Mwananchi (2021), wanaeleza kuwa kutokana na utafiti uliofanywa, ulionyesha kuwa wanawake kawaida huongea maneno 45,000 hadi 50,000 kwa siku na mwanamume huongea maneno 15,000. Wanaendelea kueleza kuwa uzungumzaji wa maneno mengi umekuwa dawa kwa wanawake kwa sababu takwimu zinaonyesha kuwa wanaoongoza kujiua ni wanaume, huku sababu kuu ya kujinusuru na na hilo kwa wanawake ni kuzungumza, kulalamika na kujadili masuala yao wakiwa peke yao. Sababu kuu inayowazuia wanaume kuongea ni mila na desturi. Kidegesturi, wao ndio wenye uamuzi, wanaoonekana kukubaliwa na familia zaidi kuliko wanawake, hivyo ikitokea akalalamika ataonekana hafai. Jambo ambalo hawataki liwatokee.

Utafiti huo ulidhibitishwa na wimbo wa jandoni. Pale jandoni, wavulana walipokea mafunzo mengi sana. Walikuwa wanaambiwa kuhusu mambo ambayo walistahili kuyafanya na mambo ambayo pia walistahili kuyaepuka. Mafunzo hayo pia yalidhihirika kupitia kwa nyimbo za jandoni. Mvulana alionywa dhidi ya kusema sana. Kusema kwingi kuliambiwa kuwa ni sifa ya wanawake. Waliambiwa kuwa ikiwa wangeona chochote au walifahamu chochote walistahili kunyamaza. Kwa sababu angeweza kusababisha mgogoro kati ya watu wawili ambao hukustahili kuwa. Kwa mfano angeweza kumuona mwanamume akipita na mwanamke ambaye si bibi yake halali kisha akaulizwa kama amemwona mwanamume huyo, kijana huyo akawa na haraka ya kujibu swali hilo. Jibu hilo lake lingeweza kusababisha kuvunjika kwa ndoa ingawa hali hiyo ingezuiliwa ikiwa angenyamaza. Kwa jumla asilimia kubwa ya wanaume huwa hawasemi sana kwa sababu mila na desturi zimewakanya. Katika ubeti huu, taswira sikivu ilitumiwa kumsawiri mwanamke kama mtu mwenye kusema

sana ilhali kwa upande mwingine mwanamume alisawiriwa kama mtu asiaye na maneno mengi.

Kusema kwingi achia wanawake
Usiwe na haraka ya kutangaza bila hakika
Eti wakati mwingine yule kapita yule
Hayo si yako zoea kufyata ulimi
Utavunja ndoa utavunja ndoa usipofyata

4.3.5 Dini

Wataalam mbalimbali wameeleza maana ya dini. Kulingana na Martineau (1843), anasema kuwa dini ni hali ya kuwa na imani kwa Mungu. Anaendelea kueleza kuwa dini ni taasisi muhimu sana kwa maisha ya binadamu. Hii pia ni mojawapo ya taasisi kongwe katika jamii. Tangu kitambo, dini imekuwa ikiathiri maisha ya binadamu katika jamii ya jadi na jamii ya kisasa. Kila pembe ya maisha ya binadamu ina chembe cha dini ndani yake. Naye Rizvi (2004), anasema kuwa neno dini ni neno la asili ya Kiarabu ambalo ni Diin (dini) ambalo lina maana mbalimbali. Kwanza, neno hilo linamaanisha Uislamu; ambapo ni imani ya umoja wa Mwenyezi Mungu. Maana ya pili ni Hukumu; ambapo linarejelea thawabu au adhabu na maana ya tatu ni Desturi; ambalo lina maana ya tabia au mazoea. Hivyo kutakana na Rizvi maana ya jumla ni kuwa mwanadamu kwa silka zake za asili hana budi kuwa na mpango wa maisha wenye msingi wa fikra za kiroho au fikara zile tuziitazo imani. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, dini ni imani kwa Mungu. Ni hali ya kuamini kiumbe mwenye ana nguvu na uwezo zaidi kuliko binadamu.

Katika jamii ya Waswahili dini ni sehemu muhimu sana katika maisha yao ya kila siku. Kuna wale ambao walikuwa ni Wakristo na wengine walikuwa ni Waislamu ila wote walimwamini Mungu au Allah. Katika nyimbo za ndoa au harusi, walikuwa wanamshukuru Mungu kwa sababu ya ndoa hiyo. Waliamini kuwa ndoa ni kipaji au baraka kutoka kwa Mungu. Walikumbushwa kuwa, kuna wengi ambao waliililia ndoa hiyo ila hawakuipata kwa hivyo wanandoa walihitajika waiheshimu ndoa hiyo kwa hali na mali. Hali kadhalika, waliamini kuwa talaka ni kukufuru. Kukufuru ni hali ya kumkosea Mungu heshima. Walihitajika wavumilie changamoto zozote ambazo wangepitia na wajaribu kusuluhisha migogoro yoyote ili kujiepusha na talaka. Jamii hii ilisema kuwa kuingia katika taasisi ya ndoa ni kufunga pingu za maisha ambapo wanandoa hawakutarajiwa kutoka. Kupitia kwa taswira hisi, maudhui ya dini kupitia kwa yalikuzwa ambapo kuna watu ambao walikuwa na huzuni kwa sababu ya kukosa kufanikiwa kuipata ndoa. Hali kadhalika, mbinu ya istiara imetumiwa kuonyesha jinsi ambavyo talaka ilichukiwa katika jamii hii kwa kutumia msingi wa dini.

Ooh ndoa ni baraka
Ukipata umshukuru Mungu
Kwani kuna wengi wanaoililia

Kwetu talaka kuitoa ni kufuru
Nimefunzwa nivumilie niushinde ujana
Ili kusudi kesho wasinong'one

Punde tu mtoto alipozaliwa, alianza kupokea mafunzo kuhusu dini na umuhimu dini. Mtoto huyu aliambiwa kuwa alistahili kukumbuka kuwa Allah yuko na yeye kila wakati na kila mahali. Walimwambia kuwa ili adumishe uhusiano wa karibu na Allah

alipaswa kuomba au kuswali kila wakati ashikilie desturi hiyo ya dini yao. Maombi hayo yaliambiwa kuwa yangemsaidia kujilinda na kujikinga kutoka kwa maadui na pia kutokana na kuwa mwaminifu kwa Allah angepokea baraka tele.

Kumbuka Allah yupo
Usisahau kuswali
Allah akulinde

4.3.6 Mabadiliko

Mabadiliko ni hali ya mtu au kitu kuwa tofauti na ilivyokuwa hapo wali. Kupitia kwa nyimbo za jadi, mabadiliko yamechimuzwa kwa njia mbalimbali kama ifuataavyo. Katika sherehe za ndoa, wanandoa waliambiwa kuwa wameanza maisha mapya ambapo kila mtu angekuwa na jukumu lake la kutekeleza. Bi. Saida alisema kuwa mwanamke ambaye awali alikuwa ni msichana mdogo aliyekuwa chini ya malezi na maelekezi ya wazazi wake, sasa amekuwa mwanamke ambaye amepata boma lake na alistahili kutekeleza majukumu ya mwanamke wa boma. Kama vile: kupika, kusafisha boma na majukumu mengine yote ya nyumbani. Hali kadhalika, alipaswa kumhudumia mume kwa kila njia na pia kumsaidia mume wake katika kukidhi mahitaji ya familia yao. Kwa upande mwingine mwanamume pia alipata majukumu mapya. Sasa amekuwa mkuu au kiongozi wa boma. Alihitajika kuelekeza na kuiongoza familia yake kwa njia inayofaa. Mwanamume huyo alitarajiwa kufanya maamuzi kuhusu masuala magumu ambayo masuala ni muhimu sana katika ndoa. Kwa hivyo walipoambiwa kuwa wanaanza maisha, ina maana walikuwa wanafungua ukarasa mpya wa maisha yao ambapo wangechukua nafasi mpya na kutekeleza

majukumu ambayo kitambo hayakuwa yao. Katika kujenga maudhui ya mabadiliko ambayo wawili hao walishuhudia, mbinu ya takriri ilitumiwa. Mbinu hii ilitumiwa kuwaonyesha kuwa kutokana na hatua waliochukua, wamefungua ukurasa mpya wa maisha yao. Pia walisisitiziwa kudumu kwa maombi kwa sababu ndoa yao haingefanikiwa bila usaidizi wa Allah.

Leo mnaanza maisha nendeni mkaishi salama
Leo mnaanza maisha nendeni mkaishi salama
Tunawatakia mema na kuwaombea baraka za Allah
Tunawatakia mema na kuwaombea baraka za Allah

Baada ya kifo kutokea familia na jamii kwa jumla ilishuhudia mabadiliko mbalimbali. Watoto waliachwa mayatima kwani wazazi ambao walikuwa wakiwalea wameaga dunia. Wazazi pia walibaki bila watoto wao, wapenzi walibaki wapweke na kwenye lindi la uchungu na jamii ilipoteza viongozi na watu ambao walikuwa wanachangia katika kuikuza jamii. Mapengo haya yote ambayo yaliachwa kutoka na kifo yalifanya watu wabadilisha mitindo yao ya maisha. Katika wimbo huu, mpenzi alifiwa na mpenzi wake. Kutokana na kifo hicho, mpenzi aliyefiwa alihisi kuwa ni mpweke, hakuwa na mtu wa kukimbilia ili amsaidie kukabaliana na kifo hicho. Mtu huyu alitamauka maishani kwa kuwa aliona kila kitu ambacho kinamzingira kimekosa maana. Hata alizungumza na mwezi kwa sababu alihisi kuwa mwezi ulipoteza razini yake na ulimchukia kwa sababu mwezi ungekuwa unampenda hungeruhusu kifo hicho kitokee. Mtu huyo aliona kuwa maisha yake yalijaa kiza totoro. Mbele hakuendeki, hangeweza kurudi nyuma na barabara aliyoitembea alihisi kuwa imekuwa ndefu kupita kiasi. Mtu huyu alishindwa kukubaliana na mabadiliko ambayo yaliletwa na kifo hicho hivyo basi alitamani aage dunia au kwa maneno yake “Nataka nibishe milango ya mbinguni”. Kupitia kwa taswira hisi, mabadiliko ambayo

yalitokea kwa kubaki upweke yalidhihirika. Hali kadhalika, kupitia kwa taswira hisi na uhaishaji, yule ambaye alifiwa alihisi kuwa hakuna kitu kizuri ambacho kimebaki kwenye mazingira ambacho kinampenda kwani alihisi kuwa hata mwezi ulimchukia na ndio sababu kifo kilimfika.

Mwezi umepoteza razini yake?
Nahisi kwamba unanichukia
Nimebaki mpweke sina kimbilio
Natembea barabara ndefu isiyo na mwisho
Natembea barabara ndefu inayopinda

Kadri mtu alivyoendelea kukua katika jamii ndivyo hali yake ya maisha yake ya maisha iliendelea kubadilika. Kupitia kwa wimbo huu, mama alipojifungua salama, alipata furaha ya ajabu. Furaha hii ilitokana na mtoto huyu kumrejesha mama yake katika siku za zilizotangulia. Mama alikiri kuwa siku zake za kisogoni zilikuwa zenye raha na za kutamanika akilinganisha na siku zake za utu uzima. Alipokuwa mtoto, kila kitu kilikuwa kinapendeza sana. Sababu kuu ya maisha ya utotoni kuwa mazuri na ya kupendeza ni kwa kuwa hakukuwa na majukumu yoyote yale kama vile kutafuta riziki au hata kulea. Kazi yake kuu ilikuwa ni kukula na kucheza. Baada ya kukomaa na kuolewa majukumu yake na matarjio ya jamii kwake yalibadilika. Mwanamke huyu alistahili awalee na kuwaelekeza watoto wake njia ambazo zilikubaliwa na utamaduni na dini. Pia alistahili kukidhi mahitaji ya watoto wake. Mojawapo ya mahitaji hayo yalikuwa ni watoto wake wasilale njaa kwa sababu hiyo ingeashiria utetepetevu katika malezi. Mwisho kabisa mama huyu alistahili kutelekeza majukumu ya ndoa, alistahili kuhakikisha kuwa mume ni safi, amsinge na kutelekeza majukumu mbalimbali ambayo yangemfanya mume aridhike ili asiwe na jicho la nje.

Kutokana na kuwa na majukumu mengi katika utu uzima, mama huyu alikosa tabasamu na raha aliyokuwa nayo utotoni. Kwani muda wake mwingi aliutumia katika kuihudumia familia yake ili isisambaratike. Mabadiliko ambayo yalishuhudiwa katika maisha ya mama ya mtoto yalifafanuliwa kupitia kwa mbinu ya kisengere nyuma ambapo mama huyo alikumbuka na kutamani siku zake za utotoni. Hali kadhalika, mbinu ya tashbihi ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo maisha ya utotoni yalikuwa mazuri.

*Tabasamu lako mwanagu
Lanirudisha kwenye siku zangu zile za utotoni
Wakati kila kitu kilikuwa kinang'aa
Kinang'aa kama jua angani
Ninapoutaza uso wako mwanangu
Wanirejesha kwenye enzi zetu za zama*

Kama jamii nyingi za Kiafrika, jamii ya Waswahili iliheshimu jando. Waliamini kuwa mvulana akipitia jandoni baada ya hapo angekuwa tayari kukabiliana na majabali ya maisha kwa sababu angekuwa amepeokea kungwi za jinsi ya kukabiliana na hali mbalimbali. Baada ya wavulana kuwasili kutoka jandoni, walirejelewa kama simba. Waliitwa simba kwa sababu sasa wao si watoto wadogo bali ni wanaume. Pili kwa sababu walidhihirisha ujasiri wakati ambapo walikuwa wakikabiliana na kisu cha ngariba na mwisho ni kwa sababu sasa walichukua nafasi mpya katika jamii. Wavulana hawa wangekuwa na nafasi ya kuongoza jamii hasa katika vita na kudumisha usalama. Kwa hivyo wale watoto ambao waliingia jandoni wakiwa waoga sasa hawapo tena. Wavulana hawa sasa wangekuwa ngao na mkuki wa ukoo wao. Wanajamii walikumbushwa kuwaheshimu wavulana hao kwa sababu walipanda cheo.

Kupitia kwa mbinu ya jazanda, mabadiliko ambayo vijana waliokuwa jandoni walishuhudia yalishughulikiwa kwa kina. Vijana ambao walikuwa waoga kama kungururu baada ya kutoka jandoni vijana hao waliitwa simba. Simba ni mnyama hatari ambaye aliaminiwa kuwa haogopi chochote. Hali kadhalikia, mabadiliko ambayo vijana hao walishuhudia, yalisistizwa kwa kutumia mbinu ya takriri. Hivyo wanajamii walihimizwa kuwapa vijana hao heshima ambayo walikuwa wanastahili kupewa.

Sasa ndio wamefika, simba kutoka mwituni
Sasa ndio wamefika, simba kutoka mwituni
Wao si watoto tena, bali wamekuwa wanaume
Wao si watoto tena, bali wamekuwa simba
Wamerudi sasa simba kutoka mwituni

4.3.7 Nafasi ya Vijana kwenye Jamii

Kulingana na Umoja wa Mataifa (2024), kijana ni mtu yeyote awe ni wa kiume au kike wa kati ya miaka kumi na mitano na ishirini na minne kwa sababu za kitakwimu. Ila wanasema kuwa kila nchi ina uhuru wa kuamua vijana ni wa umri upi. Kulingana na Katiba ya Kenya (2010), inakubaliana na maelezo ya Lubeleje na Mmassay katika kifungu cha mia mbili sitini (260) kuwa kijana ni mtu wa jinsia yoyote ile aliye kati ya miaka kumi na mitano na thelathini na nne. Umoja wa Kitaifa umetambua mchango mkubwa wa vijana katika kuziendeleza jamii zao mbalimbali ambazo zimekumbwa na changamoto nyingi kwa kutenga tarehe 12 Agosti kila mwaka kuwa siku ya vijana duniani. Vivyo hivyo, katika jamii ya Waswahili vijana hawajaachwa

nyuma. Walitoa mchango mkubwa katika jamii yao na pia jamii iliwatarajia watoe michango zaidi aushini mwao.

Kijana alisawiriwa kama mtu ambaye ni mtiifu sana. Utiifu wa vijana ulidhihirika hasa walipokuwa jandoni wakitayarishwa kwa kuhusu maisha ya utu uzima na pia walipotayarishwa kwa maisha ndoa. Wanajamii wenye hekima na walioheshimiwa walipewa jukumu la kuwaelekeza vijana kuhusu mambo ambayo walistahili kuyafanya na yale ambayo walistahili kuyaepuka. Walifunzwa kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa sababu iwapo wangekosa kufanya kazi wangeumia kwa sababu ya njaa. Mwanamume alifunzwa majukumu yake aliyostahili kuyatekeleza kama mume na kiongozi wa familia na mwanamke alifunzwa mambo aliyopaswa kuyatekeleza kama bibi wa boma. Kupitia kwa kisengere nyuma, vijana wamesawiriwa kama watu ambao ni watiifu kwa sababu walikumbuka kuhusu yale waliyofunzwa wakitayarishwa kwa ajili ya ndoa.

Ahsante mama, ulinifunza nikajua
Baba akasema kuomba ni mwiko
Raha ya chumvi ni kunua

Mwanamke lazima awe safi
Kanga alisugue
Mume akirudi sharti viatu kumvua

Pia wawili hawa walistahili kufuata maagizo ya jinsi ya kuijenga ndoa yao ili waepuke talaka. Kupitia kwa takriri, wawili hawa walikumbushwa kuhusu umuhimu wa kuitunza ndoa yao. Jamii hii iliamini kuwa talaka ni kufuru au pia ni laana.

Wazazi na wanajamii walipohudhuria sherehe ya ndoa, walikuwa na matumaini kuwa wawili hawa wangetii mafunzo yao kama vile kutofikiria kuhusu talaka.

Kwetu talaka kuitoa ni kufuru
Nimefunzwa nivumilie niushinde ujana

Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kitawatenga
Mkaahidi kupendana milele kwani kifo ndicho kitawatenga

Kijana alisawiriwa kama mtu mwenye bidii. Baada ya mtoto kuzaliwa, kuna baadhi ya nyimbo ambazo mtoto huyo aliimbiwa. Baadhi ya nyimbo hizo zilionyesha matarajio ya jamii kwa mtoto huyo. Alipotimiza umri wa miaka kumi na mitatu, wazazi au walezi wake walianza kumfunza majukumu mbalimbali kama vile: kuenda shambani, kuvuna minazi na kuenda baharini kuvua. Alipotimiza umri wa miaka kumi na sita, kijana huyo alitarajiwa kujiunga na wanaume wengine ili kutekeleza majukumu hayo. Iliaminiwa kuwa akishiriki katika shuguli za kuikimu familia yake kabla ya kuo baasi akitimiza umri wa kuo hangeshindwa kukidhi mahitaji ya familia yake. Kupitia kwa kisengere mbele, mtoto anafunzwa kuhusu majukumu ambayo yalikuwa yakimsubiri. Isitoshe, kupitia kwa taswira sikivu kijana huyo na wanaume wengine kwenye familia yao walikuwa wakiamka asubuhi ili kuenda shambani kulima kabla ya jua kuwa kali.

Naingoja siku ambayo utakuwa duma
Siku ambayo utaingia baharini
Uende ukavue ulete dagaaa

Kumekucha jogoo tayari amewika
Tuende shmbani tukalime
Kabla ya jua kuzidi
Tuende tukapalilie mahindi
Shamba letu limejaa

Kijana alitarajiwa awe ni mtu mwenye heshima kwa wote na mwadilifu. Kulingana na TUKI (2019), wanasema kuwa mtu mwadilifu ni yule anayetenda haki bila kupendelea upande wowote. Mama na walezi wake walitarajia kijana huyo awe ni mtu mwenye maadili na mwenye heshima kwa watu wote bila kutumia vipimo au misingi yoyote ile. Awe ni mwenye kuheshimu kila mtu kwenye jamii kuanzia mtoto mdogo hadi mtu mkongwe. Pia alitarajiwa kuwa kabla ya kuingia kwenye ndoa, ahakikishe amemtafuta mwanamke aliyempenda ili ndoa yao iwe ya furaha. Kupitia kwa kisengere mbele, mtoto alifunzwa kuhusu maadili aliyotarajiwa kudumisha wakati ambapo angekuwa kijana. Hali kadhalika, kupitia kwa tashbihi anafunzwa kuhusu maisha ya ndoa ingawa bado alikuwa na miaka kabla ya ndoa yenyewe kufika.

Kijana alisawiriwa kama mtu ambaye ni jasiri. Baada ya wavulana kutoka jandoni, jamii iliwachukulia kama watu ambao walikuwa majagina. Jamii iliwafananisha na simba, simba ni mnyama ambaye ni mkali na haogopi jambo lolote lile. Wavulana hawa walitarajiwa kuonyesha kuwa wana uwezo wa kuenda kupigana na kuikinga familia kutoka kwa maadui. Kando na hilo, wavulana hawa walistahili kuonyesha kuwa wana uwezo wa kuongoza familia yao hasa kupitia kwa matendo yao, maneno yao na uhusiano wao na watu wengine kwenye jamii. Vijana hao pia walikumbushwa kuwa wakati wa kuingia jandoni wangekumbana na kisu cha ngariba ambacho kingewasababishia uchungu mwingi sana ila walionywa kuwa hawakuwa na nafasi ya kumwaga hata tone la chozi. Walistahitahili kuuvumilia uchungu huo kwa sababu hiyo ndiyo ingedhihirisha kuwa wamekomaa. Hali kadhalika, wavulana hao

walitarajiwa kuwa wapole. Jamii hii iliamini kuwa baada ya kutoka jandoni wavulana walistahili kuwa watulivu au wanyamavu. Tabia ya kusema sana waliambiwa kuwa ni ya wanawake. Hisia za mwanamume zilisastahili kufumbatwa. Kupitia kwa taswira hisi nafasi ya vijana kuwa Jasiri ilibainishwa. Kwani waliambiwa kuwa kisu cha ngariba ni kichungu ila hawakustahili kumwaga hata tone la chozi. Aidha, kupitia kwa takriri ujasiri wa vijana hao ulidhihirishwa waliporejelewa kama simba kutoka mwituni.

Kuwa tayari kukutana na kisu cha ngariba
Kilicho na makali kuwili
Ingawa uchungu ni mwingi sana
Huna nafasi ya kumwaga tone la chozi

Sasa ndo wamefika simba kutoka mwituni
Sasa ndo wamefika simba kutoka mwituni
Wao si watoto tena bali wamkuwa wanamume
Wanaume sasa, wao ni simba kutoka mwituni

4.4 Hitimisho

Sura hii ilingazia jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilivyotumiwa katika kuendeleza maudhui. Maudhui kama vile kazi katika jamii ya Wakisii yalishughulikiwa kupitia kwa mbinu ya takriri. Wakisii walijishughulisha na kilimo cha vyakula mbalimbali kama vile: njugu, wimbi, mboga na mahindi. Hii ilikuwa shughuli muhimu sana ya kiuchumi ambayo iliwasaidia kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Kando na hilo, mabadiliko yalishughulikiwa hasa baada ya wavulana kutoka jandoni. Wavulana hawa walirejelewa kama dume. Maudhui ya ndoa pia yalishughulikiwa ambapo wanandoa walikumbushwa umuhimu wa ndoa. Wanaume walionywa kutowatalikia wake zao kwa sababu angentaliki mke wake jamii ingemfukuza. Maudhui mengine ambayo tulishughulikia ni nafasi ya mwanamke kwenye jamii ambapo mwanamke alistahili kufanya kazi mahususi kama kuteka maji na kuenda shambani. Tulishughulikia taasubi ya kiume ambapo tulibaini kuwa wanandoa walishinikizwa

wapate watoto wa kiume kwa sababu yeye ndiye aliyeaminiwa kuwa angeendeleza kizazi chao. Kwa upande mwingine katika nyimbo za jadi za maudhui ya malezi yalidhihirika. Mwanamke aliaminiwa kuwa yeye ndiye mwalimu wa kwanza wa mtoto huyo. Walimfunza mtoto huyo mchanga kuhusu tamu na chungu ya maisha. Hali kadhalika, maudhui ya uwajibikaji tuliyashughulikia kwa kina ambapo wanajamii walikumbushwa kuwajibika katika jambo lolote lile walilokuwa wakifanya. Tuliyaangazia maudhui ya utamaushi ambapo baadhi ya wanajamii walitamaushwa na changamoto mbalimbali za maisha kama vile kifo. Hali kadhalika, mwanamke alipewa jukumu la kuiendeleza ndoa yake. Alitahadharishwa kuwa mahasidi ni wangi na hivyo alikuwa na jukumu la kumshughulikia mume wake vizuri ili kumzuia asiwe na jicho la nje. Waliamini kuwa chochote kilichokuwa kikifanyika duniani kilikuwa ni Majaaliwa ya Mungu. Hulka na mienendo yao ilipaswa kulingana na sheria za Mungu hivyo ndivyo wangepata baraka za Mungu. Vijana pia walichorwa kuwa wao ni watu muhimu sana katika jamii, walitarajiwa katika kazi yoyote ile waliyokuwa wakifanya kwa sababu wao ndio viongozi wa kesho. Katika sura inayofuata, tuliangazia

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Sura hii ya tano ni hitimisho la utafiti huu. Muhtasari wa sura zote zilizotangulia umetolewa. Aidha, tumeshughulikia matokeo ya utafiti ambayo tumejadili kwa kina kulingana na malengo na maswali ya utafiti. Isitoshe, tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kubainisha jinsi ambavyo watunzi wametumia mbinu za mtindo katika nyimbo za jadi ili kusawiri historia na tamaduni za jamii ya Wakisiii na Waswahili wa Kenya. Hali kadhalika, ulilenga kuonyesha mbinu za mtindo zilizotumika kwenye nyimbo za jadi za jamii teule na mwisho tulichunguza jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilitumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Katika kufikia malengo ya utafiti huu, tasnifu hii imegawa katika sura tano.

Sura ya kwanza ilishughulikia msingi wa suala la utafiti. Kutokana na usuli wa mada, tuliweza kuangazia nyimbo kwa jumla, aina za nyimbo na baadhi ya tafiti ambazo zimeshughulikia kipera cha nyimbo. Hapo ndipo tuliweza kubaini kuna pengo ambalo lilstahili kuzibwa na utafiti huu. Aidha, tulidhihirisha malengo ya utafiti huu na maswali ambayo yalituongoza katika utafiti wetu. Mbali na hayo, tuliangazia sababu za kufanya utafiti huu na je, utafiti huu ungekuwa na umuhimu gani katika uwanja wa fasihi? Pia tuliafafanua upeo na mipaka ya utafiti huu na misingi ya nadharia ambapo mihimili ya nadharia ya mtindo ilitumiwa katika kufikia malengo ya utafiti. Tulipitia

maandishi na tafiti mbalimbali ambazo zimeshughulikia kipera cha nyimbo na kuonyesha jinsi ambavyo tafiti hizo zinatofautiana na utafiti wetu. Kwa jumla sura hii ndiyo ilikuwa mwongozo wa utafiti wetu.

Sura ya pili ilianguzia jinsi ambavyo mbinu za kimtindo zilitumika kusawiri historia na tamaduni za jamii teule kupitia kwa nyimbo za jadi. Mambo mbalimbali yalishughulikiwa kama maana ya historia na maana ya tamaduni. Tulishughulikia historia ya Wakisii kama vile janga la njaa liliwakumba, vita vya kwanza vya dunia na migogoro kati ya Wakisii na majirani zao. Hali kadhalika, tulianguzia tamaduni za jamii teule kama vile: tohara, ndoa, kazi, na taarabu kwa jamii ya Waswahili pamoja na biashara zao hasa katika bahari Hindi.

Katika sura ya tatu tulizihakiki mbinu mbalimbali za kimtindo katika nyimbo teule na ujumbe unaowasilishwa kupitia kwa nyimbo. Tulihakiki mbinu kama vile: jazanda, taswira, takriri, kisengere nyumba, tashihisi, tashibihi na chuku. Pia tulionyesha jinsi ambavyo mihimili ya nadharia ya mtindo imetumiwa kuchunguza mbinu hizi.

Sura ya nne ilichunguza maudhui yanayochimuzwa kupitia kwa mbinu za kimtindo. Baadhi ya maudhui ambayo tulianguzia ni pamoja na taasubi ya kiume, ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii, nafasi ya vijana katika jamii, uwajaibikaji, mabadiliko, malezi, migogoro, utamaushi na kifo.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Malengo haya ndiyo yalituongoza katika kukusanya data yetu. Lengo la kwanza lilikuwa ni kubainisha jinsi ambavyo mbinu za mtindo zilitumiwa na watunzi katika kusawiri tamaduni na historia za jamii ya Wakisii na Waswahili. Lengo la pili lilikuwa ni kubainisha mbinu za mtindo

zilizotumiwa kwenye nyimbo za jadi za jamii teule. Nalo lengo la tatu lilikuwa ni kuchunguza jinsi ambavyo mbinu za lugha zilivyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Kutokana na utafiti utafiti wetu, tulidhihirisha jinsi ambavyo mbinu za mtindo zimetumiwa kusawiri historia na tamaduni. Kupitia kwa takriri, njaa ambayo iliathiri jamii ya Wakisii kati ya mwaka wa 1888-1892 na mwaka wa 1914-1918 ilidhihirika. Kutokana na janga hili la njaa, Wakisii wengi waliaga dunia. Mbinu hii ya takriri ilitumiwa kuisisitiza umuhimu wa kuhifadhi na kutumia mavuno au mazao yao vizuri. Mazao hayo yawe machache au mengi hawapaswi kuyatumia vibaya kwa sababu hawajui kesho yao itakuwa vipi.

Isitoshe, tuliangazia Vita vya Kwanza vya Dunia na athari ya vita hivyo kwa Wakisii kwa sababu walichangia katika kupigana vita hivyo. Kupitia kwa kisengere nyuma, tunaambiwa kuwa *Abatureti* (wazee wa Kijiji) walichangia katika kutekwa nyara kwa vijana barubaru na wanaume wenye nguvu ambao walienda kupigana. Wanajamii walihisi kuwa viongozi wao waliwasaliti kwani jukumu la viongozi ni kuhakikisha kuwa raia wako salama. Aidha, kutokana na tamaa ya bidhaa za viwandani walizopewa na wazungu walihari kuwasaliti watu wao.

Hali kadhalika, mgogoro kati ya Wakisii, Wakipsigis na Wamaasai pia ulidhihirishwa. Kupitia kwa utafiti huu, tulibaini kuwa mbinu ya taswira ilitumiwa konyesha jinsi ambavyo wavulana ambao waliotoka jandoni walikuwa wakihamasishwa waende kupigania jamii yao. Vijana hao walitakiwa waende warudishe ng'ombe na mifugo wengine ambao walichukuliwa na Wakipsigis. Wanajamii kupitia kwa mbinu ya takriri waliambiwa wanoe silaha mbalimbali ambazo wavulana wangetumia.

Tohara pia ni tamaduni muhimu katika jamii ya Wakisii. Ili mtoto mvulana aheshimiwe na kila mtu, ni lazima aende jandoni. Pale jandoni, walifundishwa mambo mbalimbali kuhusu maisha hasa ya utu uzima. Pale ndipo walipofunzwa tamaduni na siri za jamii yao. Kupitia kwa nyimbo, wanajamii waliambiwa wawaheshimu wavulana hao. Akina mama wa wavulana hao walikumbushwa kuwa sasa wavulana hao wamekuwa wanaume hivyo hawastahili kuwatuma mtoni kwa sababu hizo hazikuwa kazi zao tena. Jukumu lao sasa lilikuwa ni kuilinda jamii. Kilimo pia kilikuwa ni shughuli muhimu katika jamii ya Wakisii. Kupitia kwa utafiti huu tulidhihirisha kuwa walishiriki katika kilimo ainati kama vile: kilimo cha mahindi, waimbi, ndizi, viazi vitamu na mtamu. Mimea hii ilitumiwa kama vyakula na ingine waliuzia majirani wao kama vile Waluo.

Kwa upande mwingine, tuliangazia tamaduni na historia za jamii ya Waswahili. Katika utafiti wetu, tulibaini kuwa ndoa ni taasisi muhimu sana. Umuhimu wa ndoa ilidhihirishwa kupitia kwa mbinu mbalimbali kama vile: jazanda, kisengere nyuma na taswira. Waliamini kuwa ndoa ni pingu za maisha kwa hivyo walionywa kuwa wakiingia katika taasisi hiyo, hakukuwa na nafasi ya talaka. Wanandoa walihimizwa wafanye juu chini ili ndoa yao ifanikiwe.

Tulibaini kuwa tohara ni muhimu sana katika jamii. Pale jandoni ndio wavulana walipofunzwa kungwi dume au mambo ya utu uzima. Wavulana walikumbushwa kuwa sasa wao si watoto tena. Kupitia kwa nyimbo waliambiwa kuwa wamekuwa wanaume hivyo matendo yai yalistahili kuonyesha hivyo. Kwa mfano, walikanywa dhidi ya kusemasema kwa sababu hiyo iliaminiwa kuwa kusema sana kulikuwa tabia ya wanawake. Pili, walikumbushwa wasikimbilie kugusa vitu vya mama zao na pia

hawakupaswa kuingia kwenye chumba cha malazi ya wazazi wao kwa sababu wangeona vitu ambavyo hawakustahili kuona.

Tulibaini kuwa Taarabu ni nyimbo ambazo zilikuwa maarufu sana katika jamii ya Pwani ya Afrika Mashariki. Tulibaini kuwa taarabu zilitumia mchanganyiko wa mziki wa Kiarabu, Kihindi na Kizungu. Taarabu ilikuwa njia mojawapo kuu ya burudani kwa Waswahili. Nyimbo hizi zilikuwa zikiimbwa katika sherehe mbalimbali za kitamaduni kama vile ndoa ambapo zilitumiwa kuwaelimisha wawili hawa kuhusu maisha ndoa, kuzaliwa kwa watoto ambapo zilitumiwa kudhihirisha furaha yao na pia kuwafunza watoto kuhusu maisha ya utu uzima. Mwisho kabisa, ziliimbwa katika sherehe za mazishi ambapo zilitumiwa kuwafariji waliofiwa na wapenzi wao.

Isitoshe, tuliangazia jinsi ambavyo mbinu mbalimbali za mtindo zilivyotumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa nyimbo hizo katika nyimbo za Wakisii. Walitumia jazanda kuonyesha furaha yao hasa baada ya mtoto wa kiume kuzaliwa. Pia walitumia jazanda kuonyesha mabadiliko ambayo vijana walioenda jandoni walishuhudia. Tulibaini kuwa mbinu ya tashihishi pia ilitumiwa kwa kiasi kukubwa katika kufafanua kuhusu mazao yaliyonawiri shambani. Walisema kuwa wimbi ulikodoa macho hivyo basi walihitajika kuenda kuvuna.

Fauka ya haya, mbinu ya taswira ilitumiwa kwa asilimia kubwa katika nyimbo hizi. Taswira hizi ilitumiwa kuonyesha hisia za furaha kutokana na kuzaliwa kwa mtoto. Taswira uoni pia ilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo mazao yalikuwa yanapendeza shambani hivyo kuwahimiza wakulima waende kuvuna. Hali kadhalika, walitumia taswira hii kusisitiza kuwa wanawake ambao ni wavivu wapewe shamba lenye magugu ili waende wakalime.

Utafiti huu ulibainisha kuwa tashbihi ilitumiwa kwa njia mbalimbali. Kwanza ilitumiwa kufananisha wavulana ambao walitoka jandoni kama simba hivyo basi wanajamii walistahili kuwaheshimu. Takriri pia ilitumiwa kusesitiza kuhusu madhara ya njaa kwenye jamii hivyo wanajamii walistahili kulinda mazao yao kwa ajili ya siku za usoni. Kwa upande mwingine chuku ilitumiwa kusesitiza majonzi na huzuni ulioletwa na kifo kupitia kwa hiyo chuku pia walifarijiwa na kuambiwa waridhie kifo.

Zaidi ya hayo, jamii ya Waswahili pia ilidhiirisha utajiri wao wa matumizi ya mbinu za mtindo kupitia kwa nyimbo za jadi. Walitumia taswira katika kuonyesha mambo ambayo mwanamke alistahili kumfanyia mume wake punde tu akifika nyumbani kama kumvua viatu na hata kumkanda. Taswira hii ilitumiwa kuonyesha hisia za furaha ya jamii kutokana na ndoa. Wanajamii walitakia mema katika maisha yao. Tashihisi ni mbinu nyingine ambayo tulibaini kuwa ilitumiwa kuonyesha utamaushi hasa baada ya mtu kufiwa na mpendwa wake. Walitaka kujua ikiwa mwezi ulikuwa umepoteza razini. Tulibaini kuwa jazanda ni mbinu ambayo ilitumiwa na wazee na akina mama katika kuwafunza waliokaribia ndoa kuhusu kungwi za ndoa. Mwanamke alikumbushwa kuwa alistahili kufanya jambo lolote lile ile amvutie mume wake. Kupitia kwa jazanda, watu wavivu walihimizwa wawe kama njiwa ambaye hujenga kiota chake wakati wa jua kisha mvua ikinyesha anajikinga. Tulibaini kuwa kisengere nyuma kilitumiwa na akina mama katika nyimbo za kusherehekea kuzaliwa kwa watoto ili kuonyesha furaha yao. Walitumia mbinu ya takriri katika nyimbo za ndoa ili kusesitiza umuhimu wa kuheshimu taasisi ya ndoa kwa sababu ililinganishwa na pingu za maisha. Wawili hawa waliambiwa kuwa hawapaswi kutengana kwa sababu yoyote ile. Pia mbinu hii ilitumiwa kuonyesha furaha ya wanajamii kwa sababu walipiga hatua muhimu sana maishani mwao.

